# بناء المجتمع المدني
# وتنميته في السيرة النبوية

## ترجمة اللغة السواحلية

تاليف

**أ. د. عبد العزيز بن إبراهيم العُمري**

أستاذ السيرة النبوية

بجامعة الإمام محمد بن سعود الإسلامية بالرياض (سابقًا)

الطبعة الأولى

**KUJENGA JAMII YA KIRAIA NA KUIKUZA KATIKA SERA YA MTUME.**

# KUJENGA JAMII YA KIRAIA NA KUIKUZA

# KATIKA SERA YA MTUME.

**UTUNZI WA**:

USTADH/DOCTOR ABDUL-ZIIZ IBN IBRAHIIM AL-UMARY

USTADH MSTAAFU WA SERA YA MTUME KATIKA CHUO KIKUU CHA KIISLAMU CHA IMAM MUHAMMAD IBN SAUD RIYADH

**KIMETAFSIRIWA KWA KISWAHILI NA:**

MUHUDHAR MUHAMMAD OMAR (NADWIY).

CHAPA YA KWANZA.

**© Abdul-aziiz Ibrahim al-Umariy, 2025**

**Al-Umariy, Abdul-aziiz Ibrahim**

**Kujenga jamii ya kiraia na kuikuza katika sera ya Mtume. / Abdulaziiz Ibrahim al-Umariy- 1. –Riyadh, 2025**

**120p; 21x14 cm**

**L.D. no. 1446/16123**

**ISBN: 978-603-05-6500-9**

بسم الله الرحمن الرحيم

**KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU**

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuweko kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao Aliyowapendelea na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo basi hao ndio wavunjao amri zetu".

Qur'ani tukufu, Suratun-Nuur aya (55).

**KUJENGA JAMII YA KIRAIA NA KUIKUZA KATIKA SERA YA MTUME.**

# FAHARASA

DIBAJI ........ 9

UTANGULIZI........ 14

MKATABA WA MADINA........ 16

KUUKUZA MJI WA MADINA NA JAMII YAKE ........ 19

KUBADILISHA JINA LA MJI WA MADINA ........ 19

MAPENZI YA MADINA NA KUIFANYA KUWA MJI MTUKUFU ........ 21

KUJENGWA KWA MSIKITI WA MTUME (SWALLALLWAAHU ALAIHI WASALLAM). ........ 24

MAENDELEO YA IDADI YA WATU NA UWIYANO WAKE ........ 26

UKUAJI WA MAENDELEO YA KIROHO. ........ 29

UKUAJI WA KIELIMU ........ 31

UKUAJI WA KIJAMII ........ 38

UKUAJI WA MAENDELEO YA KIAFYA ........ 43

UKUAJI WA MAENDELEO YA KIUCHUMI........ 47

UKUAJI WA MAENDELEO YA KIBIASHARA ........ 49

URATIBU WA SERIKALI NA UGAWAJI WA MAJUKUMU. ........ 52

UADILIFU NA USAWA ........ 56

KUPANGILIA AMANI NA USALAMA ........ 64

UJENGAJI WA TABIA NA MAADILI ........ 72

HITIMISHO........ 109

**KUJENGA JAMII YA KIRAIA NA KUIKUZA KATIKA SERA YA MTUME.**

# DIBAJI

Ziko juhudi aina tofauti za kuifahamisha (kuijulisha) maana ya jamii ya kiraia. Maana yake ya kiasili ni jamii inayohukumiwa na kanuni chini ya utawala (uongozi) wa dola.

Kwa hakika mwanadamu anajihusisha na njia tofauti za kazi na maisha yake, pamoja na kupatikana wengine wengi wanaojihimu na jamii, wanakuwa na maandalizi ya kuyapangilia (maisha ya kijamii) pamoja na kujitolea kuwafaidisha watu.

Kuitwa jamii ya kiraia, neno hilo linanasibishwa na mji, na kutoka tamko hilo ndiko kulikotoholewa neno umiji na utamaduni, nako nikujilazimisha na kufata sababu za maendeleo, kwa hivyo uraia, –ni mkusanyiko wa watu katika nidhamu na majukumu-. Tokea kutumwa kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) ilikuwa inaeleweka kuwa yeye alikuwa ana pupa ya kueneza ibada ya kuabudiwa Mwenyezi Mungu mmoja na kumpwekesha na kusimamisha dola yenye huruma na nidhamu, yenye uadilifu inayotekeleza amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya waja wake kwa kila aina ya huruma na uadilifu. Na tokea siku za mwanzo za ulinganizi wa uislamu katika mji wa Makka, Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anawabashiria (kuwapa habari njema) maswahaba wake kuhusu kuenea kwa uislamu sehemu zote za ulimwengu na kushinda kwake na kutawala kwa mipangilio yake tofauiti. Na mji wa Makka na miji iliyo pambizoni mwa hizo ambako ujumbe wa uislamu ulianza, ulikua ni mji uliosimama kwa ada na desturi ambazo nyingi miongoni mwa hizo ni za kidhalimu, hakuna sharia maalumu wala nidhamu iliyoasisiwa (iliyojengwa na kupangiliwa) kijamii, wala hakukuweko na uamuzi wenye uadilifu.

Ndipo ulipokuja uislamu, ukaja na kuhifadhi haki ya Mwenyezi Mungu na haki za waja wake kwa mambo yenye huruma, uadilifu na usawa, pamoja na zile dharura tano kama alivyozitaja imam Ghazaaliy katika kitabu chake "*Al- mustasfaa*" na Ashaatwibiy katika "*Al-muwafaqaat*" na kufanya wema katika kila kitu pamoja na siasa ya ndani na ya nje, inayochunga mambo yanayosimamia jamii yoyote ya kiraia iliyoendelea. Na wakati jambo la kuigeuza jamii ya mji wa Makka kuwa jamii na dola ya kiislamu lilipokuwa gumu kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam), alianza kutafuta watu katika makabila na miji mingine ambao watamsaidia katika sehemu inayofaa, watu wenye kuitia nguvu dola ya kiislamu ambayo waislamu wataishi katika jamii hiyo ya kibinadamu na ya kiislamu, yenye amani na kusaidiana. Wasaidiane katika kujenga uma ambao unazishinda uma mwengine unaofungamana na Mwenyezi Mungu (Mtukufu) na sharia yake, ili uwaongoze wanadamu kunako utukufu na ukamilifu. Pia uma huo uifanyie usawa nafsi yake na watu wa dini nyengine katika wanaotaka maisha mazuri.

Mtume (Alaihissalaam) akaanza kuijulisha nafsi yake kwa makabila tofauti wakati wa misimu ya waarabu akawa anatafuta wenye kumnusuru ili asimamishe jamii yenye uwezo wa kujipangia mambo yake na kutetea uwepo wake mbele ya maadui. Na kwa msaada wa kimungu, Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alipata lile analolitaka kwa ma Answaar miongoni mwa watu wa mji wa Madina waliomjia katika msimu wa hijja wakamsikiza na wakamsadiki, wakajiandaa kuufanya mji wao ndio kituo cha daawa na dola yake inayotarajiwa na jamii ya kiislamu yenye amani, wawe ni wenye kumnusuru na kumtia nguvu katika yale yanayotakikana katika nidhamu na mpangilio,

mpangilio wa kimtume katika mambo ya kiidara na wadhifa wa uma na kuipangilia dola na yale yaliyokusanywa na mpangilio huo katika mifano ya sera na sunna, ndio msigi ulioangaziwa katika mipangilio ya uislamu na idara ya dola na jamii yake.

Maswahaba wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) walikuwa wakidhulumiwa katika mji wa Makka, naye akawa anawasubirisha na kuwabashiria yakwamba itafika siku ambayo dhuluma itazuiwa na uadilifu utatawalishwa, sio katika mji wa Makka peke yake, hilo litakuwa katika sehemu nyingi wanazozijua. Wakati Khabbaabu ibn al-Arat alipomshtakia yale yaliyokuwa yanampata katika maudhi na kumtaka awaombee mabaya wale waliomdhulumu, alimwambia: “Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu (Mtukufu) jambo hili litakamilika hadi aliepanda mnyama atembee kutoka San,aa hadi Hadhramaut, hana analoogopa isipokuwa Mwenyezi Mungu na mbwa mwitu juu ya mbuzi wake, lakini nyinyi mna haraka”.[1]

Ahadi ya Mwenyezi Mungu ilikuwa ni kuupa ushindi uislamu na kuwatawalisha waislamu juu ya ardhi na kuwapa umakinifu, hilo linamaanisha kusimama mpangilio na nidhamu, ambao kwa mpangilio huo, utapatikana uhakika wa utulivu unaokusanya kati ya kuweka sharia na kuitekeleza katika maisha kupitia siasa ya dunia ikifuatishwa na dini. Ahadi hii ilikuwa iko wazi kama ilivyo

---

[1] Ameipokea imamu Bukhari katika sahihi yake Kitaabul-maghaaziy mlango wa “yale yaliyompata Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasallam) na maswahaba wake kutoka kwa washirikina katika mji wa Makka. Juz 5 uk 238.

katika neno lake Mwenyezi Mungu: (Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoi mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuweko kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri zetu). Suratu An-nur aya 55. Kuwafanya makhalifa katika ardhi, inamaanisha kuwapa uwezo wa kutekeleza hukumu yake, mpangilio wa kisiasa na idara zake.

Kwa hakika ilikuwa bayana kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) yakwamba nidhamu ya kiislamu ya kisiasa aliyoiwekea misingi yake itairithi mipangilio ya kilimwegu ya kileo, kama mpangilio wa utawala wa Kisra katika nchi ya Fursi, na ya Kaisari katika nchi ya Rome.

Swahaba wa Mtume Jabir ibn-Samura (Radhwallwaahu anhu) amepokea yakwamba Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) Alisema: “Kundi moja miongoni mwa makundi ya waislamu au waumini (kama ilivyo katika riwaya nyingine) wataifungua hazina ya Kisra iliyoko katika kasri jeupe”.[2]

Pia alisema wakati akilipiga jiwe (kulivunja) akiwa anachimba Khandak, “Allwaahu-Akbar, nimepokea funguo za Sham, Wallwaahi mimi ninayaona majumba yake mekundu kutoka hapa nilipo”, kisha alisema “Bismillaahi” Akalipiga jiwe jingine -lililokuwa gumu limezuia kuchimbika-, akavunja thuluthi ya lile jiwe, Akasema: “Allwaahu-Akbar, nimepewa funguo za Fursi,

[2] Angalia ibn Ishaaq, Assiratun-Nabawiyyah uk. 271.

Wallwaahi nauona mji wa Madaain na nayaona makasri yake meupe kutoka hapa nilipo”. Kisha Akasema : “Bismillaah”, Akalipiga pigo jengine, likan’goka lile jiwe lililokuwa limebaki, Akasema: “Allwaahu-Akbar, nimepewa funguo za Yaman, Wallwaahi ninaiona milango ya San,aa kutoka hapa nilipo”.[3]

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa akiwalea maswahaba wake kwa kuwajulisha juu ya upeo utakaofikia dola ya kiislamu, hadi kufika sehemu mbali mbali za ardhi katika nidhamu ya taasisi ya kidini, kiidara na kisiasa.

Tokea siku za mwanzo za ulinganizi wake, Mtume alikuwa na pupa ya kuona kusimama kwa dola yenye nidhamu ya kibinadamu inayowapangia watu na kuwapeleka kunako uadilifu na usawa, nae -rehema na amani zimfikie- alikuwa anashikilia nafasi ya juu katika uongozi katika dola ya kiislamu pamoja na utukufu wa utume na ujumbe wake kwa wakati mmoja. Aidha aliwaandaa maswahaba wake juu ya kuupangilia ulimwengu wote na kusimamisha tawhidi na uadilifu baada ya kuondoka kwake (Swallallwaahu Alaihi asallaam).

[3] Ameipokea imam Ahmad katika Musnad yake juz 4 uk 303, na idadi kubwa ya wanachuoni wameifanya kuwa ni hadithi hasan akiwemo ibn Hajar. Angalia Dr Akram Dhwiyaaul-Umariy Assiiratun,Nabawiyya juz ya 2 uk 432. Na Dr Mahdiy Rizqullah Ahmad katika Assiiratun-Nabawiyya kupitia vitabu vya asili masomo ya kupambanua uk 449, Hamish 42.

## UTANGULIZI

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu (Mtukufu) rehema na amani zimfikie mjumbe wa Mwenyezi Mungu, pamoja na jamaa zake na maswahaba wake na watakaofuatia.

Baada ya hayo, kwa hakika nimeandika na kusoma mengi katika sera ya Mtume Mteule (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) nikapata yakwamba kumtumikia mwanadamu na maisha yake ya kijamii na kuyapangilia na kujenga uadilifu wa usawa, ni katika mambo muhimu aliyoyaleta Mtume (Rehema na amani zimshukie). Kwa nini isiwe hivyo hali yakuwa Mwenyezi Mungu amesema kuhusu yeye:(Nasi hatukukutuma (hatukukuleta) ila uwe rehema kwa walimwegu wote). Suratul-Anbiyaa, aya (107). Rehema hii inamaanisha maisha yenye utulivu na kurahisisha mambo ya maisha pamoja na saada (utukufu) wa kesho akhera.

Hayo nimeyapata yameenea katika nyanja za sunna na sera ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam). Nimeandika kuhusu mambo hayo kupitia kitabu changu cha sera "*Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Manabii*" vilevile maudhui haya nimeyaelezea katika makongomano tofauti ya kielimu, nimeonelea kuyatoa katika utafiti pekeyake kama ilivyo katika anwani ilioashiriwa, "*Kujenga jamii ya kiraia na kuikuza katika sera ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam)*" ili kuiweka karibu (yaani kurahisisha kueleweka) katika akili za kizazi kipya na wanaojishughulisha na kujua tamaduni mbali mbali ili wapate kuona kuwa mteule Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) amezipita, kuzitangulia na kuzishinda zama zote katika kupangilia maisha ya kiraia na jamii yake, na kuhakikisha maisha huru yenye utukufu na uadilifu kwa waislamu na wasiokuwa

waislamu, katika wanaotaka maisha ya amani na kujumuika (kuchanganyika) na jamii na kutekeleza haki na wajibu.

Namuomba Mwenyezi Mungu aturejeshe kwenye maisha hayo, kurejea kuzuri na atuandalie uongofu katika jambo letu hili.

## MKATABA WA MADINA (NA KUJENGA JAMII YA KIRAIA)

Mtume (Alaihissalaam) alikuja ili asimamishe jamii ya kibinadamu yenye uadilifu, inayohifadhi haki za mwanadamu, utukufu na amani yake. Alikuja na dini sahihi, ni kama Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyosema: (Na anayetaka dini isiyokuwa ya kiislam basi haitakubaliwa kwake, na akhera atakuwa mwenye hasara (kubwa kabisa). Aali-Imran aya (85). Watu walikuwa na khiyari ya kuingia katika uislamu baada ya kuja kwa dini hiyo ambayo haikuwepo. Mwenyezi Mungu Amesema: (Hakuna kulazimisha mtu (kuingia) katika dini uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayekataa shetani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila shaka ameshika kishiko chenye nguvu kisichokuwa na kuvunjika. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia na mwenye kujua). Al- Baqara aya (256). Kwa hivyo katika hilo watu wako huru baada ya kufikiwa na ujumbe huo.

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alipokuja katika mji wa Madina waislamu walikuwa ni wachache ukiwalinganisha na wasiokuwa wao katika mayahudi na washirikina wa Madina. Pamoja na hilo alikuwa na pupa ya kufahamiana nao wote, na kuandikiana nao mkataba ili kuzilinda haki zao na kuzihami, na kusimamisha maisha ya amani yenye ushirikiano wa jamii zote katika mji wa Madina.[4]

Mtume (Alaihissalaam) alifanya pupa katika kupangilia mafungamano ya wakazi wa Madina kati ya waislamu na wasiokuwa waislamu, na mapema sana aliandika mkataba juu ya

[4] Angalia Al- Balaadhiriy katika Ansaabul-Ashraaf Juz 31 uk 86.

jambo hilo.[5] Na alikuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) wakati wa kufika kwake mji wa Madina ameahidiana na mayahudi na kuandikiana nao maandishi akawekeana nao masharti yakwamba wasiwasaidie maadui zake na pia wamsaidie juu ya yeyote atakaemvamia, ndio mkataba uliojulikana kama mkataba wa Madina.

Bila shaka mkataba huu au Sahifa hii –kama wengine wanavyouita- au dasturi (sharia na mpangilio) kama wengine wanavyouita yamethibiti maandishi yake mwanzoni mwa kugura kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).

Kwa hakika mkataba huu au sahifa hii –kama wengine wanavyouita- ama desturi wanayoshirikiana – kama wengine wanavyoiita- [6] ni kabla ya kutuma vikosi vya kivita (tu), bila ya kushiriki yeye mwenyewe. Pia zimepokewa riwaya nyengine za mkataba na maandishi uliopatikana kati ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akiwa pamoja na waislamu, walifanya mkataba kati yao na mayahudi na watu wengine katika wakazi wa Madina, nasi hizo hazipingani na mkataba wa kwanza au kuuvunja.

Kwa hakika mkataba huu ilikuwa ni kuandika mapatano na ujirani mwema ili waekeane nae amani wala wasisaidiane na maadui zake kumpiga vita na wasimame pamoja nae mbele ya

---

[5] Angalia sira ya ibn Hishaam juz 1 uk 50. Na kwa kusoma zaidi katika Takhriij ya riwaya zilizopokea habari ya ahadi hiyo: angalia, Dr Akram al-Umariy Assiiratu Annabawiyya Asswahiiha, juz 31 uk. 276.

[6] Angalia Swaalih al-Shaamiy katika kitabu Min Maiinussiira uk 180.

yeyote anayemfanyia uadui na kuitishia amani ya mji wa Madina al-munawara (yenye nuru).

Kwa hakika mkataba huu unamaanisha kusimamisha nidhamu inayoongozwa na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) na kuyapangilia majukumu ya ki amani na kuwatetea wakazi wote pamoja na kutomlazimisha yeyote kuacha kuiangalia na kuifata dini yake pamoja na kujuwa yakwamba katika kipindi hiki vitisho juu ya mji wa Madina vilikuwa vimesimama kwa nguvu kutoka kwa washirikina wa Makka waliokuwa wanatoa vitisho kimoja baada ya chengine.

Wala haikuwa imepokewa katika mkataba huu wala mwengine wowote kumtoa yeyote katika mayahudi au wakazi wa Madina wasiokuwa waislamu mda wakiwa wanajilazimu na masharti ya maisha ya kushirikiana na amani ya kijamii ya kijumla inayowahusu watu wote wa Madina, pamoja na mambo yanayomkinika kuwa yamefanana na makazi yanayoshirikisha watu wote, pamoja na kila kundi kuhifadhi haki zake katika itikadi na dini.

Hapana shaka kuwa mkataba huu wa Madina, unahesabiwa ni mfano bora wa kupangilia uadilifu na majukumu ya kijamii na marejeo ya kinidhamu yaliyoandikwa, yanaweza kurejelewa pamoja na kwamba Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa hajui kusoma wala kuandika, ni mkataba ambao unafanana na baadhi ya mipangilio katika dola za kisasa zinazoruhusu uhuru wa dini na kutokuwalazimisha watu kuingia katika dini pamoja na kujilazimisha na amani na nidhamu ambayo watu wanashirikiana pamoja katika majukumu ya kijamii. Na pia

mkataba huu umezingatiwa kuwa ndio msingi katika kusimama dola ya mji wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) na kuyatia nguvu majukumu ndani ya mji huo kupitia mikono ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika maandalizi ya kuitekeleza sharia kulingana na kuteremka kwake na kuyatia nguvu majukumu kupitia mkono wa mtu muadilifu kuliko watu wote, Mtume Muhammad (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).

## KUUKUZA MJI WA MADINA NA JAMII YAKE

Ni hakika kuwa uislamu ulikuja kwa jamii za kibinadamu ili uzipendekeze kunako kumtii Mwenyezi Mungu na kumpwekesha, ili ukiinuwe kiwango cha utukufu wake (mwanadamu) na kuitia nguvi nidhamu, uenuwe uzalishaji na uyahami mazingira na kuihami ardhi kutokana na ufisadi, uimarishe ardhi kwa yale yanayowafaa wanadamu. Na mji wa Madina ulikuwa ndio mfano bora katika jambo hili kwa namna ambayo Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliupangilia kwa sharia mbali mbali pamoja na wasia (maelekezo) na mipango ya kikazi na utekelezaji wa kimiji na kimipango, uliowafanya watu wote wakawa wanashindana katika kuzalisha na kuondoa baadhi ya uvivu na kuwategemea wengine au kutarajia maovu. Ndipo hali ya mji wa Madina -ambao ulikuwa na kubadilika baada ya kugura kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kulikobarikiwa- ikawa dhahiri.

## KUBADILISHA JINA LA MJI WA MADINA

Kabla ya kuja kwa uislamu mji wa Madina ulikuwa unajulikana kama Yathriba, na maana yake ni “baadhi ya lawama”, na jina hilo limekuja katika Qur,ani takatifu: (Na taifa moja miongoni

mwao liliposema “Enyi wenyeji wa Yathribu (Madina) hamna pahali pa kukaa nyinyi, basi rudini (makwenu msiingie katika jeshi pamoja na Muhammad)”, na kundi jengine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume kwa kusema: “ hakika nyumba zetu ni tupu”, hawakutaka ila kukimbia tu). Suratul-Ahzaab aya (13). Na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alilichukia jina hili na akaamrisha libadilishwe kwa jina la Madina.[7] Na inavyojulikana ni kuwa linamaanisha maendeleo na utamaduni na utulivu na yale yanayoambatana na mji na jamii yake. Mji wa Madina umetajwa mara nne katika Qur’an tukufu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na katika mabedui wanaokaa pembezoni mwenu katika vitongoji vya karibu yenu hapo (Madina) kuna wanafiki. Na katika wenyeji wa Madina (Pia kuna wengine wanafiki) wamebobea katika unafiki, (hata) huwajui (kuwa ni wanafiki) sisi tunawajua. tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa katika adhabu kubwa). Suratu At-Tauba aya (101). Pia Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: (Haikuwapasa watu wa Madina –na mabedui wakaao pembeni mwao- kubaki nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (wasende vitani) wala (haiwapasi kujipendelea nafsi zao kuliko nafsi yake (mtume)- wakamuacha Mtume kwenda vitani, wao wakasalia na raha zao Madina). Hayo ni kwasababu yakuwa hawapatikani na kiu wala taabu wala njaa katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakanyagi njia iwachukizayo makafiri, wala hawamtii adui hasara yoyote. Ila huandikiwa kitendo chema (kabisa) kwa ajili ya hayo. Hakika Mwenyezi Mungu haharibu ujira wa watendao wema). Suratu-At-Tawba, aya (120). Pia Mwenyezi Mungu

[7] Rejea Al-Rafaaiy, hadithi zilizopokewa kuhusu fadhila za mji wa Madina uk. 301.

Mtukufu amesema: (Kama wanafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao na watangazao uovu mjini hawataacha (visa vyao hivyo vya upotofu). Kwa yakini tutakusalitisha (tutakuondokesha) juu yao, kisha hawatokaa humo karibu yako ila muda kidogo tu, (kisha litawafika lakuwafika). Pia Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: (wanasema, "tukirudi Madina, mwenye utukufu atamfukuza mnyonge" (Yaani hilo kubwa lao la unafiki linaloitwa Abdalla bin Ubay litamtoa Mtume), na utukufu hasa ni wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wa waislamu, lakini wanafiki hawajui). Suratu Al-Munaafiqun aya (8).

Aidha Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) ameiita Madina kwa majina mengine kama Twaaba na Twayyiba na Al-Mubaaraka na Al-Mushrifa na Daarul-imaan na Al-haswiina, na yote hayo ni majina yanayoonyesha uzuri wa jina hilo na linapelekea kutarajia mambo mazuri.[8]

## MAPENZI YA MADINA NA KUIFANYA KUWA MJI MTUKUFU

Mtume (Alaihissalaam) alikuwa na pupa ya kuweka utukufu wa mji wa Madina akauwekea mipaka na akauombea, kama ilivyopokewa kwa imam Bukhari katika sahihi yake yakuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alisema: "Hakika Ibraahim aliifanya Makka kuwa mji mtukufu na akauombea, na mimi naifanyia Madina kuwa ni mji mtukufu pamoja na sehemu

[8] Angalia Swaleh al-Rafaaiy, katika hadithi zilizopokewa katika fadhila za mji wa Madina uk. 305.

iliyo katika milima yake miwili”.[9] Aidha Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliomba dua hii: “Ewe Mwenyezi Mungu tupendezeshee (tufanye tuipende) Madina kama mapenzi yetu ya kuipenda Makka au zaidi”.[10] Na hapana shaka kuwa kupenda mahali kunapelekea kupahifadhi, kupalinda na kuishi hapo.

Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliweka sharia nyingi kwa ajili ya kulinda mazingira na maisha ya kawaida katika mji wa Madina, miongoni mwa hizo ni neno lake (Swallallwaahu Alaihi Wasallam): “Hakika Ibrahiim aliifanya Makka kuwa mji mtukufu, na mimi naifanya Madina kuwa ni mji mtukufu. Ni sehemu tukufu zile zilizo kati ya hara zake mbili (Hara ni ardhi yenye mawe meusi yaliyochakaa kama yaliyochomwa moto) na sehemu yake yote imehifadhiwa, haikatwi miti yake, hakufukuzwi (kukimbizwa) kiwindwa chake wala hakichukuliwi kilichookotwa humo ila kwa anaetaka kukijulisha, wala haifai kukatwa miti yake isipokuwa kwa anaelisha ngamia wake, wala haifai kuchukuwa silaha kwa ajili ya kupigana ndani ya mji huo”.[11] Na kwa hakika sharia na amri hizo za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) zimechangia katika kuhifadhi mazingira ya kawaida ya hali za mji wa Madina. Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliwasifu watu wa Madina na wakazi wake na walioujia mji huo kutoka sehemu

---

[9] Angalia Swahih ya imam Bukhariy, Kitaabul- Maghaaziy katika mlango Uhud ni Jabali linalotupenda nasi twalipenda Juz 4 uk 40.

[10] katika hadithi aliyoipokea Imam Bukhariy katika sahihi yake hadithi nambari 3926 na imam Muslim katika sahihi yake hadithi nambari 1376. Pia angalia takhrij ya hadithi hii kwa Arrafaaiy na katika hadithi zilizopokewa kuhusu fadhila za mji wa Madina uk 176.

[11] katika riwaya ya imam Ahmad katika musnad yake uk 119.

nyengine na walioguria hapo (Mwenyezi Mungu Awarehemu), kama alivyosema katika hadithi yake: “Hakika imani inajificha katika mji wa Madina kama vile nyoka anavyojikunja na kuingia katika tudu yake”. [12] Na kwa hakika imamu Muslim katika swahihi yake ameweka mlango aliouita “*Kuhimiza (kusisitiza na kupendezesha) katika kuishi mji wa Madina*”, na katika hadithi mashuhuri zaidi (iliyotangaa) ni ile watu waliopokezana kwa ufupi kutoka katika hadithi ndefu ya Mtume, inayosema: (na Madina ni bora kwao kama wangekuwa wanajua).[13]

Pia kumepokewa hadithi nyingi za kuuombea baraka mji wa Madina, katika hizo ni ile iliyopokewa na Bukhariy na Muslim: “Hakika Ibrahiim aliifanya Makka kuwa mji mtukufu na akauombea Mungu, na mimi naifanya Madina kuwa ni mji mtukufu kama Ibrahim alivyoifanya Makka kuwa mji mtukufu tukufu na nimeiombea baraka katika kibaba na pishi yake kama Ibrahim (Alaihissalaam) alivyoiombea Makka”.[14] Aidha ni kama alivyosema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) “ Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu tupendezeshee Madina, tuipende kama tunavyoipenda Makka au zaidi ya hivyo, ijaze siha na

[12]Imepokewa na imam Bukhariy katika mlango wa fadhila za Madina kukusanya na kusoma uk 215.

[13] Hadithi hii ni katika riwaya ya imam Bukhariy hadithi no: 1875 na Muslim hadithi no 1387 na Imam Maalik katika Muwatwa yake Juz 2 uk. 888. Na pia imepokewa na wasiokua wao. Angalia Takhriij ya hadithi hiyo kwa Arrafaaiy katika hadithi zilizopokewa katika jambo hilo. Uk 190.

[14] Ameipokea Bukhariy na Muslim. Angalia takhriij yake kwa Arrafaaiy, katika hadithi zilopokewa kuhusu jambo hilo. Uk. 215.

tubarikie katika pishi na kibaba chake, na tunakuomba ewe Allwaah uigurishe homa yake uipeleke Juhfa”.[15]

## KUJENGWA KWA MSIKITI WA MTUME (SWALLALLWAAHU ALAIHI WASALLAM).

Katika kazi za mwanzo za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika mji wa Madina ilikuwa ni kuweka sehemu ya msikiti wake. Kwa hakika ngamia wake alikita magoti katika sehemu ulipo msikiti wake. [16] Mahala palipokuwa wakati huo wanaswali baadhi ya watu katika waislamu, mahala ambapo palikuwa ni Mirbad (sehemu ya kuanikia tende). Ilikuwa ni sehemu ya vijana wawili ambao ni mayatima, Sahlu na Suhail, waliokuwa katika ulezi wa As,ad ibn Zuraara (Radhwiallwaahu anhu). Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alipomuona ngamia wake amekita magoti yake sehemu hiyo akasema: “Hapa ndipo mashukio Mwenyezi Mungu akipenda”. Kisha aliwaita wale vijana wawili akaelewana nao bei ya sehemu hiyo ili aifanye kuwa ni mahala pa kujenga msikiti, lakini wale vijana wawili wakasema “La hatutokuuzia, tutakupa kama zawadi ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu”. Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akakataa kupachukuwa kama zawadi kutoka kwao, akapanunua kutoka kwa vijana hao kisha akapajenga msikiti. [17]

---

[15] Ameipokea Bukhariy, katika kitabu fadhila za mji wa Madina juz. 32. Uk 225. Angalia takhriij yake kwa Arrafaaiy katika hadithi zilizopokewa kuhusu fadhila za mji wa Madina.

[16] Ibnu Saad Assiratun-Nabawiyya juz 1 uk 237

[17] katika riwaya ya imamu Bukhariy iliyo katika sahihi yake na tamko ni lake yeye. Katika mlango kugura kwa Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasalam) na Maswahaba wake Juz 4 uk 254.

Hima kubwa ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) ilikuwa ni kupatikana msikiti atakaoabudiwa humo Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake (asiyekuwa na mshirika).[18]

Kinyume na kuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anachukuwa hiba na zawadi lakini katika sehemu kama hii hakukubali, bali aliamrisha itolewe thamani yake kutokana na mali yake, kwa sababu hiyo ndipo alipokadiria kima chake na kuitoa thamani yake kwa vijana hao wawili (Sahhi na Suhaily). Na msikiti huu unahesabiwa kuwa ni waqfu wa kwanza katika uislamu, na mtoaji wa waqfu huo ni mteule Mtume Muhammad (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).

Kwa hakika jengo la msikiti huo mtukufu lilijengwa tena pamoja na kupanuliwa baada ya vita vya Khaibar,[19] na mipaka ya msikiti huo tokea wakati wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) hadi leo hii bado inajulikana, na imewekwa alama za rangi ya kijani iliyoandikwa kwa maandishi yaliyo wazi, yeyote anayezuru msikiti wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) anaweza kuyaona na kuyasoma yale yaliyoandikwa.

---

[18] Dr, Suaad Maahir ametunga kitabu alichokiita kitabu cha misikiti katika sera ya Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasallam) kilichotolewa na taasisi ya kijumla iliyoko Cairo. 1987.

[19] Swahihi ya Bukhari hadithi namba 3909. Kitaabu manaqibil-answaar mlango wa hijra ya Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasallam) pamoja na maswahaba wake kuelekea Madina. Pia angalia Ibn. Abi-Shaiba Al-Maghaaziy uk. 152.

## MAENDELEO YA IDADI YA WATU NA UWIYANO WAKE

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa na pupa ya kuongezeka kwa watu katika mji wa Madina na kuzaana kati ya waislamu, na kwa sababu hiyo alifurahi sana na waislamu wakafurahia pamoja naye kwa kuzaliwa mtoto wa kwanza wa muhajirina, baada ya hijra yake ya kuguria Madina. Amepokea imam Bukhariy kutoka kwa Asmaa binti Abu-Bakar yakwamba alichukua mimba ya Abdallah ibn Zubair (Radwiallwaahu anhu) akiwa mji wa Makka anasema: “nikatoka hali yakuwa nimepevusha (mimba yake imekamilika karibu ya kuzaa) nikaja mjini Madina nikashukia mtaa wa Qubaa nikazaa katika mtaa huo, kisha nikamleta mtoto wangu (Abdullaahi ibn Zubeir) kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) nikamuweka mapajani mwake, kisha akaitisha tende akaitafuna kisha akamvivia mate katika mdomo wake, kikawa kitu cha kwanza kilichoingia moyo wake ni mate ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kisha akamfungua mdomo wake (kwa tende aliyoitafuna) kisha akamuombea Mwenyezi Mungu (Mtukufu) na kumbariki (kumuombea baraka), akawa ndiye mtoto wa kwanza kuzaliwa katika uislamu (katika mji mtukufu wa Madina).

Pia ni kama zilivyokuja amri mbali mbali za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) zinazotilia mkazo umuhimu wa waislamu kuwa wengi pamoja na kuwalea watoto vizuri na kuwaandaa, miongoni mwa hizo ni maneno yake Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) pale aliposema: “Oweni mwenye kupendeza mwenye kuzaa, kwa sababu mimi

nitajifakhiri kwa ajili yenu mbele ya umati mwengine siku ya kiama”.[20]

Kwa hakika aya za Qur,ani zimekuja na amri zinazoamrisha kumuhifadhi mtoto na kutilia mkazo uhakika wa kuwepo rizki yao, wao na wazazi wao, katika neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu; (Wala msiwauwe watoto wenu kwa kuogopa umaskini, sisi ndio tunaowaruzuku wao na nyinyi (pia) kwa hakika kuwauwa ni hatia kubwa). Suratul–Israai aya (31).

Hesabu ya kwanza ya watu (censer) iliyojulikana katika uislamu ilikuwa ni wakati wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam). Imepokewa kuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alisema: “Niandikieni wale waliosilimu katika watu”, anasema Hudhaifa ibnul Yamaany (Radhwiallwaahu anhu): “Tukamuandikia watu elfu moja na mia tano (1500)”.[21] Hili lilikuwa ni kutilia umuhimu moja kwa moja katika kujua uwezo wa kibinadamu na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anamuelekeza kila mtu katika jambo linalomfaa.

Ni katika jambo linalojulikana kuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anahimiza watu kugura kwenda Madina, lakini pamoja na hilo alikuwa na pupa ya kuyadhibiti mambo yasivuke mipaka ya kuitingisha Madina na mpangilio wake, na kupatikana mwanya katika mpangilio wake wa kimakazi na watu. Kwa sababu hiyo ndipo pale waliposilimu baadhi ya makabila wakataka kugura wote kwenda kuishi mjini Madina. Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliwaamrisha

[20] imepokewa na Imam Ahmad katika Musnad yake Juz 3 uk 245.
[21] al- khuzaaiy katika Takhriijuddalaalati al-ssamiah uk. 230.

kubakia majumbani mwao ili wengine wajifunze kutoka kwa wengine, wapate kuwa wamejiandaa kwa kuzifata amri zake [22](baada ya kuzijua). Kama ambavyokwamba pia alisitisha jambo la kugura kutoka Makka ambalo ni jambo linalojulisha uwiyano wa kimakazi katika mji wa Madina na miji mengine.[23]

Sio hayo tu, bali hata upangaji wa makao ndani ya mji wa Madina yenyewe ilikuwa ni jambo muhimu, ndipo pale Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alipoujenga msikiti wake mtukufu na ma- Answaar wakajuwa fadhila za msikiti huo na fadhila za kuswali ndani yake. Banu Salama walitaka kuyawacha majumba yao yaliyoko pambizoni mwa mji wa Madina ili waweke makao yao karibu na msikiti wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam), lakini Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) hakulipendelea jambo hilo kutoka kwao. Kama ilivyopokewa katika riwaya ya Anas (Radhwiallwaahu Anhu): (Banu- Salama walitaka wabadilishe makao yao ili yawe karibu na msikiti, Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akachukizwa na jambo la kuuwacha mji wa Madina uwe mtupu. Akasema: “Enyi banu salama kwani hamtarajii kuzibakisha athari zenu?” Ndipo walipobaki wasiyagure makazi yao).[24]

---

[22] ibnu Abiy Shaiba, Al-Maghaaziy uk. 347 na Umar ibn Shubba. Tarekhe ya Madina Juz 2 Uk 482-488.

[23] angalia swahih ya imam Bukhariy hadithi namba 3405-3406. Inafatia mlango wa makazi ya Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasalam) katika mji wa Makka baada ya kufunguliwa mji wa Makka.

[24] Ameipokea imam Bukhari katika fadhila za mji wa Madina mlango wa Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasallam) kuchukia mji wa Madina kuachwa kuwa mtupu.

## UKUAJI WA MAENDELEO YA KIROHO.

Bila shaka kuzidi kwa idadi ya wakazi wa mji kwa wingi bila kutilia umuhimu sampuli ya ukuaji huo kwa kuyajuwa na kuyapangilia mambo na hali ya kila mkazi, huwa hakuna umuhimu, ndipo ukaona Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa na pupa yakwamba kila mmoja ahisi na kujuwa hali ya nafsi yake bila ya kuwa na kiburi, aiambatanishe hali hiyo kwa ucha mungu na unyenyekevu na kuwa mpole kwa waislamu na kuwa na huruma na wanadamu wote.

Pia jambo hilo linalazimu kuikinaisha roho ya kila mmoja katika wakazi wa mji, kimaana na kuitia nguvu. Pia linalazimisha kujenga (kupatikana) kujiamini katika nafsi ya mwanadamu tokea siku za mwanzo katika maisha yake, pia linapelekea kuikuza hali yake ya kinafsi kuanzia jina lake analoitwa, ndipo Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akawa na pupa ya kuwaita watu kwa majina mazuri –si hivyo tu- bali alikuwa anayabadilisha majina mabaya kwa majina mazuri, alikuwa pia anyabadilisha majina mashuhuri ambayo ni mabaya[25] waliyokuwa wanapewa baadhi ya watu na kujulikana kwayo. Kwa sababu hiyo ndipo aliposhiriki katika kuitwa majina ya watu wengine waliozaliwa wakati wa uhai wake, kwa mfano kama Abdallah ibn Zubeir,[26] pia Hasan na Husein, watoto wawili wa

---

[25] Angalia Dr Adnaan al-wazzaan katika enyclopadia ya haki za mwanadamu katika uislamu.

[26] amepokea ibn Abiy shaiba katika Al-maghaziy uk 153. Pia angalia riwaya ya Bukhariy katika fat,hul-Baariy juz 15 uk 104

Aliy ibn Abi-Twalib (Radhwiallwaahu anhum)[27] na wengine wasiokuwa hao katika waliozaliwa Madina baada ya hijra ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).

Pia utapata kuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliyabadilisha majina ya baadhi ya waliogura. Mtu mmoja alikuwa anaitwa Juail akambadilisha akamwita Amran[28], pia alikuwa akiwapa mashababu na watu wote kwa jumla majina yenye heshima na sifa za kimaana wakati wa kuwaita, alikuwa akiwaita kwa majina wanayoyapenda katika Alqaab na Kunniyya ( kama mtu kuitwa babake fulani au sifa fulani, kama Saifullah alilompa Khalid ibnul-Waliid. Alikuwa akimwita mtoto mdogo kwa "ewe kijana changu" au kuwaita kwa majina waliyopewa, alikuwa anamwita ndugu mdogo wa Anas bin Maalik "Abaa-Umair" haya yalikuwa ni kwa watu tofauti kila mmoja kivyake.

Ama kuhusu uma wa Mtume Muhamamd (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kwa hakika Mwenyezi Mungu (mtukufu) amesema kuhusu uma huo: (Nyinyi ndio uma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (ulimwenguni). Suuratu Aali-Imran aya (110). Je baada ya mwito huu kuna unyonge au kusita na kubaki nyuma? Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu Ameinua shani ya umma wa Mtume Muhammad (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kuliko umma wote, kwa ujumla na mtu mmoja mmoja (wote ni watu bora). Kama ilivyotangulia katika Qur'ani Tukufu.

---

[27] angalia Abdul-Aziz al-Umariy, Rasuulullwaahi wakhaatamannabiyyiiin diinun wadaula (Al-muaayishuuna li-rRasuul) sehemu ya tano uk 121

[28] ibnu-Saad Attwabaqaat juz 4. Uk 254: Tafsiri ya Jua'hi ibn suraaqa al-dhwamariy.

## UKUAJI WA KIELIMU

Tokea kuanza kuteremka kwa Qur,ani tukufu na aya zake za mwanzo kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) uislamu ulikuja kukumbusha elimu na kalamu, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba. Amemuumba mwanadamu kwa tone la damu. Soma na mola wako ni karimu sana. Ambaye amemfundisha (mwanadamu ilimu zote hizi) kwa wasita (msaada) wa kalamu (zilizoandika vitabu, watu wakapata ilimu) Suuratul-Alaq, aya (1-5).[29]

Hayo yalitukia katika wakati ambao waarabu walikuwa wanatawaliwa na ujinga, kutokujua kusoma, kuandika, hekaya ngano na uzushi, pamoja na kuweko kiwango kidogo cha elimu katika vituo vya sehemu za mijini. Na kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) Aliguria mji wa Madina akiwa anahimiza juu ya suala la elimu na kusoma[30] na alikuwa anaitukuza daraja yake (elimu) katika nafasi za waislamu.

Bila shaka jambo hilo lilikuwa lina athari yake katika jamii ya watu wa Madina katika kuikuza upande wa kielimu, ndipo yakawa makao na maskani yake ni ya kielimu.

Kwa hakika maswahaba walikuwa wanasoma neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu (Enyi mlioamini mnapoambiwa (katika mikutano "wafanyieni wasaa wenzenu katika (nafasi za) kukaa" wafanyieni nafasi. Na Mwenyezi Mungu atakufanyieni

[29] Kwa urefu Zaidi rejea kitabu: Al-harbiy cha Muhammad ibn Ahmad Iqra-bismi Rabbika chapa ya 1-ya Naadi Jaazan Al-adabiy 1422h.

[30] Kwa urefu Zaidi rejea kitabu: Al-wakiil cha Muhammad Assayyid Harakati za kielimu wakati wa Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasallam) na makhalifa wake waongofu chapa ya -1- Daarul-mujtamaa Jedda mwaka 1406h .

nafasi (duniani na Akhera) na (hata) ikisemwa “Simameni (ondokeni muwapishe wenzenu), basi ondokeni. Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu; na waliopewa elimu watapata daraja zaidi, Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote) Suratul Mujaadila, aya 11.

Aidha imamu Bukhari katika sahihi yake ameweka maandishi aliyoyaita maandishi ya elimu[31] ameleta milango hamsini na tatu kupitia hadithi nyingi na ameshereheshа aya nyingi, mfano wa hayo ni neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Je, afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya mola wake (ni sawa na asiyefanya hivyo) Sema; Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?” Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu). Az-Zumar, aya (9). Pia neno lake Mtukufu: (Na wanakuuliza habari ya roho, sema roho ni jambo lililohusika na Moila wangu (Mwenyezi Mungu), nanyi hamkupewa katika elimu (ujuzi) ila kidogo kabisa. Nayo ni ilimu ya vitu visivyokhusika na roho). Suratu-Banu-Israel aya (85). Pia neno lake Mtukufu (Na katika watu na wanyama wanaotambaa na wanyama (wengine) Pia rangi zao ni mbali mbali, kwa hakika wanaomwogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wale wataalamu (wanavyuoni). Bila shaka Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mwenye nguvu, msamehevu). Suratu Faatwir aya (28). Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) Alisema “Hapana shaka (hafai mtu kuhusudiwa) isipokuwa katika mambo mawili, Mtu aliyepewa mali na Mwenyezi Mungu akawa amesalitiwa kwa kuitumia katika mambo ya haki, na mtu aliyepewa hekima na

[31] Sahihi ya imamu Bukhari hadithi nambari 73.

Mwenyezi Mungu Mtukufu akawa anahukumu kupitia elimu hiyo na anaifundisha (watu wengine).[32]

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anamuamrisha mwenye elimu kuwafundisha wengine. Kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) Aliuhimiza ujumbe wa Abdul-Qais kuwafundisha jamaa zao akawambia: “Rejeeni kwa watu wenu mkawafundishe”.[33] Na kujua kuandika katika mji wa Madina, nafasi ya kwanza ilikuwa inapewa na kupatikana kwa mayahudi waliokuwa wanajua kuandika na kusoma na kuwafundisha watoto wao katika sehemu ambazo zinajulikana kama madrasa siku hizi.[34] Walikuwa wanajikita zaidi katika kufundisha herufi za kiibraniah wanazozitumia kwa kuandikia lugha ya kiarabu, kwa hakika baadhi ya watu wa kabila la Aus na Khazraj walisomea kujua kuandika kutoka kwa mayahudi, miongoni mwao wakiwemo waandishi wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika ma Answaar.[35]

Kwa hakika waislamu walijua thamani ya kujua kuandika kabla ya hijra ya kuguria Madina, kwa namna ambayo tunampata Faatwima binti Khattawaab na mume wake Saeed ibn Zaid katika mji wa Makka wakiwa wanasoma Suuratu-Twaha katika Sahifa iliyokuwa mikononi mwao wakiwa pamoja na Khabbaab ibn-

[32] Sahih ya Imam Bukhariy hadithi nambari 73

[33] Amepokea Bukhari katika sahihi yake ni hadithi no:87.

[34] Rejea; Muhammad al-Iid al-Khatraawiy katika kitabu chake: Madina katika wakati wa ujahilia uk 99.

[35] Angalia: Mustwafaa al-Adhwamiy. Waandishi wa Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasalam) Al-maktabul-Islaamiy chapa ya 1 Bairut mwaka 1401h.

Arat, hilo ni pale alipowaingilia nyumbani mwao Umar ibnul-Khattwaab (Radhwiallwaahu Anhu) na kugundua uislamu wao.[36]

Kujifundisha kusoma na kuandika kulikuwa ndilo lengo kubwa la wengi katika maswahaba katika mji wa Madina baada ya hijra. Na alikuwa Ubaada ibnu-Swaamit (Radhwiallwaahu Anhu) akiwafundisha watu wa Sufa kujua kuandika na kusoma.[37]

Baada ya kumalizika vita vya Badri kulikuwa na kundi kubwa la mateka wanaotokana na washrikina wa kikuraishi wanaojua kuandika na kusoma, wasiokuwa na mali ya kujikombolea nafsi zao kutokana na utumwa, ndipo Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alipokubali yakwamba kila mateka mmoja miongoni mwao awafundishe watoto kumi katika watoto wa Madina, kujua kusoma na kuandika kwa mkabala wa kuachwa huru.[38] Wakati huo ndipo kundi kubwa la vijana wa Kianswaar walipojifundisha kusoma na kuandika, ndipo jambo hili likawa ni sababu ya kuenea kujua kusoma na kuandika katika jamii ya watu wa Madina. Na hapana shaka kuwa wasomi hao walichangia katika kuwafundisha wengine baadae. Na huenda ikawa pupa ya kuiandika Qur,ani na Sunna ilioanza wakati wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) baada ya hapo ikahesabiwa ni katika sababu muhimu zaidi ya kuenea kujuwa kuandika, pia hali

---

[36] Ibnu-Hisham, Assiratul-Nabawiyyah Juzuu.1. uk 345, pia angalia, Abdul-Aziiz al-Umariy: Rasuulullwahi-wakhaataman-nabiyyiina- Diinun wadawla. Katika mlango wa (kusilimu kwa Umar Ibnul Khatwaab ( Radhwiallwaahu Anhu).

[37] Dr. Akram al-Umariy. Jamii ya kiraia wakati wa Mtume, sehemu ya kwanza uk 96.

[38] Abdul-Azii al-Umary: Rasuulullwaahi wakhaataman- Nabiyyiin- Diinun-wadaula (Ghazwatu-Badri), sehemu ya tatu uk.607.

ni hiyo hiyo katika waandishi wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) waliochangia katika kuandika barua zake kwa maamiri wake na kwa wafalme wa ulimwengu, walikuwa ni waandishi ambao baadae idadi yao ilifikia kuwa ni waandishi sitini (60) (Radhwiallwaahu Anhum).[39]

Huenda ikawa umuhimu wa haki za wengine na dharura ya kuzitilia nguvu ni jambo la kimsingi linalohesabiwa kuwa lilipelekea umuhimu wa kujua kuandika, na jambo hili ni lile lilotolewa ishara yake katika aya ndefu zaidi katika Qurani tukufu ambayo ilijulikana kama aya ya deni, katika neno lake Mtukufu. (Enyi mlioamini mnapokopeshana deni kwa muda uliowekwa, basi iandikeni na mwandishi aandike baina yenu kwa uadilifu, wala mwandishi asikatae kuandika; kama alivyomfunza Mwenyezi Mungu.

Hivyo basi naandike. Na ayatamke maneno hayo ya kuandikwa hivyo, (mkopaji) ambaye juu yake iko haki, naye amwogope Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wake, wala asizungumze chochote ndani yake. Na kama yule ambaye juu yake iko haki (mkopaji) ni mpumbavu au mnyonge au yeye hawezi kuandikisha mwenyewe basi aandikishe msimamizi wake (yule mtu anayemwendeshea mambo yake) kwa uadilifu. Na mshuhudishe mashahidi wawili katika watu wenu wanaume (wailsamu) lakini ikiwa hakuna wanaume wawili basi mwanaume mmoja na

[39] Angalia Mustwafa al-Aadhwamiy: Waandishi wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) uk.179. Pia angalia Muhammad Humaidullah: Al-wathaaiq issiyaasiyya lil-ahdin-Nabawiy wal Khilaafatur-Raashida na Ahmad AbdulrRahmaan isiy Kitaabul,wahyi, Daarul-liwaa, chapa ya kwanza Riyadh mwaka 1400h na Jamalud-Diin abi Abdillaahi Muhammad ibnu Abii-Hadida, Al-Misbaahul-Mudhwiiu fiiy kuttaabin-Nabiy.

wanawake wawili (watatosha), katika wale mnaowakubali kuwa kama mashahidi. Ili ikiwa mmoja wao (katika wale wanawake) akipotea, mmoja wao amkumbushe mwengine. Na mashahidi wasikatae waitwapo wala msipuze kuiandika (hiyo deni) ikiwa ndogo au kubwa mpaka muda wake; hiyo (ya kuandika) ndiyo bora mbele ya Mwenyezi Mung na imara zaidi kwa ushahidi; na pia ni yakupelekea kuwa msiwe na shaka. Illa ikiwa ni biashara iliyohudhuria mnayopeana baina yenu, basi si vibaya kwenu msipoiandika. Na shuhudisheni mnapouziana. Wala asitiwe taabuni mwandishi wala shahidi. Na kama mkifanya hivyo, basi hakika hilo ni kosa kwenu. Na mwogopeni Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anakuilimisheni; na Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu). Al-Baqara aya.282.

Pia imejulikana yakwamba katika zama za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) baadhi ya wanawake walikuwa wanajua kuandika na wanawafundisha wanawake wengine na huenda jambo hilo likawa ni kwa kushajiishwa kulikotokana naye, wala hapana shaka kuwa hilo lilipatikana kwa yeye kulikiri (kulikubali lifanyike). Na kwa yakini imepokewa yakwamba alisema kumwambia Shifaa binti Abdallah (Radhwiallwaahu anha) -naye anatokana na bani Adiyy ibn Kaab katika maquraish- alikuwa amesilimu kisha akaguria Madina, -“kwani humfundishi huyu Ruqya ya kumsomea mtu aliyeumwa na chungu kama ulivomfundisha kuandika”.[40] Na iwapo Ashifaa (Radhwiallwaahu Anhaa) alimfundisha mama wa waislamu Hafsa (Allwaah Amridhie) kujua kuandika, haiwi mbali kuwa aliwafundisha wanawake wengine kama ambavyokwamba pia walipatikana walimu wengine wawili wa kike waliokuwa

[40] Ibnul-Qayyim: katika Zaaduul-maadi juzu 3. Uk34.

wakifundisha kuandika na kusoma katika mji wa Madina zama za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).[41]

Kwa hakika sisi tunajua kuwa kuhimizwa kwa elimu na kusoma kulikopokewa katika Sunna za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) na Qur,ani kabla yake, hakuwahusu wanaume peke yao pasi na wanawake, lakini inahusu uma wote pamoja na jinsia zao, umri na makundi yao mbali mbali kwa jumla.

Huenda ikawa kusawirisha idadi ya waandishi wanaojua kuandika katika mji wa Madina na kukuwa idadi yao baada ya hijra ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kwa kipindi cha miaka mine, kunatupa mwelekeo wa kuonyesha namna kulivyokuwa kuenea kwa watu wanaojua kuandika katika mji wa Madina baada ya wakati huo, na hilo ni kwa taathira ya moja kwa moja kutoka kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) pamoja na taathira ya hukumu za sharia ya kiislamu na kuifanyia kazi, kwa namna ambayo ilitarajiwa yakwamba idadi hiyo itapanda zaidi ya mara tatu au mara nne. Pamoja na hayo kulitilia nguvu jambo hilo- wakati huo huo-kuhusu hali ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) ni kuwa kutokujuwa kwake kusoma na kuandika ni muujiza uliopatikana katika haki yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: (Na hukuwa mwenye kusoma kitabu chochote kabla ya hiki; wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume. (Ingekuwa hivyo) wangefanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki). Suratul-Ankabut aya (48).

[41] Angalia Abdul-Aziiz al-Umariy: Al-hirafu wasswanaati fil-Hijaz fil-asrin-Nabawiy (Al-Qira,atul-Walkitaaba) uk. 35

## UKUAJI WA KIJAMII

Kabla ya kuja kwa uislamu jamii ya Madina ilikuwa ni kama jamii yoyote ya kiarabu na kijahilia, ilikuwa inatawaliwa na ada na desturi za kikabila, ilikuwa ni jamii yenye ujinga mwingi, na miongoni mwa ada zao kulikuwa na baadhi yake ni nzuri. Na mahala popote aliposhukia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) -naye ndiye aliyetumwa kuwa ni rehema kwa walimwengu wote- alikuwa anakuja na tabia tukufu na sifa njema zinazoshukuriwa, sifa ambazo zinanyoosha mkono wa mabadiliko ya kijamii katika jamii ya mji wa Madina.

Pia huenda ikawa katika kadhia muhimu ni kushiriki na kuchangia katika kujumuika (kuchanganyikana) kijamii na kugawanya majukumu,[42] kueneza sadaka, zaka na kuwaliwaza na kuwasaidia wanaohitajia msaada kwa namna ambayo kunaeneza kudhamini na kushugulikia mambo ya kijamii, na katika hayo ni lile lilotukia kati ya muhaajirina na answaar, na yale yaliotukia katika kuwasaidia wanaohitajia katika waislamu wa kawaida, bali sadaka na hisani pia zilikuwa zinafanyiwa hata wasiokuwa waislamu tukiongezea na maelekezo ya ki Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) juu ya kujizuia na kuomba na kujitosheleza kutokana na watu wengine.

Bila shaka kulikuwa na vyanzo vyengine vya kuingiza mapato, vyanzo ambavyo vinapelekea uharibifu wa kitabia na kijamii kama uzinifu, Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alivipiga vita, na uislamu ulikua na hukumu ya mkato kaktika kuiharamisha na kuweka adhabu kali kwa kosa hilo, kwa kuwa ni

[42] Harakaati: Ibrahiim Ssiyaasiyaasatu wal-Mujtamaa fil-asri an-Nabawiy: Daarul-aafaaqal-Jadiidah Al-Maghrib 1409 h/1987m uk 237

miongoni mwa sababu muhimu za ufisadi katika jamii na familia na kupoteza nasaba na kudhihiri maradhi ya kinafsi, kupotea majukumu na kukata kizazi. Jambo hilo lmekuja kutiliwa mkazo katika neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na ambao tupu zao wanazilinda isipokuwa kwa wake zao au kwa (wanawake) wale waliowamiliki mikono yao ya (kulia). Basi hao ndio wasiolaumiwa) Suratul- Muuminuun aya (5-6).

Aidha nikwamba uislamu umewawekea wanandoa (mke na mume) haki zilizopangiwa mipaka yake (kisheria), umeamrisha kuheshimiana na kuwa na tangamano zuri kati yao na mapenzi na huruma, na kutendeana mema kunakopatikana kutoka pande zote mbili. Naye Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alilitekeleza hilo katika kuamiliana kwake na wake zake, alikua ni mfano hai katika upande huu.[43] (na pande zote nyengine)

Kama ambavyo pia tembo lilikua linachukua nafasi kubwa katika jamii na linahesabiwa kuwa ni katika vyanzo vya fahari kwa waarabu, ulipokuja uislamu ululiharamisha kidogo kidogo hadi mwisho likawa ni katika madhambi makubwa.[44] Ndipo tabia za watu wengi zilipobadilika kwa sababu ya kuharamishwa kwake.

Kwa hakika uislamu umekuja kuzidisha mafungamano ya kijamii, ukakufanya kuunga kizazi ni katika mambo makubwa yanayomkurubisha mtu kwa Mwenyezi Mungu na kuangalia hali ya jamaa wa kizazi cha mtu na kuwafanyia mema na kuwapa

---

[43] Angalia Al-kamadaaniy: adiib, fannu taamulin- Nabiyy fiyl-hayaa tiz-zaujiyya chapa ya 1 daarul- bashaair-al-islaamiyya Damascus, 1425 h uk 17.

[44] Angalia : Swahihu ya Bukhari ya kitaabul-ashribah (baabu innal khamru wal- maisiru wal-ans waab wal-azlaamu rijsun min,amali shaitwaan) na kutokea hadithi no 5575-5602.

matumizi yao, kuwa ni katika milango ya thawabu kubwa iliyoambatanishwa na tawhidi na uadilifu, Mwenyezi Mungu mtukufu anasema: (Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na kufanya hisani na kuwapa jamaa (na wengineo) na anakataza uchafu na uovu na dhulma anakunasihini ili mupate kufahamu (mufuate). Suratu-Nahl, aya (90).

Aidha Mwenyezi Mungu amekufanya kuwafanyia wema wazazi wawili ni wajibu wa kisheria, umeambatanishwa na kumtii Mwenyezi Mungu na kujikurubisha kwake, Anasema: (Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yoyote ila yeye tu. Na (ameagiza) kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi kama mmoja wao akifikia uzee (naye yuko) pamoja nawe au wote wawili basi usiwaambie hata Ah, wala usiwakemee. Na useme nao kwa msemo wa heshima (kabisa). Suratu Bani-Israel Aya (23).

Pia uislamu umeyafanya mafungamano mazuri na jirani, ni wajibu wa kisheria. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni ihsani wazaza wawili, na jamaa na mayatima na masikini na majirani walio mbali na rafiki walio ubavuni (wema) na msafiri aliyeharibikiwa, na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kulia (kuume). Bila shaka Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wajivunao Suratu Annisaa aya (36). Na pia Mwenyezi Mungu amekufanya kusaidiana kwa mambo mema na uchaji Mungu ni alama ya kijamii ya jumla pale aliposema Mtukufu:(Na saidianeni katika wema na taqwa, wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu: hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu) Suratul Maidah, aya (2).

Mambo yote haya yamezidisha kuchanganyika kijamii na kutengeza jamii katika mji wa Madina baada ya hijra, ikawa ni sababu ya kuikuza jamii na kujuliana hali wao kwa wao na wengine kuwasamehe wengine. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na wale ambao jeuri inapowafikia huzitetea nafsi zao. Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa na (ubaya) huo: lakini anayesamehe na kusuluhisha ugonvi; ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu; bila shaka yeye hawapendi madhalimu). Suratu Ash-Shuura, aya (39-40). Seuze na wasia wa kijumla katika tabia na kuamiliana vizuri na kwapuuza wajinga. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na waja wa Mwenyezi Mungu (anaowapenda ni wenye sifa hizi), ni wale wanaokwenda (na kurejea) ulimwenguni kwa unyeyekevu na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya salama). Suratul-Furqan aya ya (63). Na pia Amesema: (na wale ambao hawashuhudii shahada za uongo, na wanapopita kwenye upuuzi hupita kwa heshima). Suratul-Furqan aya (72). Pia Mwenyezi Mungu ameamrisha kulipa kwa wema wakati wa dharura, Amesema (Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Ondosha (ubaya unaofanyiwa kwa wema); tahamaki yule ambae baina yake na baina yako kuna uadui atakua kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu). Suratu- Fusswilat aya (34).

Pia Mwenyezi Mungu amezifanya tabia tukufu ni lengo lilotukuka kwa jamii na mtu binafsi. Mwenyezi Mungu mtukufu amesema (Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao huenda wakawa bora kuliko wao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao, huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane majina mabaya (ya kejeli) jina baya kabisa mtu kuambiwa ni asi baada ya kuwa ni muislamu (na kufanya haya ni uasi) na wasiotubu, basi

hao ndio madhalimu (wa nafsi zao). Enyi mlioamini (jiepusheni sana kuwadhania watu) dhana (mbaya) ni dhambi wala msipeleleze (habari za watu). Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine je, mmoja wenu anapenda kula nyama ya ndugu yake aliyefariki? La, hampendi; (basi na haya msiyapende). Na mcheni Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni mwenye kupokea toba na mwingi wa kurehemu). Suratul-Hujurat aya (11-12). Mwenyezi Mungu mtukufu akawafanya watu kuwa ni sawa kama meno ya kichana wala hakubagua kati yao, na Qurani iliweka wazi jambo hilo, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Enyi watu! kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamme (mmoja; Adamu) na yule mwanamke (mmoja Hawa) na mjuane (tu basi, sio mkejeliane). Hakika aheshimiwae sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchae Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote) Al- Hujurat, aya (13).

Aidha Mwenyezi Mungu ameharamisha kiburi na kujitukuza kuliko watu wengine pale Aliposema: (wala usiwatazame (usiwafanyie watu jeuri) Kwa upande mmoja wa uso, wala usitembee katika ardhi kwa maringo; Hakika Mwenyezi Mungu Hampendi kila ajivunae, ajifaharishae). Luqman aya (18). Pia Mwenyezi Mungu amekufanya kutengenea kwa jamii na ardhi kwa jumla ndilo lengo la muislamu, pale aliposema Mwenye utukufu; (wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwishwa kutengezwa na mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Bila shaka rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu sana na (wale waja wake) wanaofanya mema). Al- Aaraf- (56).

Mwenywzi Mungu amelifanya jambo la kuusiana kwa haki na subira kuwa jambo hilo ni jambo la kibinadamu la wajibu, Amesema. (Naapa kwa zama (zako ewe Nabii Muhammad).

Kuwa binadamu yuko katika hasara, isipokuwa wale wanaoamini na wakafanya vitendo vizuri, na wakausiana (kufata) haki na wakausiana (kushikamana) na subira (kustahamiliana). Suratul -Asr, aya (1-4). Nyenzo hizi za kijamii zilienea na kushukia mji wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) pamoja na jamii yake baada ya kugura kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) zikaleta ukuaji wa kijamii ambao haujaonekana mfano wake katika historia ya kibinadamu, wala athari yake haikukomea katika mji wa Madina peke yake wala zama zake tu, ndipo ikawa Madina ni Twayyiba (sehemu au mji mzuri) kama alivyouita Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam). Ni kama ilivyo, ibada zote za kiislamu zinaelekea kueka misingi yenye kukataza (kuzuia) uovu na uchafu na miongoni mwa ibada hizo ni ibada ya swala.

Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: (Soma uliyoletewa wahyi (uliyofunuliwa) katika kitabu hiki ulicholetewa (na usimamishe swala) bila shaka swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuia (huyo mwenye kuswali) mambo machafu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu (lililomo ndani ya swala) ni jambo kubwa kabisa (la kumzuia mtu na mabaya). Na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyatenda). Suratul-Ankabuut, aya (45)

## UKUAJI WA MAENDELEO YA KIAFYA

Kabla ya kuja kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam), mji wa Madina ulikuwa umesongwa na matatizo mengi ya kiafya kwa wakazi wa mji huo, miongoni mwa hayo ni yale yaliyoambatana na mazingira, hasa homa iliyoenea kwa watu wake kwa sababu ya mashamba na yanayofungamana nayo katika vidimbwi (vya maji yaliyotuama ambayo ni machafu yanayosababisha kukaa kwa vidudu na kuzaliana kwa virusi). Ndipo Mtume

(Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alipoiombea dua hii: “Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu tupendezeshee Madina tuipende kama tunavyoipenda Makka au zaidi ya hivyo; Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu tubariki katika kibaba chetu na ututengezee mji wetu (uupe afya) uigurishe homa yake hadi Juhfa (Sehemu iliyo nje ya Madina)”.[45] Na ni jambo lililo wazi katika dua hii kuwa inaonyesha kutilia maanani kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) jambo la afya ya mji wa Madina na watu wake.

Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliugua kama wanadamu wengine na aliwashajiisha watu kufanya matibabu na kutafuta njia za kupoza maradhi kama ilivyo katika maneno yake: (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) “Mwenyezi Mungu hajaleta maradhi isipokuwa ameteremsha na dawa yake”. [46]Alidumisha jambo la kujitibu na alikuwa anatilia mkazo kujitibu na dawa za kiasili zilizo sawa (zifaazo kujitibu nazo kisharia) kama asali na dawa nyenginezo, imepokewa kutoka kwake (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kuwa alisema: “Poza (tiba) iko katika mambo matatu, kunywa asali na chanjo za kuumika (kupiga chuku) na piso (kupiswa au kuchomwa na moto), na mimi nawakataza uma wangu na kujitibu huko kwa (kupiswa na moto)”.[47]

Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alisimama msimamo wa mkato (na uamuzi usiotingishika) dhidi ya wasiwasi

---

[45] Ameipokea Bukhari: kitaabu fadhwaailul-Madina juz 2 uk 225

[46] Angalia: Muunis, Husein tarehe ya kiafya ya Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasallam) katika mtiririko wa Iqra. Daarul-maarif Cairo 2000m.

[47] Angalia Fairuuz Abaadiy ya Ahmad Abdur-Rahiim al-Sa,aih na Umar Hamza kutoa muongozo wa Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasalam) inayoitwa Sufrussaada: Markazul-kitaab chapa ya 1 -1417h uk 228.

na hekaya na uzushi unaosababisha maradhi ya kinafsi na kimwili, miongoni mwa maradhi hayo ni kama kurusha ndege[48] na kupiga fali mbaya (kutarajia mabaya) na akawathibitishia kupiga fali nzuri (kutarajia mazuri) na alikuwa anaamrisha kutumia baadhi ya mitishamba na mimea, kama Habbatissaudaai (yaleusi) na dawa nyengine za mitishamba.

Ama katika nyanja za tiba ya kujikinga, aliweka msingi wake katika neno lake: “Mnaposikia kuwa tauni iko katika ardhi (mahala popote) msiingie mahala hapo. Na inapotokea katika ardhi nanyi muko humo msitoke sehemu hiyo”.[49] Pia ni kama alivyoweka msingi muhimu katika afya na matibabu ya kujikinga na kujiagua kutokana na kujizuia na kuacha kula kupita kiasi, na kwa funga za faradhi na za sunna, katika hayo ni neno lake: “Hajajaza mwanadamu chombo ambacho ni kibaya kuliko tumbo, inamtosheleza binadamu tonge chache za chakula zinazoweza kuusimamisha mgongo wake, basi ikiwa hapana budi aligawanye sehemu tatu, thuluthi moja iwe ni ya chakula chake na ya pili iwe ni ya kinywaji chake na thuluthi nyengine iwe ni ya pumzi zake”.[50] Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anakiri (anakubali) kuitwa matabibu ili kuja kuwatibu wagonjwa, kama ilivyotokea kwa swahaba wake Saad ibn Abi-Waqaas (Radhwiallwaahu anhu) alipougua katika hijjatul-wadaai.[51]

---

[48] Angalia Ibnu Qayyim, Attwibbun-Nabawiy uk-229

[49] swahiihul-Bukhaariy,Fat,hul-Baariy Juz 21 uk 303.

[50] ibnul-Qayyim: Zadul-maadiy juz 3 uk 68

[51] ibn saad: Attwabaqaatul-kubraa juz 3 uk 147 Bukhaariy katika sahihi yake, kitaabul-maghaaziy, Baabu hijjatul-wadaai hadithi nambari 4409.

Kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliupiga vita uchawi na kuwendea makuhani kwa kutaka tiba, lakini alikiri ruqya iliyo sahihi kutoka katika Qur'ani na dua. Na katika siku zake (za uhai wake) ilijengwa hospitali ya kwanza katika uislamu, kwa namna ambayo Rufaada al-Aslamiyyah (Radhwiallwaaahu anhaa) alisimamisha hema kwa kuwatibu majeruhi[52] katika vita vya Khandaq, na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alimuweka Saad ibn Muaadh ndani ya hema hilo wakati alipojeruhiwa katika vita hivyo, Akasema: "Muwekeni ndani ya hema la Rufaada ili nipate kumtembelea (kumuamkua) nikiwa karibu nae".[53] Vile vile, amri za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) zilichangia usafi na kuhimiza kuoga katika hali ya kujikinga na maradhi na kuenea kwake. Ulikua wasia wake katika usafi wa chakula na njia ya kukihifadhi na kukifunika una mchango mkubwa katika kuhifadhi afya ya kijamii kwa wanadamu. Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alihimiza kutahiri na baadhi ya mambo ya kimwili ambayo yanachangia katika kukinga kiwiliwili kutokana na maradhi na vidudu vinavyoambukiza, kama alivyosema katika neno lake: "Umbile ni mambo matano au mambo matano ni katika umbile la mwanadamu, kutahiri na kunyoa nywele za kinena, kukata kucha kung'oa nywele za kwapa (kunyoa) na kupunguza masharubu".[54]

Hakika mafundisho haya yote yameathiri katika mji wa Madina na wakaathirika nayo wakazi wake wakayatekeleza katika maisha

[52] ibn Hishaam: Assiiratun-Nabawiyya juz 3. Uk 238 na Ibn Hajar Al-Iswaaba juz 4 uk 303. Na Attwabariy tarekhe yake juz 3 uk 673.
[53] ibnu-Hishaam, Assiratu,Nabawiyya juz uk 238 na Ibn Hajar, Al-Iswaaba juz 4 uk 303 na Attwabariy: Tarekhe yake juz 3 uk 673.
[54] Ibnu-Hishaam, Assiratun,Nabawiyya Juz 3 uk 238.

yao sawa sawa mtu mmoja mmoja au kwa jumla, japokuwa ni mafundisho yaliyoelekezwa kwa wote, lakini jamii ya watu wa Madina wakati wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) waliathirika nayo (zaidi) ndipo ikapatikana kuyapeleka kwa watu wengine na ilichangia katika kuyaendeleza kiafya, kuendeleza ambako kulianzia muda alipofika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika mji wa Madina, na athari yake inaendelea hadi leo na hadi Mwenyezi Mungu (Mtukufu) atakapoirithi ardhi na walioko juu yake.

## UKUAJI WA MAENDELEO YA KIUCHUMI

Tokea utotoni mwake Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa ni mzalishaji (kiuchumi), alikuwa ni kiigizo katika jambo hilo, bila shaka alikuwa akiwachungia mbuzi watu wa Makka ili apate pato, amsaidie Ami yake Abu-Twaalib katika kuwakimu watoto wake. Na kwa hakika (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) Alisema: “Mwenyezi Mungu hakumtuma Mtume yeyote isipokuwa alichunga mbuzi” maswahaba wake wakasema: “Je hata wewe?, akasema: “ndio, hata mimi nilikuwa nikiwachungia watu wa Makka kwa ujira wa *qaraariitwi* (vijipesa vinavyopatikana kutokana na masalio ya dinari baada ya kusurufiwa)”.[55]

Alipofikia kuwa mwanamume (aliyekamilika na kuwa mkubwa mwenye nguvu) aliajiriwa na Khadija binti Khuwailid ili

[55] Ni wingi wa Qiiratwi, nayo ni sehemu katika dinari: Angalia ibnu Hajar katika Fat,hul-Baariy juz 10 uk 5.

amfanyie biashara katika mali yake.[56] Alikuwa na misafara mingi kwa sababu ya biashara. Alikuwa anahimiza watu kufanya kazi na kuzalisha, Alisema; "Hajakula mmoja wenu kabisa chakula ambacho ni bora kuliko chakula cha kazi ya mkono wake". Akaendelea kusema: "na alikuwa Daudi (Alaihissalaam) hali isipokuwa chaklula kinachotokana na kazi ya mikono yake".[57] Na alikuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) anawapigia maswahaba wake mifano ya mitume waliokuwa wanafanya kazi na wazalishaji akisema: "Zakariyya (Alaihissalaam) alikuwa ni seremala".[58] Na ulikuwa mwenendo wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) pamoja na wafanyakazi katika mji wa Madina ni mwenendo wa kuwashajiisha, alikuwa mara nyengine anaitikia mwaliko wa fundi mshonaji katika chakula[59] na anamuacha mtoto wake Ibrahiim kunyonyeshwa na mwanamke aliyekuwa muhunzi.[60] Na kwa hakika miondoko hii na mengine ilikuwa na nafasi yake katika kubadilisha mtazamo wa watu wa Madina na wasiokuwa wao katika waarabu waliokuwa wanazidharau baadhi ya kazi kama uhunzi na nyengine zisizokuwa hizo.[61]

Kwa hakika sharia tofauti za dini ya kiislamu alizozitekeleza Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) zimechangia katika

---

[56] Angalia Abdul-Aziiz al Umariy, Mjumbe wa Mwenezi Mungu na mwisho wa mitume na manabii- dini na dola- (Mtume kumuoa bibi Khadija), Sehemu ya kwanza uk 231; (na ameifasiri katika sehemu ya tano uk 1140).
[57] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake, mlango wa chumo la mtu kutokana na amali ya mkono wake, hadithi nambari 2072.
[58] Ibnu Majah, juz ya 2 uk 773.
[59] Angalia Sahihi ya Bukhariy Juz 3 uk 13.
[60] Ibnu Hajar, Al-Iswaaba Juz 4 uk 98.
[61] Angalia Abdul-Aziz al-Umariy, al-hiraf waswanaati fil hijaaz fil asri an-nabawiy (mauqiful-islaam minal hirafi wa swanaat) uk 43

kuzidisha pato la mji wa Madina na ukuaji wa kiuchumi katika nyanja zote, miongoni mwa hizo ni kama zifuatazo:

## UKUAJI WA MAENDELEO YA KIBIASHARA

Mtume (Alaihissalaam) alipofika mji wa Madina biashara ilikuwa mikononi mwa mayahudi, wanayashughulikia masoko yake hasa soko la banuu Qainuqaa,[62] ambalo lilikuwa maarufu kwa jina lao, nalo ni mashuhuri zaidi katika masoko ya Madina wakati wa kugura kwake. Na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa na pupa kuwa waislamu wasishindwe katika masoko ya Madina na uchumi wake. Pia soko la banu Qainuqaa linahesabiwa katika masoko muhimu ya mji wa Madina katika zama za ujahilia (za kabla ya uislamu) na pia baadhi ya waarabu katika kabila la Ausi na Khazraj walikuwa wana harakati za kibiashara katika mji wa Madina pamoja na kuweko masoko mengi madogo madogo ambayo yanahusiana nao kama soko la Muzaahim.[63]

Aidha mji wa Madina ulikuwa unaongoza kwa mazao yake ya ukulima yakiwemo tende na mazao mengine. Kama ambavyo kwamba watu wa Makka na wasiokuwa wao, wanakuja Madina kwa kununua Tende na mazao mengine ya ukulima na vitu vyengine vidogodogo vinavyotengezwa hapo. Pia mayahudi walikuwa wanasimamia na kuziongoza rasilimali ambazo wanawakopesha watu kwa riba, walikuwa wakisaidiwa na mali hizo katika kuongoza na kuyaendesha mambo katika mji wa Madina. Na pia kabila la Ausi na Khazraj lilikuwa na mchango

---

[62] Umar ibn Shubba, Historia ya Madina Juz ya 1 Uk 304.
[63] Assamhuudi, Wafaaul,wafaa juz 4 uk 1306

katika uchumi wa Madina, na mchango wao wa kiukulima ulikuwa una nguvu zaidi kuliko mchango wa kibiashara.

Kadhalika wakati Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alipoguria mji wa Madina pamoja na maswahaba wake, wengi katika muhaajirina walikuwa na kipawa cha kibiashara, wengi wao walikuwa muda wakifika Madina (tu) wanauliza mahala soko lilipo, wakawa wananunua na kuuza kwa kutafuta riziki miongoni mwao akiwemo Abdur-Rahmaan ibn Auf [64] na Umar ibnul-Khattwaab (Radhwiallahu Anhumaa).

Kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alihisi kuwa mayahudi wanaishikilia biashara katika mji wa Madina kupitia kulishikilia kwao soko la banu Qainuqaa, akataka kuifanya Madina iwe na soko jengine ambalo liko mbali na kushikiliwa na mayahudi (liwe katika milki ya waislamu), ndipo alipokita hema katika sehemu ya banii Zubeir, akasema: “Hili ndilo soko lenu”, jambo hili liliwakasirisha sana mayahudi, wakahisi hatari ya soko hili kukingamia na kushindana na soko lao, ndipo alipokuja Kaab Ibn- Ashraf akaingia ndani ya hema hilo, akazikata kamba zake. Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akasema: “Hapana shaka nitaligurisha sehemu ambayo itakasirisha kuliko hapa”. akaligurisha katika sehemu inayojulikana kama soko la Madina, kisha akasema: “Hili ndilo soko lenu hapatotiwa dhiki wala kuchukuliwa kodi”.

Mtume pia alikataza kuchukuliwa kodi kutoka kwa mtu yoyote katika soko la Madina jambo lilolifanya kukuwa na kupendwa na

---

[64] Angalia riwaya ya Bukhariy katika sahihi yake, Kitaabul-Maghaaziy, mlango “namna Mtume alivyounganisha kati ya Maswahaba wake”, hadithi nambari 3937.

watu wengi, na kwa hakika kuchagua kwake Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) soko hili, lilikuwa ni jambo liloafikiwa sana, kwa namna ambayo sehemu hiyo ilikuwa ni kama mlango wa kuingilia mji wa Madina kwa wale wanaokuja kutoka upande wa Shamu, Makka na Yaman au kutoka miji ya makabila mengine yalio karibu na Madina, jambo lilolifanya soko la waislamu kuwa linayapokea makundi ya watu na wafanya biashara wakati wa kufikia kwao mji wa Madina na kabla ya kufika soko la banu-Qainuqaa, ambapokwamba pia ni jambo lililowaudhi mayahudi, wala hapana shaka yakwamba amali hii ina sehemu yake katika kuendelea kwa biashara, kuuza na kununua kati ya waislamu na wasiokuwa wao na kuamsha (kukuza) upande wa biashara kwao wao. Hapo ndipo polepole ilipozidi biashara katika soko la waislamu mjini Madina ambayo ilikuwa ni natija ya uchangamfu wa Muhaajiriina ambao wengi wao wanatokana na kabila la kikuraishi ambao asili yao ni wafanya biashara, wakawa Abu-Bakar na Umar na Uthmaan (Radhwiallwaahu anhu) ni katika wanaofanya kazi ya kuuza na kununua, na alikuwa Uthmaan na Twalha ibnu-Ubaidullaahi (Allah awaridhie) ni katika wauza ngano katika soko la Madina. Naye Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anawapitia wauzaji katika soko la Madina na ananunua bidhaa kutoka kwao na anawatahadharisha na kufanya hadaa, na pia Maswahaba (Radhwiallwaahu anhum) walikuwa wanashiriki katika misafara ya kibiashara kutoka Madina kuelekea Shamu siku za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).[65]

---

[65] Ibnu Kathiir, Assiratun-nabawiyah juz 2 uk 249.

## URATIBU WA SERIKALI NA UGAWAJI WA MAJUKUMU.

Kwa hakika miji ya kiarabu -hasa Hijaaz na Najd- ilikuwa mbali na mpangilio wa kisiasa na kiidara. Ilikuwa ni miji inayonyenyekea mila, ni makabila ambayo yanajitawala na kujiendeshea mambo yao bila nidhamu yoyote, hapakuwepo na siasa wala dola inayosaidia, mara nyingi ilikuwa ni hivyo. Wala katika mji wa Makka hakukuwa na uongozi unaosikika na idara yenye kubeba jukumu. Katika mji wa Madina hakukuwa na jambo lolote miongoni mwa mipangilio hiyo, kwa namna ambayo walikuwa na mipangilio ya kikabila na ada zake pamoja nakwamba walikuwa ni wakazi wa miji, lakini ilikuwa haina mpangilio au idara maalumu, hadi ilipokua chini ya hukumu ya Mtume (Swallallwahu Alaihi Wasallam). Bila shaka idara ya hukumu yake ilikuwa ni moja miongoni mwa alama zilizo wazi ambazo zimekuja katika Qur’ani, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: (Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni kuzirudisha amana kwa wenyewe (wanaozistahiki). Na mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa haki. Bila shaka mawaidha anayokutoleeni Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye asikiyae (na) Aonae. Enyi mlioamini mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (waislamu wenzenu). Na kama mkihitilafiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hiyo ndio kheri, nayo ina matokeo bora kabisa). Suratu An-Nisaa, aya (58-59). Pia Anasema: (Kwa hakika tuliwapeleka mitume wetu kwa dalili wazi wazi na tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu na tumekiteremsha (tumekiumba) chuma

chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu, na ili Mwenyezi Mungu amjulishe anaye mnusuru na Mitume yake, na hali yakuwa hawamwoni Mwenyezi Mungu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda). Qur'ani Tukufu, Suratul-Hadyd, aya (25).

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa ndiye kiongozi wa dola, na anawasaidia wafanyikazi na watumishi[66] na wanaoshughulikia idara mbalimbali, alikuwa na pupa juu ya mambo ya idara na kupanga majukumu, na tokea *baia ya Aqaba* ya pili (alipokutana na Answaar wakati wa hijja mjini Makka) Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliwapanga waliombai (kumuunga mkono na kuchukuwa ahadi) na akawataka wachague wawakilishi baina yao, ambao watakuwa ni wenye kubeba majukumu kwa niaba ya wengine, ili kupokea amri na maelekezo na kufatilia katika kila jambo linalomuhusu[67]. Na *baia* hiyo ilifanywa na wanaume pamoja na wanawake na ni yenye maana maalumu[68]. Imepokewa katika kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu kama Anavyosema. (Ewe Nabii watakapokujia wanawake walioamini wanakuahidi yakwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawawauwa watoto wao, wala hawataleta uzushi wanaouzua tu wenyewe baina ya mikono yao na miguu yao, wala hawatakuasi katika jambo jema, basi

[66] Angalia, 'Wafanyakazi wa Mtume katika miji',uandishi wa Khalifa ibnu Khayyaat na tarehe yake uk 60. Kuwataja wafanyakazi wake (Swallallwaahu alahi wasalam) na Abdul-Aziiz al-Umariy "Utawala wa kimiji katika zama za Makhalifa waongofu (utawala wa kimiji katika zama za mtume) uk 39.
[67] Angalia Abdul Aziiz al Umariy "Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa mitume-dini na dola (baia ya Aqaba ya pili) sehemu ya pili uk 384.
[68] Al-kattaaniy, Mpangilio wa kiidara Juz 1 uk 222.

peana ahadi nao na uwatakie maghufira kwa Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira, mwingi wa rehema). Al-Mumtahina aya (12).

Amri za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) zilikuwa ziko wazi katika kupangilia majukumu katika mkusanyiko wowote, sawasawa uwe wa watu kidogo au wengi. Kwa hakika amesema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam): “Si halali (haifai) kwa watu watatu watakaokuwa jangwani (wanasafiri) katika ardhi isipokuwa wamueke mmoja wao awe kiongozi”.[69] Na pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa akiendesha mambo ya dola kiaskari, na kwa hakika lilikuwa jambo la mpangilio na kupanga uongozi na kuwatii viongozi na kuwaskiza kwa wema ni katika jambo ambalo Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliulea umma wa kiislamu kwa jambo hilo.

Kwa hakika Madina ilikuwa ni dola ya kiislamu na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa ndie kiongozi mtekelezaji wa mji wa Madina pamoja na cheo cha utume, alikuwa ndiye anayeshughulikia kuyaendesha mambo yake. Kama ambavyo pia alikuwa akimweka kiongozi (msimamizi) wa mji wa Madina yeyote anayemchagua katika maswahaba wake wakati akiwa mbali na mji huo mtukufu. Na kwa hakika watu wa sera wametaja majina ya watu waliowekwa na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika kila vita wakati yeye hayuko na miongoni mwa watu mashuhuri waliopewa uongozi na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) juu ya mji wa Madina

[69] Ameipokea Imam Ahmad katika musnad yake Juz 2 Uk 177.

ni Abdallah Ibn Ummi Maktoum[70] (Radhwiallwaahu anhu) kwa namna ambayo imetajwa kuwa alimueka kiongozi wa Madina mara 13 ( kumi na tatu)[71] miongoni mwa hizo ni wakati wa vita vya Badri[72] na vita vya Hamraaul-Asad na vita vingine.[73]

Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alimpa uongozi Uthman ibn Affaan kuongoza mji wa Madina katika baadhi ya vita vyake[74](Swallallwaahu Alaihi Wasallam).

Kadhalika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliwapanga maamiri na wafanyakazi wa kila wilaya zilizojulikana katika zama zake (Swallallwaahu Alaihi Wasallam), na zikafata mji wa Madina, miongoni mwa hizo ni: wilaya ya Yaman, Makkatul-Mukarrama,[75] Twaif, Bahrain[76] na Oman[77]. Na Mtume

---

[70] Abdallah ibn ummi Maktoum (Radhwiallwahu anhu) ni swahaba wa kikuraishi aliyesilimu kitambo katika mji wa Makka, alikuwa ni katika muhajirina wa kwanza na yeye ndie kipofu alietajwa katika Suratu Abasa. Alipata shahada katika vita vya Qaadisiyah (Ibnu Hajar, Al-iswaabah juz 2 uk 525.

[71] Ibn hajar, Al-Iswaabah juz 2 uk 523.

[72] Khalifa ibn Khayaat katika tarehe yake uk 96.

[73] Ibnu Hishaam, Assiratun-Nabawiyah juz 3 uk 101-102.

[74] Assuyutwiy tarehe ya makhalifa juz 1 uk 148.

[75] Attwabariy. Tarehe yake juz 3 uk 126 na Uttaab ibnu Usaid yeye ni ibnu Abil-Aiswi ibn Umaiyah ibn Abdi-shamsi, kutokana na makuraish, alisilimu siku ya fat,hu Makka na Mtume akamchagua kua mfanyakazi wa Makka, Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikufa hali yeye bado anaongoza Makka. Abu-Bakar akambakisha hapo hapo, na alikufa katika zama za utawala wa umar (Radwhiallwahu anhu). Ibnu Saadiy, Attwabaqaat Juz 5 uk 446. Na Ibnu Hajar katika Al-iswaabah, juz ya 2 uk 451.

[76] Al-Baladhiriy katika Futuhul-buldaan uk 90.

[77] Khalifa ibn Khayyaat katika tarehe yake. Uk 97, As-Suhailiy, Ar-raudhul-unuf. Juz 4, uk 250

(Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikua akiwashauri sana maswahaba wake hali yakuwa yeye ndie kiongozi wa dola ya kiislam. Pale alipoteremshiwa suratu Shuura ili iutie nguvu msingi huu, kama ulivyo katika neno lake: (Na wale waliomuitikia Mola wao kwa (kila amri zake) na wakasimamisha sala, na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku). Ash-Shuura, aya (38).

Pia katika neno lake Mwenyezi Mungu: (Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekua laini kwao (Ewe Muhammad). Na kama ungekua mkali na mwenye moyo mgumu bila shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe wewe na uwaombee msamaha kwa (Mwenyezi Mungu) na ushauriane nao katika mambo ufungapo nia, mtegemee Mwenyezi Mungu tu ufanye hili ulilaazimia, hakika Mwnyezi Mungu huwapenda wamtegemeao). Aali Imran, aya (159).

Kwa hakika imethubutu yakwamba Mtume alikuwa akitaka ushauri kwa maswahaba wanaofanya kazi nae kabla kupitisha maazimio muhimu, hadi baadhi ya maswahaba wakajulikana kuwa ni washauri wake (swallallwaahu Alaihi Wasallam).

## UADILIFU NA USAWA

Uadilifu ni msingi muhimu wa kiislamu na kibinadamu, ndio unaohukumu na kuyaweka sawa mambo ya muislamu katika hali za mtu pekeyake, na za kijumla, hasa hali zinazofungamana na mambo ya watu wengine pindi muislamu anapotawalia mambo ya watu, pia ni jambo bora lilotukuka ambalo nidhamu zote, zama na sehemu zote liliukimbilia ili kuhakikisha (kuupata na kua nao katika jamii zao). Na kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: (Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu,

na kufanya hisani, na kuwapa jamaa (na wengineo), na anakataza uchafu na uovu, na dhulma. Anakunasihini ili mupate kufahamu (mfuate). Suratu An-Nahl, aya (90).

Pia Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: (Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni kuzirudisha amana kwa wenyewe (wanaozistahiki). Na mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa haki. Bila shaka mawaidha anayokutoleeni Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye asikiyae na aonaye). Suratu-An-Nisaa, aya (58).

Aidha Mwenyezi Mungu mtukufu amesema: (Waite kwenda kufanya haya, na mwenyewe utengenee (unyoke) kama ulivyoamrishwa, wala usifate matamanio yao, na useme "Naamini vitabu alivyoteremsha Mwenyezi Mungu, na nimeamrishwa nifanye uadilifu baina yenu, Mwenyezi Mungu ndiye Mola wenu na (pia) ni Mola wetu, vitendo vyetu ni kwa ajili yetu, na vitendo vyenu ni kwa ajili yenu (wenyewe), hakuna ugomvi baina yetu na nyinyi, Mwenyezi Mungu atatukusanya pamoja na marejeo ni kwake). Suratu Ash-Shura, aya (15). Pia Mwenyezi Mungu amesema: (wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na (haya) wanayoyafanya madhalimu. Hakika yeye anawaakhirisha tu mpaka siku ambayo macho (yao) yatakodoka (yatoke nje kwa hofu), (wawe) wanakwenda mbio vichwa juu, na macho yao hayapepesi, na nyoyo zao tupu (haziko wanahema kwa mbio, mapepe). Na uwaonye watu siku ambayo itawafikia adhabu, waseme waliodhulimu (nafsi zao) "mola wetu tuahirishie muda mdogo. Tutaitikia wito wako na tutawafuata mitume", (waambie) "je? Hamkuwa mumeapa zamani yakwamba nyinyi hamtapata muhamo wowote (wakuihama dunia)? Na mkakaa katika mahala mule walimokua wamekaa wale waliodhulumu

nafsi zao na ikakudhirikieni jinsi tulivyowafanya, na tumekuelezeni mithali zote, (na nyinyi hamkujali kitu). Suratu Ibrahim, ya (42-43). Pia Mwenyezi Mungu anasema: (Enyi mlioamini kuweni wasimamizi wakupitisha haki kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, muwe mkitoa shahada kwa uadilifu, wala kuchukiana na watu kusiwapelekeeni kutowafanyia insafu (uadilifu) fanyeni uadilifu huko, ndiko kunakomkurubisha mtu na uchamungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) mnayoyatenda). Suratu Al-Maidah, aya (8).

Hapana shaka yakwamba uadilifu hauhusiki katika kuhukumu peke yake, lakini ni jambo linaloelekezwa kila muislamu katika kazi yoyote nao ni kiini cha kazi ya kiidara, kwa namna ambayo msimamizi wa idara anafaa awe muadiifu kwa wafanyakazi wake na awe muadilifu pia kwa wale alio na mafungamano nao katika kazi yake. Na uadilifu unatakikana kuweko katika kila mwanadamu, hata katika kuiongoza familia yake na kazi zake yeye mwenyewe, basi itakuwaje akiwa mtu ni mwenye cheo na kazi yenye kufungamana na watu wote au baadhi yao? Bila shaka atatakikana awe muadilifu zaidi.

Kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anajihadhari na kufanya dhuluma na katika yanayoashiria hilo ni neno lake: “iogopeni dhuluma, hakika dhuluma ni giza siku ya kiama”.[78] Katika hilo pia ni kama vile alivyokuwa akiamrisha kutekeleza uadilifu na kusimamisha adhabu (za kisharia) kwa

[78] Ameipokea Bukhariy katika Sahihi yake malango “dhuluma ni giza siku ya kiama” juz 3, uk 99. Na ameipokea imam Ahmad katika musnad yake juz 2 uk 92.

mnyonge na mwenye nguvu na kutahadharisha juu ya kulipuuza jambo hilo kama ilivyo katika kauli yake: “Hakika liliwaangamiza wale waliokuweko kabla yenu (mayahudi na manaswara) kuwa alikua akiiba mtu mtukufu miongoni mwao walikuwa wakimuacha na akiiba mtu ambae ni dhaifu wanamsimamishia adhabu, Naapa kwa Mwenyi Mungu lau kama Faatwima binti Muhammad (Radhwiallwaahu Anhaa) angeliiba ningeukata mkono wake.[79] Mtume alikua akisimamia na kuongoza hukumu kati ya watu yeye mwenyewe.[80] Alikua akipupia kufanya uadilifu na anachelea kuichanganya haki ya wagomvi, akachukua haki ya wengine na kuwapa wengine, anatahadhari ya kufanya uadui juu ya watu wengine japokuwa ni kwa hukumu katika uamuzi wa mambo. Kwa sababu hiyo imepokewa kua yeye alisikia wagomvi mlangoni mwa nyumba yake akawatokea akasema: “Hakika mimi ni mwanadamu na kwa hakika wananijia wanaogombana na huenda ikawa baadhi yenu wana ufasaha zaidi kuliko wengine (katika kujua kuzungumza) nikadhania kuwa ni mkweli nikampa haki ya jambo hilo, basi yoyote nitakaemuhukumia (kumpa yeye) haki ya muislamu ajue hiyo ni sehemu ya moto basi na aichukue au aiwache”.[81] Na kwa hakika alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu anahukumu baina ya watu wote na anafanya kazi ya kuzitekeleza haki kwa wenye haki sawa sawa wawe ni waislamu au makafiri, na anabainisha misingi ya kitabia ya mahakimu na wanaohukumiwa na anatahadharisha urongo katika madai au yamini ambayo

[79] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake, hadithi nambari 3733.
[80] Kwa urefu Zaidi angalia al-Qurtubiy Abdallah Muhammad ibn Faraj al Maalikiy “hukumu za Mtume” chapa za kimji za Qatar, Doha-Qatar (haikuandikwa mwaka wa kuchapishwa)
[81] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake, hadithi nambari 2458.

inapelekea mwanadamu kuchukuwa haki ambayo si yake. Kwa hakika imepokewa kutoka kwa Abdallah ibn Masoud (Radhwiallwaahu Anhu) yakwamba alisema: Amesema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam), “Mwenye kuapa kwa yamini (kiapo) cha uongo ili ajichukulie mali ya mtu muislamu, huwa katika yamini hiyo ni muovu, atakutana na Mwenyezi Mungu hali ya kua amemkasirikia”[82], na katika hilo imeteremka neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na jiepusheni na usemi wa urongo). Qur’ani Takatifu, Suratul -Hajj, aya ya (30).

Aidha ni kama maelekezo yake yalivyo wazi katika kufanya usawa kati ya wanaoteta na kutokuhukumu kwa matamanio na kuhukumu kwa nidhamu ya kisharia ilio wazi, na mfano wa hayo ni neno lake Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam): “Ushahidi ni juu ya yule mshitaki na yamini ni juu ya yule aliyepinga (mashtaka)”.[83] Na Qur’ani imetaka kusimamishwa uadilifu pasi na matamaniyo, japo kuwa haki ni juu ya mtu mwenye heshima na utukufu kwa wanadamu, bali hata iwe juu ya mtu nafsi yake, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Enyi mlioamini kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu, au (juu ya) wazazi wenu na jamaa (zenu) Akiwa tajiri au maskini (wewe usitazame). Mwenyezi Mungu anawastahikia Zaidi (kuliko wewe). Basi msifate matamanio mkaacha kufanya uadilifu. Na kama mkipotoa (shahada) au mkajitenga (na) kushuhudia, Mwenyezi Mungu atakuteseni); na Mwenyezi

[82] Kutoka hadithi ya Bukhariy, mlango wa ugomvi. Hadithi namba 2416

[83] Imam Bukhariy katika sahihi yake ‘katika maandishi ya ushahidi’ (mlango uliokuja kuelezea yakwamba kuleta ushahidi ni juu ya mshtaki) juz 3, Uk 146.

Mungu anazo khabari za yote mnayoyatenda) Suratu An-Nisaa, aya (135). Na imepokewa katika hadithi Qudsiy, kua Mwenyezi Mungu (Mtukufu) Amesema: (Enyi waja wangu, hakika mimi nimejiharamishia dhulma juu ya nafsi yangu na nimeifanya kuwa ni haramu kati yenu, basi msidhulumiane)[84]

Kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) ametahadharisha mahakimu madhalimu kwa neno lake pale aliposema: “Mahakimu ni watatu, mahakimu wawili wako motoni na hakimu mmoja yuko peponi, hakimu aliyehukumu pasi ya haki hali yakua anajua kua hukumu hiyo si haki, huyo yuko motoni, na hakimu aliyehukumu na yeye hajui akazipoteza haki za watu, huyo pia yuko motoni, na hakimu aliyehukumu kwa haki, huyo yuko peponi”.[85]

Ni kama ambavyo pia uislamu umeharamisha rushwa na ni jambo linalopelekea dhuluma na kuwapokonya watu haki zao, lina athari kwa mahakama na mahakimu. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swallallwaahu Alaihi Wasallam): “Mtume wa Mwenyezi Mungu Amemlaani mwenye kutoa hongo (rushwa) na mwenye kupokea hongo na al-r-Raaish (yule anaefanya mawasiliano baina yao)”.[86] Na jambo la hukumu lilikuwa limeenea kwa watu wote katika jamii ya kiislamu na lilitekelezwa katika zama za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika

---

[84] Ameipokea Muslim katika “Kitaabul-birri” mlango wa kuharamisha dhulma. Juz 8, Uk 17. Pia Imam Ahmad katika musnad yake Juz 5, uk 160.
[85] Ameipokea Tirmidhy “Kitaabul-ahkaam” Namba 1322 Juz 3 uk 612
[86] Ameipokea Ahmad katika musnad yake Juz 2 uk 164 na Juz 5, uk 279. Na Tirmidhy katika “Kitaabul-ahkaam” hadithi nambari 1336. Juz 3 uk 622, na ibnu-Maaja katika “Kitaabul-ahkaam” na ad-Daaramiy katika hukumu.

jamii ya Madina lilikuwa linawakusanya waislamu na wasiokuwa waislamu, na haja ya uadilifu.

Ni jambo linalotakikana kwa watu wote waislamu na wasiokuwa waislamu, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (wasikiao uwongo, walao haramu, basi wakikujia, wahukumu baina yao au jipuze nao. Na ukijipuza nao, basi wao hawatakudhuru chochote. Na ukiwahukumu, basi toa hukumu baina yao kwa uadilifu. Bila shaka Mwenyezi Mungu anawapenda waadilifu). Qur'ani Tukufu, Suratu Al-Maida aya (42).

Kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alianza kwa kufanya kila ambalo katika jambo hilo kunapatikana kupangilia uadilifu, kwa kuwachagua makadhi (mahakimu) katika sehemu za mbali na Madina. Kwa hakika alituma idadi ya maswahaba kwenda kuhukumu katika utesi wa watu na alikuwa akiwaelekeza[87] na halikubakia jimbo lolote linalofata dola ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) isipokuwa aliweka maamiri na wale wanaohukumu baina ya watu na kusimamisha uadilifu kati yao. Na huenda ikawa desturi ya kilimwengu ilio mashuhuri katika hukumu ni barua ya Abu-Musa al-Ash,ariy katika hukumu[88] na katika ambalo halina shaka ni kuwa Umar ibn Khatwaab (Radwiallwaahu anhu) aliyatoa (maelekezo hayo)

[87] Al-Mawaaridiy, Al-Ahkaam As-sultwaaniya Uk 67.

[88] Sharhu ibnul-Qayyim, barua ya Umar kwa Abu-Musa al-Ash-ariy. Iko katika kitabu chake "Ilaamul-Muwaqiin an Rabbil-A'lamiin, katika kurasa zinazozidi 450, (Ibnul-Qayyim, Ilaamul-Muwaqiin an Rabbil-Alamiin) Juz 1 Uk 86-406, Juz 2 Uk 1-165.

kutoka yale aliyojifundisha kutoka kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika mambo ya hukumu na uadilifu.[89]

Wala hapana shaka yakwamba kupangika maisha na amani katika jamii yoyote ya kibinadamu, hakusimami isipokuwa kwa nidhamu (mipango) na kanuni na sharia zilizo wazi ambazo watu wote wanakua ni sawa katika nidhamu hiyo pamoja na kuweko marejeo ya kihukumu ya kuhifadhi haki, na kupatikana nguvu ambazo zinasaidia katika kuzirejesha haki kwa wenyewe na kuzuia dhuluma na kuzitekeleza hukumu za maamuzi. Jambo hili likipatikana linawapelekea watu wote kupata amani na kuwa pamoja katika nidhamu hii (kuipa nguvu) ya uadilifu inayodhamini haki, na inasaidia katika maisha mazuri na kuzalisha kuliko sahihi, kuliko mbali na kuwaibia watu, na kuzifanyia uadui mali, heshima au nafsi zao.

Hivi ndivyo ambavyo Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alivyoijenga jamii ya kiislamu katika mji mtukufu wa Madina, yaani kwa maelekezo ya kimungu na utelekezaji wa kimtume, yalikuwa katika mji wa Madina na miji au sehemu zilizokua chini ya hukumu na idara yake katika sehemu za visiwa vya arabuni (bara arabu) zilijengwa juu ya uadilifu. Na nidhamu hii ikawa ni kurunzi kwa dola za kiislamu na jamii zake, amani yake inazidi kila wanapoigiza na kwenda juu ya njia yake, na haki zinapotea kila dola hizo zinapokuwa mbali na njia yake.

Kwa hakika wanachuoni na wasomi wa sharia na watungaji katika nyanja hizi, wametunga tungo ambazo ni vigumu kuzihesabu katika turathi za kielimu ya sharia iliyo adilifu, sharia

[89]Ibnul-Qayyim Ilaamul-Muwaqiin an Rabbil-A’lamiin Juz 1 Uk. 85-86, Al-Hawaariy, Idara na misingi ya kielimu uk.176.

ya kiidara, kikanuni na ya kisiasa. Inamkinika kuangaliwa katika upande wa kimiji na kiraia,[90] na kwa hakika wengi katika vijana wa uma wa kiislamu wamekosa kujua na wengi katika viongozi na wenye kuamua mambo (viongozi wenye amri na uamuzi wa mambo) ndipo wakapotea na kuwapoteza wengine.

## KUPANGILIA AMANI NA USALAMA

Kuhifadhi amani ni haja ya dharura katika haja za kibinadamu, ni dharura inayosisitizwa katika jamii zote za kibinadamu, na wakati alipotumilizwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) ilikuwa miji ya waarabu inaishi katika hali ya kutokuwa na mpangilio wa kiislamu, kwa namna ambayo mwenye nguvu anamkandamiza aliye dhaifu (mnyonge msonge), inatawala hali ya fujo (kukosekana nidhamu na mpangilio), na watu wanashindwa kusafiri na kuzihami nafsi zao isipokuwa kwa nguvu na mapatano baina ya makundi ya watu ambayo yanasaidiana katika (kuweka amani), wala hawakuwa na mpangilio au sharia na kanuni inayowalinda watu kutokana na uadui wa watu wengine. Amani ilikuwa ni ya watu wote tokea ilipodhihiri dola ya kiislamu, ikapatikana katika mji wa Madina na kuifanya (amani) ni katika malengo yake ya kwanza. Kwa hakika kukusanya kati ya kuzuia uovu na kumsimamishia adhabu aliekosea na kuzihifadhi haki na kupangilia uadilifu na kuieneza amani, ni jambo ambalo ni katika matakwa ya kibinadamu baada ya dini na tauhidi ikifatana na kupata riziki (lishe), na yote haya yanapelekea katika ijaazi iliyo wazi katika neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Basi na wamuabudu Bwana wa nyumba hii (al-Kaaba). Ambaye

[90] Angalia Muhammad Fat'hi Uthman katika "Asili ya fikra za kisiasa na kiislam".

anawalisha (wakati waarabu wenzi wao wamo), katika njaa, na Anawapa amani (wakati wenzi wao wamo) katika khofu). Suratu Quraish, aya (3-4). Bila shaka hii ni Tauhidi na riziki na amani inayofuatana katika ijaazi hii ya ki Mwenyezi Mungu na imefungamanishwa na nyumba ya Mwenyezi Mungu (Mtukufu) na kibla cha waislamu ambayo ndio alama ya sehemu hiyo, ni nidhamu (mpangilio) na dini wakati huo huo. Na aya za Qurani zimekuja ili ziwakumbushe watu juu ya umuhimu wa amani na imefungamanishwa na riziki. Katika neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Ambae amewalisha (wakati waarabu wenzi wao wamo) katika njaa, na Akawapa amani (wakati wenzi wao wamo) katika khofu). Suratu Quraish, aya (4).

Pia neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi, kama Alivyowafanya makhalifa wale waliyokuweko kabla yao. Na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, wawe wananiabudu hawanishirikishi na chochote. Na watakao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri zetu) Suratu An-Nur, aya (55). Pia neno lake: (Humo mna ishara zilizo wazi (za kuonyesha utukufu wake na ukongwe wake miongoni mwa hizo ni) mahali alipokua akisimama Ibrahim, na anayeingia (nchi hiyo) anakua katika salama. Na Mwenyezi Mungu amewajibia watu kufanya hija katika nyumba hiyo, yule awezae kufunga safari kwenda huko. Na atakayekanusha (asende na hali yakua anaweza) basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kuwahitajia walimwengu). Aali Imra, aya (97). Na pia neno lake: (Na (kumbukeni) aliposema Ibrahim “Mola wangu Ujaalie mji huu wa (Makka) uwe na amani. Na uniepushe mimi na wanangu na

kuabudu masanamu”). Suratu Ibrahim aya (35). Na pia katika neno lake mtukufu: ((Hapana shaka kuwa) wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na ushirikina kua hao ndio watakaopata amani, nao ndio walioongoka) Qur’ani Tukufu, Suratu Al-An-Am aya (82).

Aidha Mwenyezi Mungu Mtukufu amebainisha katika visa vya mitume waliopita umuhimu wa Imani katika maisha ya mataifa, ama katika kaumu ya Nabii Swaaleh. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: (Je, (mnafikiri kuwa) mtaachwa salama katika haya yaliyopo hapa (kwenu)). Suratu Ash-Shuaraa, aya (146).

Ama kuhusu miji yote na mataifa mengina, Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: (Au watu wa miji (hiyo) wameaminisha yakuwa adhabu yetu haitawafikia mchana, hali wanacheza? Je, wameaminisha kuadhibiwa na Mwenyezi Mungu hawaaminishi adhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ila watu ambao (watakuwa) wenye khasara). Al-Aaraf, aya (98-99). Pia katika neno lake: - (Na Mwenyezi Mungu anakupigieni mfano wa mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikiujia kwa wingi kutoka kila mahali. Lakini ukazikufuru neema za Mwenyezi Mungu, kwa hiyo Mwenyezi Mungu akauvisha vazi la njaa na khofu kwa sababu ya yale waliyokua wakiyafanya). Qur’ani Tukufu, An-Nahl, aya (112).

Aidha Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikua anawabashiria Maswahaba wake kama ilivyopokewa katika sehemu zaidi ya moja yakwamba amani itaenea kwa dini hii, na katika hizo ni neno lake alipomwambia Adiyy ibn Haatim: “Naapa kwa Mwenyezi Mungu inakaribia kusikia yakua mwanamke anatoka mji wa Qaadisiyya akiwa juu ya ngamia

wake mpaka aje azuru nyumba hii (al-Kaaba) hana anachoogopa”.[91] Na pia alisema: “Wallwaahi Mwenyezi Mungu (Mtukufu) atalitimiza jambo hili (uislamu) mpaka atembee mtu aliyepanda mnyama kutoka San,aa hadi Hadhramauti, haogopi isipokuwa Mwenyezi Mungu (Mtukufu) au mbwa mwitu juu ya mbuzi wake, lakini nyinyi mna haraka”.[92]

Amani na usalama kati ya watu ndio ilokua katika malengo muhimu ya uislamu, na kwa hilo ililazimu kuipiga vita hofu na mambo yanayopelekea watu kuwa na hofu. Na kwa sababu hiyo ndipo ikawa lengo la uongozi wa dola iliyokuwa ikiongozwa na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) ni kuhakikisha amani.

Naye Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikua anatilia mkazo katika hadithi na mazungumzo yake kati ya watu juu ya kuwapa amani na kutokuwafanyia uadui, na miongoni mwa maneno mashuhuri aliyoyasema katika hija ya kuagana na waislamu alisema: “Zindukeni, ni mwezi gani ambao mwaujua kua ni mtukufu Zaidi?” Wakasema: “Ni mwezi wetu huu -yaani mwezi wa Dhul-hijja”, kisha akasema: “Je, ni mji gani ambao mnaujua kua ni mtukufu Zaidi?” Wakasema: “Ni mji wetu huu (yaani Makka)” Akauliza tena: “Ni siku gani mnayoijua kua ni tukufu zaidi”, wakasema: “Ni siku yetu hii (siku ya Arafa)” Akasema: “Hakika Mwenyezi Mungu (Mtukufu) na mwenye kushinda Ameharamisha damu zenu juu yenu na mali zenu na heshima zenu, isipokuwa kwa haki yake, kama alivyoharamisha

[91] Attwabariy Tarehe yake juz 3 Uk.150. pia angalia, ibnu Abii Shaibah, Al-Maghaaziy Uk 142 na ibnu Hishaam Assiratun-Nabawiyah Juz 4 Uk 581

[92] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake Maandishi ya Al-Maghaaziy, mlango wa Yaliyompata mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) na maswahaba wake kutoka kwa makafiri wa Makka. Juz 5 Uk 238.

kufanya maovu katika siku yenu hii, katika mji wenu huu, ndani ya mwezi wenu huu. Je, nimefikisha jambo hilo?" Aliuliza mara tatu, katika mara zote hizo wanamjibu ndio, ndipo akasema: "Mna nini" au akasema: "ole wenu msirejee baada yangu kuwa makafiri, baadhi yenu wakawa wanazikata shingo za wengine".[93]

Bila shaka alitilia mkazo umuhimu wa amani katika maisha ya mwanadamu kwa neno lake: "Yeyote atakayeamka miongoni mwenu akiwa na amani kwa familia yeke ana afya ya mwili wake, ana chakula cha siku yake (hiyo) ni kana kwamba ameletewa (ameipata) dunia yake yote"[94]. Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) amesema: "Haifai kwa muislamu kumtishia ndugu yake muislamu".[95] Na katika dua yeke alikuwa akiomba kwa kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu tusitiri aibu zetu, na utupe amani tutokane na hofu yetu (tuliyonayo)"[96].

Kwa hakika dola ya kiislamu katika mji wa Madina ilitekeleza sehemu yake katika kueneza amani na salama kati ya watu,[97] waislamu na wasiokuwa waislamu na hilo lilikuwa ndio msingi wa mkataba wa Madina kati ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) na wakazi wote wa Madina, pamoja na makabila yake. Ilikuwa ndio ulinzi unaowashirikisha kati yao na kueneza amani

---

[93] Katika riwaya ya Bukhariy, katika Sahihi yake kuhusu maandishi ya adhabu za kisheria. Hadithi nambari 6785, Ibn Hazmi, Al-Muhalla, Maandishi ya kuhusu hijja Juz 4. Uk 84

[94] Ameipokea Tirmidhy katika Zuhdi, Hadithi namba 2346. Juz 4 Uk 574

[95] Ameipokea imam Ahmad katika musnad yake Juz 5, Uk 262.

[96] Ameipokea imam Ahmad katika musnad yake Juz 2, Uk 25.

[97] Kwa urefu zaidi katika maudhui haya, angalia (Dr. Abdallah Turkiy, "amani na umuhimu wake katika maisha ya watu katika uislamu" chapa ya "wizara ya mambo ya kiislamu" Riyadh 1417H)

ndani ya mji huo, na kutokuwasaidia wale wanaosababisha hofu kwa watu wake, miongoni mwa wazushao mambo ya utovu wa usalama na wasiokuwa hao.[98] Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anafatilia yeye mwenyewe amani ya mji wa Madina na usalama wa watu wake na wanaoingia mjini humo, na alikuwa anasimamisha adhabu za kisharia kwa watu waovu wanaofanya uharibifu katika ardhi, wanaomwaga damu, wanaovuruga amani ya watu na usalama wao. Imamu Bukhariy katika sahihi yake ameweka maandishi aliyoyaita (maandishi ya adhabu za kisharia na yanayotahadharishwa katika mambo ya adhabu hizo). [99]Ameleta habari hiyo katika milango tofauti ikiwemo "*mlango wa kutekeleza adhabu za kisharia kwa mtukufu na mtu mnyonge*"[100] na mlango wa (karaha, ubaya, haramu) ya kuombea msamaha katika adhabu ya kisharia muda imeshapelekwa kwa kiongozi.[101] Katika mlango huo imepokewa hadithi kutoka kwa bibi A'isha (Radwiallwaahu Anhaa) kua makuraishi liliwatia udhia (kero) jambo la mwanamke wa ki bani-Makhzuum aliyeiba wakasema: "Ni nani atakayezungumza na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kuhusu habari hiyo", wakasema, "Nani anaeweza kua na ushujaa wa kuzungumza nae isipokuwa Usama ibnu Zaid, kipenzi cha Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam)". Ndipo Usama alipomzungumzia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akamwambia: "Ewe Usama! Unamuombea mtu juu ya hukumu ya Mwenyezi Mungu" kisha Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akasimama

---

[98] Angalia Abdul-Aziiz al-Umariy, Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa manabii-Dini na dola-(Mkataba wa Madina) sehemu ya 3 uk 551

[99] Sahihi ya Bukhariy Juz 8 Uk 13

[100] Sahihi ya Bukhariy Juz 8 Uk 16.

[101] Sahihi ya Bukhariy Juz 8 uk 16.

akawahutubia watu akasema: “Hakika liliwaangamiza wale waliokuweko kabla yenu, walikuwa akiiba mtu mtukufu miongoni mwao wanamuacha na akiiba mtu dhaifu wanamsimamishia adhabu, naapa na Mwenyezi Mungu, lau Faatwima binti Muhammad (Radhwiallwaahu anhaa) angeliiba, ningemkata mkono wake”.[102]

Bila shaka imamu Bukhari katika sahihi yake ameweka mlango, kuhusu neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu (na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao, malipo ya yale waliyoyachuma ndiyo adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na mwenye hekima)[103] Suratu Al-Maidah aya (38).

Kwa hakika Mtume Muhammad (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliitekeleza adhabu ya mwizi kwa yule mwanamke wa kibanii Makhzoum, wala utukufu wake, wala uombezi wa Usamah bin Zaid na wengineo katika watu watukufu wa Makka haukumzuia kutomsimamishia hukumu ya kisharia. Na linalodhihiri ni kua yeye alitekeleza hukumu ya mwizi zaidi ya mara moja katika uhai wake (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).[104]

Hukumu ya wizi ilikuwa na mchango mkubwa katika amani ya watu na mali zao, na wezi kuogopa kusimamishiwa adhabu, ilifikia hadi ya kuwa wizi ulipungua na ulikaribia kukosekana katika zama za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).

---

[102] Ameipokea Bukhariy katika Sahihi yake, Maandishi ya hukumu za kisheria mlango wa, kusimamisha adhabu kwa mtukufu na mnyonge, Juz 8 Uk 16.

[103] Sahihi ya Bukhariy ‘Maandishi ya adhabu za kisheria’ mlango wa 13, Juz 8 Uk 16.

[104] Angalia Sahihi ya Bukhariy Juz 8 Uk 15-18.

Hapana shaka kuwa mji wowote na jamii yoyote inayotekeleza adhabu ya wizi, wizi unapungua na watu na mali zao wanakuwa na amani. Pia jambo hili lilikuwa liko wazi kua katika adhabu na hukumu ya kulipiza kisasi linazuia watu kufikiria kuuwa na kumwaga damu, wakishajua kuwa damu zao ziko kwenye uangalizi na kuwa kisasi kiko nyuma yao, wakifanya jambo la kumwaga damu za wengine. Na kwa kuzingatia hilo ni kuwa bila shaka katika kisasi kuna kuzihami (kuzihifadhi) damu na maisha ya watu kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Mtakua nao uhai (mzuri) katika kulipiza kisasi enyi wenye akili, ili msalimike). Al-Baqarah, aya (179).

Kwa hakika pia imejulishwa na kujulikana hukumu na adhabu ya kufanya uovu, nayo ni ie iliyopokewa katika neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Basi malipo ya wale wanaopingana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake (kwa kufanya aliyowakataza) na kufanya uovu katika nchi ni kuuwawa na kusulubiwa au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho (mkoni wa kulia kwa mguu wa kushoto na mkono wa kushoto kwa mguu wa kulia) na kuhamishwa katika mji. Hii ndiyo fedheha yao katika dunia: na akhera watapata adhabu kubwa, isipokuwa wale watakaotubia kabla hamjawakamata. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe (na) mwingi wa kurehemu). Al- Maidah, aya (33-34).

Mtume (Alaihissalaam) alijua haja ya watu ya kuwa na amani na kuishi bila kutiwa khofu, ndipo akawapa amani maadui wake katika mji wa Makka wakati alipoingia mjini humo akiwa ameufungua kwa namna ambayo alitangaza kuwa yeyote atakayeingia nyumba ya Abi-Sufyaan atapata amani, na yeyote atakayejifungia nyumbani kwake amepata amani, na yeyote

atakayeingia msikitini (msikiti wa Haram, Makka) yumo katika amani.[105] Alikuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) anajua (kabisa) umuhimu wa amani katika maisha ya watu na kwa sababu hiyo, ndipo ikawa miongoni mwa jambo la kwanza alilowakumbusha watu baada ya kuifungua Makka ni kuharamisha kumwaga damu.[106]

## UJENGAJI WA TABIA NA MAADILI[107]

Bila shaka jamii zote za kibinadamu na hasa zile za kiarabu, tabia zao ziliharibika na baadhi yao wakawafanyia ubaya wengine na baadhi yao wakawadharau wengine.[108] Na ilikuwa bidii ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika kuibadilisha jamii ya Makka kiundani, ni kujaribu na kufanya bidii yenye nguvu na ya kikweli kama ilivyokuwa bidii yake ya kueneza ulinganizi wa kiislamu na yanayofungamana nao katika sharia na jengo lake, kitamaduni na kitabia na mafungamano ya kibinadamu na uhusiano wa ndani kabisa kati ya watu wa jamii hiyo kwa jumla, kuanzia kwa wenye ukuruba, mababa na watoto

---

[105] Angalia Abdul-Aziiz al-Umariy 'Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa mitume na manabii-dini na dola (Fat,hu Makka) Sehemu ya 3 Uk 797.

[106] Angalia Sera ya ibn Hishaam Juz 4 Uk 415.

[107] Huenda ikawa mazuri Zaidi yaliyoelezwa katika maudhui haya ni aliyoyakusanya Bukhariy katika "Kitaabul adab" katika milango tafauti, katika tabia na usamehevu na kuamiliana na jirani na masikini na watu wa kizazi na wasiokuwa hao katika milango inayozidi (128). Angalia sahihi ya Bukhariy Juz 7 Uk 68-125.

[108] Kwa urefu Zaidi katika maudhui haya, rejea: Dr Ahmad ibn Abdul-Aziiz Ibnu Qaasim al-Haddaad tabia za mtume katika Qur'an na Sunna katika juzuu tatu katika toleo la Daarul-Gharbi, al-Islaami, Bairut chapa ya 2, 1419H

wao katika muingiliano baina ya dini, tabia na jamii. Na kwa hakika makuraishi waliipinga na kuizuia daawa (ulinganizi) hiyo, wakaikingamia na kumpiga vita mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Makuraish walimuudhi yeye (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) pamoja na maswahaba wake, jambo lililomfanya kutafuta sehemu nyengine ili asimamishe jamii ya kiislamu inayojitenga na kujulikana kwa utamaduni na tabia zake na muiongiliano wake, ndipo kukawa kuguria Madina ndio mwanzo wa kujenga jamii mpya ya kibinadamu iliyo ya kiislamu yenye amani, kwa namna ambayo walikuja muhaajirina wakazoeana na wakaungana, wakaunga udugu pamoja na Answaar ikapatikana kutoka kwao ile iliyojulikana kama nidhamu ya udugu ambayo ilidhihirisha madini (asili) ya jamii iliyo safi, yenye kuunganisha udugu kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na pia (wapewe) wale waliofanya maskani yao hapa (yaani Madina) na wakautakasa uislamu (wao barabara) kabla ya (kuja) hao (muhajirina huko Madina) na wakawapenda hao waliohamia kwao, wala hawapati, hawaoni dhiki nyoyoni mwao kwa hayo waliyopewa (hao muhaaajirina) na wanawapenda kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo. Na waepushwao na ubahili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli). Suratu- Al-hashr, aya (9).

Jengo la jamii ya maswahaba na uma wote uliokuja baada yao lilikuwa ni la kushikamana, pamoja na udugu baina yao. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na (kadhalika wapewe mali hao waislamu) waliokuja baada yao (wakawa wanapendana na waislamu waliotangulia (wanawaombea dua) wanasema: Mola wetu tusamehe sisi na ndugu zetu waliotangulia (kufa) katika uislamu. Wala usijaalie katika nyoyo zetu undani kuwafanyia

waislamu (wenzetu) mola wetu! Hakika wewe ni mpole sana mwenye rehema mno. Suratul-Hashri aya (10).

Kwa hakika kuzitakasa nafsi na kuzijenga tabia kulikuwa ni katika asili ya daawa ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kama ilivyokuja katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Kama tulivyomleta Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kwenu anayetokamana na nyinyi, anakusomeeni aya zetu na kukutakaseni na kukufundisheni kitabu na hikima na kukufundisheni mliyokuwa hamuyajui). Suratu Al-Baqara, aya (151). Na pia neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Yeye ndiye aliyeleta Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika watu wasiojua kusoma, anayetokana na wao, awasomee aya zake na kuwatakasa na kuwafunza kitabu na hikima (ilimu nyenginezo). Na kabla ya haya walikuwa katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri). Suratu Al-Jumu,a aya (2).

Kwa hakika sharia tofauti za dini ya kiislamu zimekuja ili kuyatia nguvu mahusiano mazuri kati ya watu wa jamii[109] na kati ya familia moja, ndipo akasema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam); ”wema ni tabia nzuru”.[110] Na pia akasema: “Hakika katika wabora wenu ni wale wenye tabia nzuri”.[111] Na pia uislamu umetia mkazo kuyaboresha mafungamano ya watoto na baba zao na baba na watoto wao, kwa namna ambayokwamba amri ya kimungu nikuwatendea wema wazee wawili, ikimaanisha

---

[109] Angalia Al-Khauliy Muhammad Abdul-Aziiz, Al-Adabun, Nabawiy, idhwaatun-baaligha wahikamun-baaligha, chapa ya kwanza, Daarul-Qalam, Bairut. 1406

[110] Ameipokea imam Ahmad katika Musnad yake Juz 2 Uk 250.

[111] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake “Maandishi ya tabia, mlango wa tabia njema na ukarimu na yale yanayochukiza katika ubahili Juz 7 uk 82.

kutengeneza mafungamano baina ya jamii na nyengine na kueneza kuwasiliana na kuoneana huruma, na kwa hakika kuwafanyia mema wazazi wawili kumefungamanishwa na kumtii Mwenyezi Mungu, kama alivyosema katika Qur'ani: (Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yeyote ile yeye tu, na (ameagizia) kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee (naye yuko) pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie hata Ah! Wala usiwakemee, na useme nao kwa msemo wa heshima (kabisa) na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa (njia ya kuwaonea huruma (kwa kuwaona wamekua wazee) na useme: mola wangu, warehemu (wazee wangu) kama walivyonilea katika utoto). Banii Israel aya (3-24).

Kama ambavyokwamba pia uislamu umetilia mkazo jambo la wenye ukaribu na kuwa na mafungamano mazuri nao katika neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na umpe jamaa (yako) haki yake, na maskini na msafiri aliyeharibikiwa, wala usitawanye (mali yako) kwa uharibifu). Suratu-Banii Israil aya (26).

Ni kama ambavyokwamba pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) yuko katika daraja ya juu ya tabia njema kama alivyosifiwa na Mwenyezi Mungu (Mtukufu) katika neno lake: (Na bila shaka una tabia njema kabisa). Suratu Al-Qalam, aya ya (4). Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaamrisha watu kumuiga yeye katika neno lake: (Bila shaka mna mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana). Suratu Al-Ahzab aya (21). Na kwa

hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) amesema: “Kwa hakika nimetumwa ili nije nikamilishe tabia njema”.[112]

Mtume alikuwa mnyenyekevu anawatembelea wagojwa, anafata jeneza, na kuitikia mwaliko, na anachukia kusimamiwa na watu, na anawanyenyekea wakubwa na wadogo. Alifikia kua hata mgeni anapokuja anampata kati ya maswahaba wake (anachanganyika nao, hajibagui) kwa kikao chake. Alikuwa mkarimu anaamrisha ukarimu, alikuwa mtukufu anaamrisha mambo matukufu, mwenye kujizuia na ubadhirifu, anaamrisha watu kuwa ni wenye kujizuia na kutosheka na vilivyomo mikononi mwa watu, ni mtu shujaa aliye mpole na anaamrisha upole, mwenye tabia laini anaamrisha ulaini, mwenye harufu nzuru, msafi anaamrisha waislamu kuwa kama hivyo, na juu ya sifa zote hizi, inakuja sifa ya kuwa na adabu nzuri na Mwenyezi Mungu (Mtukufu), kuanzia katika Tawhidi na kuridhika kwa kumuabudu yeye na kuwa na dhana njema naye na kumtegemea, na kumuogopa na kuridhika na aliyoyagawanya na kutarajia mema yaliyoko kwake na kumcha yeye na kumuogopa kwa yaonekanayo na yasioonekana na kutaanasi kwa kumtaja na kumshukuru na kumwabudu vyema, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Hakika wanaoamini kweli ni wale ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu Mtukufu nyoyo zao hujaa khofu; na wanaposomewa aya zake huwazidisha imani na wakamtegemea Mola wao tu basi; (hawana kuamini mizimu wala pango wala shetani wala makaburi wala mengineo. Ambao wanasimamisha sala wanatoa zaka katika yale tuliyowapa). Suratu Al-Anfal Aya (3-4). Na neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Basi

---

[112] Ameisahihisha al –Albaniy, angalia musnad ya Imam Ahmad Juz 2 uk 381. Na imepokewa kwake vile vile “Ili nikamilishe tabia njema”

nikumbukeni kwa kunishukuru kwa hii neema niliyo kuneemesheni ya kukuleteeni Mtume (Nami) nitawakumbukeni na nishukuruni wala msinikufuru). Al-Baqara, aya (152). Pia Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: (Mutakuwaje hamuweki heshima ya Mwenyezi Mungu na hali yeye amekuumbeni namna baada ya namna?). Suratu Nuh, aya (13-14). Na pia amesema: (Na hushughuliki katika kazi yoyoyte, wala husomi humo (Kitu chochote) katika Qurani wala hamfanyi kitendo chochote (chingine) isipokuwa sisi tunakuwa mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo. Hakifichikani kwa Mola wako kitu chochote (hata) kilicho sawa na uzito wa mdudu chungu, la katika ardhi wala katika mbingu. Wala (hapana) kidogo kuliko hicho wala kikubwa isipokuwa kimo katika kitabu (cha Mwenyezi Mungu) kielezacho (kila kitu)). Suratu Yunus, aya (61). Na katika kukumbusha kua na adabu nzuri na Mwenyezi Mungu, Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) amesema: "Muoneeni haya Mwenyezi Mungu ukweli wa kumuonea haya, kihifadhini kichwa na kilichoyakusanya na tumbo na ilivyoshikamana navyo, na yakumbukeni mauti na kuoza"[113] na pia amesema:- "Mwenyezi Mungu Mtukufu ana haki ya kuonekana haya kuliko wanadamu".[114] Na katika uzuri wa adabu na Mwenyezi Mungu, ni kurejea kwake na kuomba msamaha na kurejea na kumkimbilia yeye kama alivyosema: (Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu, mimi kwenu nimuonyaji waziwazi ninayetoka kwake) Suratu Adh-Dhaariyaat, aya (50). Na pia amesema: (Na neema yoyote mliyonayo, basi imetoka kwa Mwenyezi Mungu (Na nyinyi

[113] Imam Ahmad katika musnad yake, Juz 1, Uk 387.

[114] Ameipokea Bukhariy katika "Kitaabul-Ghusli" mlango wa "Aliyeoga uchi pekeyake akiwa amejitenga na aliye jisitiri, kujisitiri ni bora". Juz 1 Uk 73.

hamshukuru). Kisha inapokuguseni dhara, mara yeye mnamlilia (mnamlalamikia)) Suratu An-Nahl, aya (53). Na pia amesema: (Basi nikumbukeni (kwa kunishukuru kwa neema niliokuneemesheni, Mtume) (Nami) nitakukumbukeni, na nishukuruni wala msinikufuru). Al-Baqara, aya (152). Na pia neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (wafanyaji mema, wanaume au wanawake, hali yakua ni waislamu, tutawahuisha maisha mema, na tutawalipa ujira wao (Akhera) mkubwa kabisa kwa sababu ya yale mema waliyokua wakiyatenda). Suratu An-Nahl aya (97). Na pia amesema (Na isomwapo Qurani isikilizeni na nyamazeni ili mpate kurehemewa). Al-Aaraf, aya (204).

Miongoni mwa tabia njema ulizoleleka nazo umma wa kiislamu ni kua na adabu nzuri na Mtume wake katika uhai wake na baada ya mauti yake, kama ilivyo katika neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Enyi mlioamini! Msitangulize (kusema lenu) mbele ya neno la) Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake; na mcheni Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia, mwenye kuona. Enyi mlioamini msipaze sauti zenu kuliko sauti ya Mtume wala msiseme kwa sauti zenu za nguvu kama mnanyosemezana nyinyi kwa nyinyi visije vitendo vyenu vikakosa thawabu, na hali hamtambui. Kwa hakika wale wanaoangusha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa kumuogopa Mungu. Basi yatakuwa kwao maghufira. Wale wanaokwita nyuma ya vyumba; (uko ndani kwako wanakuja kukugongea madirisha na kukwita), wengi wao hawafahamu (adabu). Na kama wangekungoja mpaka uwatokee ingekua bora kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghufira (na) Mwenye rehema). Suratu-Al-Hujurat, aya (1-5).

Kwa hakika Qur'ani imewaamrisha maswahaba wa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) kuzifata amri zake na kutokumuasi, katika neno lake Mtukufu: (Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu anawajua miongoni mwenu waondokao kwa utoro wakajificha. Basi wajihadhari wale wanao kaidi amri yake, usije ukawapata msiba au ikawafika adhabu iumizayo). Suratu An-Nur Aya (63). Na neno lake: (Naapa kwa (haki ya) Mola wako. Wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa). Suratu Al-Nisaa, aya (65). Aidha Qurani tukufu imetilia mkazo juu ya kua na adabu nzuri na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) na wasimkimbie akiwa katika jambo linalohusiana na watu wote isipokuwa kwa idhini yake, na hilo liko katika kauli yake Mwenyezi Mungu: (Waislamu wa kweli ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na wanapokuwa pamoja nae katika jambo linalohusiana na wote, hawaondoki mpaka wamuombe ruhusa (Mtume) kwa hakika wale wanaokuomba ruhusa, hao ndio wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na watakapokuomba ruhusa kwa ajili ya baadhi ya kazi yao, mruhusu umtakaye miongoni mwao (ukiona kua kweli ana udhuru) na uwaombee maghufira kwa Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu ni mwingi wa msamaha (na) mwingi wa rehema. Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu anawajua miongoni mwenu wale waondokao kwa urongo wakijificha. Basi wajihadhari wale wanaokaidi amri yake. Usije ukawapata msiba au ikawafika adhabu iumizayo). Suratu N-Nuur, aya (62-63). Na

pia neno lake Mtukufu: (Haiwi kauli ya waislamu wanapoitwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili Ahukumu baina yao, ila kusema; “tunasikia na tunakubali”, na hao ndio watakaofuzu. Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kumheshimu Mwenyezi Mungu na kumwogopa, hao ndio wenye kufuzu (kufaulu). Na wanaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kiapo chao kikubwa yakwamba ukiwaamrisha (kutoka kwenda vitani) bila shaka wataondoka (wende). Sema “msiape”; utii wenu unajulikana (wa uwongo tu) Hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) mnayoyatenda”. Sema “Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume, na kama mkikengeuka basi ni juu yake huo (mzigo) aliotwika; (kazi aliyopewa kufikisha ujumbe). Na juu yenu (huo mzigo) mliotwikwa. (kutii). Na mkimtii mtaongoka; Hapana juu ya Mtume ila kufikisha (ujumbe wake) waziwazi). Suratu An-Nur, aya (52-54).

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikua ameupa mgongo ulimwengu na anaamrisha waislamu kua kama hivyo, alisifika na sifa tukufu ambazo zinahimiza usafi na kuheshimu hisia za wengine katika chakula chake na kinywaji chake na nguo zake na muonekano wake. Na alikua anaamrisha kueneza mapenzi kati ya watu, amesema rehema na amani zimshukie: “Je siwajulisheni yule anayependeza zaidi kwangu na aliye karibu na mimi (kwenye makazi yangu siku ya kiama?) ni wale wenye tabia njema walio wanyenyekevu wanaozoea na wanazoeleka”.[115] Pia alikuwa anasema: “Yule ambaye inampendeza kuepushwa na moto na aingie peponi na kimjie kifo chake hali yakua

[115] Ameipokea Bukhariy “Kitaabul,manaaqib” mlango wa “fadhila za maswahaba” Juz 4 uk 218. Na imam Ahmad katika Musnad yake Juz 4 Uk. 193.

anashuhudia kua hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kua Muhammad ni mja na Mtume wake, na awatendee watu yale anayopenda watu wamtendee”.[116] Pia ni kama alivyosema: “Naapa na yule ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake, hamtoingia peponi mpaka muwe waumini, wala hamtokua waumini hadi mpendane, je, siwajulishi kitu ambacho mkikifanya mtapendana, peaneni salamu baina yenu”.[117] Na pia alikuwa akiwasalimia watoto anapopita mbele yao. Na pia Mwenyezi Mungu (Mtukufu) ameamrisha kuomba ruhusa na kupeana salamu kama ilivyo katika neno lake: (Enyi mlioamini msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa (mpige hodi) na muwatolee salamu waliomo humo. Hayo ni bora kwenu; huenda mtakumbuka (mkaona ni mazuri haya mnayoambiwa)). Suratu An-Nur, aya (27). Na neno lake mtukufu aliposema: (Na waja wa Mwenyezi Mungu anaowapenda ni wenye sifa hizi: Ni wale wanaokwenda (na kurejea) ulimwenguni kwa unyenyekevu na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu (maneno ya salama). Al-Furqan, aya (63). Na neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Wala usitembee (usende) katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala huwezi kufika urefu wa majabali). Suratu Bani-Israel, aya (37). Pia anasema: (Wala usiwatazame) usiwafanyie watu jeuri kwa upande mmoja wa uso, wala usende katika nchi kwa maringo; Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunae, ajifahirishae). Suratu –Luqman, aya (18). Pia ni kama alivyokuwa akiamrisha upole ambao ni moja katika sababu za mazoea katika familia na katika jamii akasema; “Hakika

[116] Angalia Abuu-Bakar al-Jazaairiy Minhajul-Muslim uk 103.
[117] Swahih Muslim “Kitaabul iiman” Juz 1 uk. 53

Mwenyezi Mungu Mtukufu anapenda upole katika mambo yote".[118] Pia ni kama alivyosema: "Haujawa upole katika jambo lolote isipokuwa hulifanya likawa zuri".[119] Na bila shaka Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliutekeleza upole kivitendo pamoja na maswahaba wake kama Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyosema akisifia jambo hilo: (Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekua laini kwao (Ewe Muhammad) na kama ungekuwa mkali na mwenye moyo mgumu, bila shaka wangalikukimbia. Basi wasamehe wewe na uwaombee msamaha (kwa Mwenyezi Mungu) na ushauriane nao katika mambo. Na ufungapo nia mtegemee Mwenyezi Mungu Mtukufu (tu ufanye hili uliloazimia). Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao). Suratu Aali-imran, aya (159). Na pamoja na upole na ulaini Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikua na mapenzi na pupa juu ya umma wake, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Amekufikieni Mtume) aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni. (Na) kwa walioamini ni mpole na mwenye huruma) Suratu At-tauba, aya (128). Na neno lake Mwenyezi Munngu; (Usinyoshe (usikodoe) macho yako (kutazama) yale tuliyowastarehesha makundi mbalimbali ya hao (wabaya) wala usiwahuzunikie (huzuni kubwa ya kujiumiza nafsi yako). Na inamisha bawa lako kwa wanaoamini (uwafunike kama kuku na ndege wengine wanavyofinika watoto wao. Yani kuwa na huruma na hawa)). Al-Hijr, aya (88). Na pia neno lake: (Na

---

[118] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake "Kitaabul-adab" mlango wa "Upole katika mambo yote" Juz 7 uk 8.

[119] Ameipokea Muslim katika Sahihi yake "Kitaabul-birr" mlango wa "Fadhila za upole" Juz 8 Uk. 22. Na ameipokea Imam Ahmad katika Musnad yake Juz 6, Uk 58-112.

uinamishe bawa lako kwa yule anaekufata katika wale walioamini). Ash-Shuaraa, aya (215).

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa ni mfano wa upole na ukarimu pamoja na tabia njema, alimuelezea hilo bibi Khadija (Radwiallwaahu Anhaa) ndipo akatulia kutokana na hofu iliyokuwa imempata baada ya kuteremshiwa wahyi, akimkumbusha na kumtajia tabia zake tukufu, alimwambia: “Naapa kwa Mwenyezi Mungu yakwamba hawezi kukuacha abadan, kwa hakika wewe unaunga kizazi na unasema kweli na unawasaidia waliolemewa, na unaleta (kuchuma) visivyo patikana (ukawasaidia watu) na unawakirimu wageni, na unasaidia makundi ya haki”.[120] Na katika hilo kunawathibitishia uma na kutilia nguvu yakwamba: (tabia njema na mambo ya kheri ni sababu ya kusalimika kutokana na kifo kibaya).[121]

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alipoingia mji wa Makka hali yakuwa ameufungua, alikuwa ni mnyenyekevu mwenye kuinamisha kichwa chake pasi na kujionyesha wala kiburi.[122] Alikuwa anasimama na mwanamke dhaifu na mtoto, anawasikiza na anawazungumzisha na kuwakidhia haja zao.[123] Na huenda ikawa hadithi ya Anas inalisherehesha neno lake Mwenyezi Mungu huhusu tabia hizo zilizo tajwa na kuashiriwa

[120] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake mlango wa kuelezea ilivyokuwa kuanza kwa wahyi kwa mtume nayo ni hadithi ya 3 kwa Bukhariy katika sahihi yake Juz 1 uk 3.

[121] Ahmad ibn Abdul-aziiz al-Haddad, Tabia za mtume katika Qur’ani na Sunna. Juz 1 Uk 77.

[122] Angalia Abdul-Azziz al-Umariy “Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa manabii-dini na dola- (Fat,hu Makka). Sehemu 3 Uk. 802.

[123] Angalia Swahih Muslim, mlango wa “Ukuruba wa Mtume na watu”.

katika Qurani anasema: “Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa akiwatembelea wagonjwa na kuhudhuria jeneza, na alikuwa akipanda punda na akiitikia mualiko wa mtumwa.[124] Alikuwa hachukii kupanda mnyama pamoja na mtu mwengine au mtoto, mara nyingi alikua akimpandisha Usama ibn Zaid nyuma ya mnyama wake na mara nyengine alikua akiwapandisha wake zake. [125] Na kwa hakika alisema; “Hakika Mwenyezi Mungu (Mtukufu) ameniteremshia wahyi yakwamba, nyenyekeeni hadi wengine wasiwafanyie jeuri wengine wala mmoja asijifakhiri juu ya mwengine” .[126]

Alikuwa anafanya kazi pamoja na maswahaba wake, akawa anatafuta kuni katika baadhi ya safari zake na anafanya baadhi ya kazi kama mtu mwengine yoyote. Na pia alishiriki katika kazi za kuujenga msikiti wake, kama ambavyokwamba alikuwa akishiriki katika kusaidia ahli yake katika kufanya kazi za kinyumbani (anakuwa katika kusaidia kazi za familia yake).[127] Na kwa hakika alizoea tabia ya haya na Mwenyezi Mungu Mtukufu amemsifu kwa hilo katika neno lake: (Enyi mlioamini msiingie nyumba za Mtume ila mpewe ruhusa ya kwenda kula pasipo (kwenda kukaa) kungojea kiive. Lakini mtakapoitwa ingieni na mnapokwisha kula tawanyikeni. Wala msiweke mazungumzo, maana jambo hili linamuudhi Mtume, naye anakuoneeni haya,

---

[124] At-Tirmidy “Kitaabul-Janaaiz” Mlango wa (32) hadithi nambari 1017 Juz 3 Uk 337.

[125] Ameitoa Bukhariy “Kitaabul-adab” mlango wa “neno la mtu kusema, Mwenyezi Mungu anifanye kuwa fidia yako” Juz 7 uk. 116.

[126] Ameipokea ibn Maajah katika Sunan yake Mlango wa haya, nambari 4179 Juz 2 Uk 1399.

[127] Kutokana na hadithi ya A’aisha iliyoko kwa Bukhariy “Kitaabul-adab” mlango wa “namna anavyokuwa mtu kwa ahli yake” Juz 7. Uk. 83.

lakini Mwenyezi Mungu haoni haya kusema haki). Al-Ahzab, aya (53).

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa akihimiza watu kufanya uadilifu katika kulinganisha kati ya mambo ya kidunia na kiakhera, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na utafute-kwa yale aliyokupa Mwenyezi Mungu- makazi mazuri ya akhera, wala usisahau sehemu yako ya dunia na ufanye wema kama Mwenyezi Mungu alivyokufanyia, wala usitafute kufanya ufisadi katika nchi; bilashaka Mwenyenzi Mungu hawapendi mafisadi). Suratu Al-Qaswas, aya (77). Kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikua ana pupa yakuwajulisha maswahaba wake namna lilivyo pendo lake kwao, ndipo alipozungumza na Muadh ibn Jabal (Radhwallawaahu Anhu) siku moja akamwambia: "Ewe Muadh, Wallwaahi mimi nakupenda" Muadh akamjibu; "Ninakutolea fidia baba na mama yangu, (niko tayari kuwatoa fidia kwa kukukinga wewe ewe Mtume wa Mungu), na mimi pia nakupenda", Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akasema:- "Na kuusia ewe Muadh, usiache baada ya kila swala kusema, "Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie niweze kukutaja na kukushukuru na kukuabudu vizuri".[128] Pia alisema: "Mmoja wenu atakapompenda ndugu yake, basi na amjulishe yakwamba anampenda".[129]

Ni kama ilivyotangulia, pia alikuwa anahimiza kufanya kila jambo linaloeneza mapenzi kati ya watu, kama kutembeleana na kupeana zawadi[130] au kutabasamu ambako alisema kuhusu jambo

---

[128] Angalia musnad ya imam Ahmad Juz 5, Uk 245

[129] Ameipokea imam Ahmad katika musnad yake Juz 4 uk 30.

[130] Sunan Tirmidhy "Kitaabul-birri" uk 34 "katika yaliyokuja katika kukubali zawadi na malipo yake" hadithi nambari 1953 Juz 4 Uk 338.

hilo “Kutabasamu kwako usoni mwa ndugu yako ni sadaka”.[131] Na akawafundisha kuamkuana baadhi yao waamkue wengine (waamkuane wao kwa wao) kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na mnapoamkiwa kwa maamkio yoyote yale, basi itikeni kwa yalio bora kuliko hayo, rejesheni yayo hayo. Hakika Mwenyezi Mungu anafanya hesabu ya kila kitu). Suratu An-Nisaa, aya (86). Na kwa hakika imamu Bukhari ameweka katika kitabu chake maandishi ya habari ya kuomba ruhusa, mlango wa -*kutoa salamu ni katika uislamu*- [132] Kama ambavyo ameweka maandishi ya kuhusu habari ya imani, mlango aliouita mlango wa kujulisha kuwa imani ni katika uislamu, pia imam Tirmidhiy katika sahihi yake ameweka mlango wa yale yaliyotajwa kuhusu habari ya ubora (fadhila) za kutoa salamu.[133] Ni kama Qurani ilivyokataza watu kijibagua kutokana na wengine na akawakumbusha asili yao moja na akaharamisha baadhi yao kuwadharau wengine. (Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huenda wakawa bora kulko wao. Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane kwa majina mabaya (ya kejeli): jina baya kabisa kuambiwa mtu ni asi baada ya kuwa ni muislamu (Na) kufanya haya ni uasi) Na wasiotubu, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao). Enyi

---

[131] Sunanu-Tirmidhiy “Kitaabul-birri” Uk 36, “na yaliyokuja katika kutenda mema” katika hadithi namba 1956 juz 4, Uk 340. Ukusanyo wa Abdallwaah Najiib Saalim, yaliyopkewa kuhusu kutabasamu katika Sira ya Mtume katika kitabu alichokiita “Tabasamu za Mtume” chapa ya kwanza ya Daaru Iqra ya kidola, Cairo, mwaka 1427H.

[132] Angalia Swahihul-Bukhariy Juz 7 Uk 128

[133] Sahihi ya Bukhariy Juz 1 uk 12. Na Swahihi-Muslim Juz 7 uk 2. Pia angalia “mlango wa kuomba ruhusa” Juz 5 Uk 52.

mlioamini! Jiepusheni sana na (kuwadhania watu dhana (mbaya) ni dhambi. Wala msipeleleze (habari za watu). Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine. Je! Mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, hapendi; (basi na haya msiyapende). Na mcheni Mwenyezi Mungu bila shaka Mwenyezi Mungu ni mwenye kupokea toba (Na) mwingi wa rehema). Suratu Al-Hujurat, aya (11-13). Mwenyezi Mungu Mtukufu ametilia mkazo udugu wa kiislamu katika neno lake aliposema: - (Kwa hakika waislmu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu (msipuuze jambo la kupatanishana) ili mrehemewe). Suratu-Al-Hujurat, aya ya (10).

(Na ikiwa makundi mawili katika waislamu yanapingana, basi fanyeni suluhu baina yao; na likiwa moja ya hayo linamdhulumu mwenziwe, basi lipingeni lile linaloonea mpaka lirudi katika amri ya Mwenyezi Mungu na kama likirudi, basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaohukumu kwa haki). Suratu Al-Hujurat, aya ya (9).

Vilevile, pia amekataza kusengenya[134] na kudharau watu, baadhi yao kuwadharau wengine (Inamtosheleza mtu kuwa amefanya shari (jambo ovu) kumdharau ndugu yake muislamu. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu mtukufu: - (Wala usiwatazame (usiwafanyie watu jeuri), kwa upande mmoja wa uso, wala usiende katika nchi kwa maringo; hakika Mwenyezi Mungu Hapendi kila ajivunae, ajifaharishae). Suratu Luqman, aya (18).

---

[134] Sunanu-Tirmidhiy “kitaabul-birri” mlango wa “yaliyokuja katika kusengenya” Juz 4 uk 491. Pia Tirmidhy katika Kitaabul-birr, mlango wa 18 juzuu 4/325, Ahmad katika Musnad yake, juzuu ya 3/491.

(Enyi mlioamini! mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika waliowauwa (muungwana kwa muungwana, mtumwa kwa mtumwa, mwanamke kwa mwanamke, na anaesamehewa na ndugu yake aliyeumia) basi ashikwe kulipa kwa wema; na yeye alipe (na kulipishwa) kwa ihsani. Hiyo ni tahafifu itokayo kwa mola wenu na ni rehema. Na atakayeruka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu iumizayo). Suratu Al-Baqara, aya (178).

Pia kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: - (Na wasiape wale wenye mwendo mzuri (wa dini) na wenye wasaa (katika maisha yao) miongoni mwenu (wasiape kujizuia) kuwapa walio jamaa na maskini na waliohama kwa njia ya Mwenyezi Mungu na wasamehe; na waachilie mbali (wapuuze yaliyopita, linalopita hupishwa) Je, nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa msamaha (na) mwingi wa rehema (Basi na nyinyi sifikeni kwa sifa hizi). Suratu-Nur, aya (22). Na neno lake Mtukufu: (Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa (ya) ubaya huo; lakini anaesamehe na kusuluhisha ugomvi, ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu; bila shaka yeye hawapendi madhalimu). Suratu Ash-Shura, aya (40). Pia neno lake Mtukufu: (Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Ondosha (ubaya unaofanyiwa kwa wema); tahamaki yule ambae baina yako na baina yake kuna uadui atakua kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu) Suratu Fusswilat, aya (34). Na neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Ambao hutoa katika (hali ya) wasaa na katika (hali ya) dhiki na wazuiao ghadhabu na wasamehe watu (na) wawafanyiao ihsani), na Mwenyezi Mungu Anawapenda wafanyao ihsani) Suratu Al-Imran, aya ya (134).

Usawa wote huu na kuwaheshimu wengine na kufanya istahi (kupatanisha) kati ya wanaoteta ni kwa ajili ya kujenga jamii ya

kiislamu yenye tabia iliyoungika na kushikamana pamoja. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: (hakuna heri katika mengi wanayoshauriana kwa siri isipokuwa (mashauri ya) wale wanaoamrishwa kutoa sadaka au kufanya mema au kupatanisha baina ya watu. Na atakaefanya hivi kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu basi tutampa ujira mkubwa). Suratu-An Nisaa, aya (114). Na kwa hakika Mwenyezi Mungu amemuamrisha Mtume wake kua na huruma, na akamuusia jambo hilo na akawaamrisha watu kuusiana kwa hilo. Na hakika ni kama alivyosema: (Kisha awe miongoni mwa walioamini na wakausiana na kusubiri na wakausiana kuhurumiana) Suratu Al-Balad, aya (17). Ni kama alivyosema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam): "Hakika Mwenyezi Mungu anawaonea huruma wale wenye huruma (wenye kuonea watu huruma) katika waja wake"[135], pia anasema (Swallallwaahu Alaihi Wasallam): "Wenye kuonea watu huruma naye Mwenyezi Mungu anawaonea huruma, na waoneeni huruma wale walioko aridhini, nanyi atawahurumia yule aliyeko mbinguni".[136] Aidha ametilia mkazo kuoneana huruma kwa jumla kati ya wasliamu na huruma ienee jamii yote ya waislamu, kwa kusema: "Mfano wa waislamu katika kupendana kwao na kuoneana kwao huruma na kufanyiana upole ni kama mfano wa kiwiliwili, pindi kinapougua kiungo kimoja katika kiwiliwili hicho kinafuatia kiwiliwili chote

---

[135] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake "Kitaabul-janaaiz" mlango wa 33, katika neno lake Mtume, "maiti anaadhibiwa kwa kilio cha watu wake wanaomlilia" Juz 2 uk 81.

[136] Katika hadithi aliyoipokea Tirmidhy "Kitaabul-birr" mlango wa (16) Juz 4 Uk 324

(kushikwa na maumivu ya maradhi kwa kukesha na kwa homa)”.[137]

Kwa hakika swala ilikua ndio ibada yenye umuhimu mkubwa zaidi kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam), pamoja na hilo alikua anaihafifisha kwa sababu ya kuonea huruma watoto. Ni kama alivyopokea Bukhariy kutoka kwa Abu -Qataada (Radhwiallwaahu anhu) kutoka kwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) yakwamba alisema: “Hakika mimi ninaingia katika swala (mara nyengine) nikataka nirefushe nikasikia kilio cha mtoto nikahafifisha katika swala yangu kwa yale niyajuayo katika uchungu wa mamake kwa ajili ya kilio chake”.[138]

Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikua ana huruma hata na watumwa, kwa namna ambayo alikufanya kuwaacha huru ni katika wema mkubwa na ni katika milango ya kinga (ya kumkinga mtu kutokana na majanga au maafa) tofauti. Na pia uislamu umeubana mlango wa utumwa baada yakwamba ulikua wazi katika sharia zote na mipangilio mengine kabla ya zama za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam). Na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliusia kua watendewe mema kwa neno lake: “Hawa ni ndugu zenu wasaidizi wenu (katika kutengeza mambo yenu ya kikazi). Mwenyezi Mungu amewajalia kua chini ya milki yenu (mnawatamalaki) na kuwatumia, basi yule ambaye ndugu yake atakua chini yake na amlishe katika kile

---

[137] Ameipokea Muslim katika sahihi yake “Kitaabul-birr” katika mlango wa “yaliyokuja katika huruma za waislamu, kuhurumiana kwao na kusikitikiana kwao” Juz 8 Uk 20.

[138] Katika riwaya ya Bukhariy, katika sahihi yake, “kitaabul-aadhaan” mlango wa (65) “mwenye kuhafifisha swala yake” Juz 1 Uk.172. na ameipokea Imam Ahmad katika musnad yake Juz 3 uk 205.

anachokula na amvishe katika kile anachovaa, wala msiwakalifishe kazi wasioiweza na kama mtawakalifisha basi wasaidieni".[139] Pia alisema: "Mmoja wenu na asiseme kumwambia Mtumwa wake, mjakazi wangu wala kijakazi changu (mwanamke), wala na mtumwa naye asiseme bwana wangu (yaani kumuita na kumtukuza kwa jina la Mwenyezi Mungu) na nana wangu (mwanamke), lakini mwenye kummiliki mtumwa aseme kijana change na msichana wangu (wa kazi) naye mtumishi aseme bwana au bibi wangu, nyinyi wote ni watumwa na bwana ni Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu na utukufu".[140]

Kwa hakika kuoneana huruma huku na tabia za kibinadamu hazikuishia kwa waislamu na wanadamu peke yao, bali sharia ya kiislamu imezifikisha hadi kwa wanyama pia, ikakufanya kuwahurumia na kuwalisha na kuacha kuwaadhibu na kuwauwa bila ya huruma wala faida yoyote kuna ujira mkubwa; ni kama alivyosema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam): "Katika kila kiumbe chenye ini lenye umaji maji (uhai) kuna malipo (kwa kukifanyia wema)".[141] Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alisema: "Ambae haonei watu huruma naye hatahurumiwa (na Mwenyezi Mungu)".[142] Na kwa hakika pia

---

[139] Ahmad ibn Hanbal katika al-Musnad juz 2 uk 247. Pia ameipokea Bukhariy "kitaabul-iiman" mlango wa "kuwa maasia ni katika mambo ya kijahilia" Juz 1 Uk. 13.

[140] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake, hadithi nambari 2434. Pia ameipokea Muslim katika sahihi yake hadithi nambari 4275.

[141] Kutoka riwaya ya Bukhariy katika sahihi yake "Kitaabul-Musaaqaat" mlango wa "fadhila za kunywesha maji" Juz 3 uk 77.

[142] Ni hadithi Muttafakun-Alaihi katika riwaya ya Abi-Huraira. Angalia swahihi ya Bukhary "Kitaabul adab" mlango wa "kumuonea huruma mtoto na

alisema: “Mwanamke mmoja aliingia motoni kwa sababu ya paka aliyemfunga akawa hamlishi wala kumwachia akaenda kula vidudu vya aridhini hadi akafa kwa kukonda”.[143]

Kwa hakika pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alisema: “Mwenyezi Mungu amemlaani yeyote aliyekichukulia kitu chochote chenye roho kua ndio lengo lake (kukiadhibu)”.[144]

Katika mafundisho haya yote ya Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) katika haki za wanyama, uislamu umeutangulia ulimwengu wa kileo kwa karne nyingi, nayo ni katika rehema za Mwenyezi Mungu aliyowawekea sharia waja wake waumini wanaofata muongozo wake, ili wawe ni rehema kwa viumbe hai wote seuze wanadamu. Na pia uislamu umetilia nguvu juu ya kusaidia watu na kusimama pamoja na wenye mahitaji kati yao, na kuwaondolea udhia kutokana na watu wengine, waume kwa wanawake, akasema Mwenyezi Mungu katika aya tofauti zinazoungana kama alivyosema: (Na wasiape wale wenye mwenendo mzuri (wa dini ) na wenye wasaa (katika maisha yao) miongoni mwenu (wasiape kujizuia) kuwapa walio jamaa na maskini na waliohama kwa njia ya Mwenyezi Mungu, Na wasamehe na waachilie mbali (wapuze yaliyopita, linalopita hupishwa ) Je, nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni

---

kumbusu na kumpiga kamamba” Juz 7 Uk 75, na pia angalia Swahihi ya Muslim hadithi nambari 4282.

[143] Ameipokea Bukhariy katika Sahihi yake “Kitaabul-musaaqaat” Juz 3 uk 77. Pia ameipokea Muslim katika Sahihi yake, katika mlango wa “uharamu wa kumuadhibu paka na mfano wake”. Juz 8, uk 35.

[144] Amepokea imam Ahmad katika musnad yake Juz 1 Uk 216, pia ameipokea Muslim katika sahihi yake “Kitaabul-abiidi” mlango wa “kukataza kuwahasi wanyama” juz 6 uk 73.

? Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa msahama (na) mwingi wa rehema. (Basi na nyinyi sifikeni kwa sifa hiyo.) Bila shaka wale wanaowasingizia wanawake waliotakasika, wasiojua (maovu) waislamu (wenye kuwasingizia watu hawa) wamelaniwa katika dunia na akhera, nao watapata adhabu kubwa, siku amabyo zitawashuhudia ndimi zao na mikono yao na miguu yao kwa yale waliyokuwa wakiyafanya. Siku hiyo Mwenyezi Mungu atawapa sawasawa malipo yao ya haki. Na watajua kwamba Mwenyezi Mungu ndie (Mwenye kulipa kwa) haki iliyo dhahiri). Suratul An-Nur, aya (22-25).

Pia Qur'ani imetilia mkazo kuamiliana vizuri na jirani na kumfanyia wema[145] kama Mwenyezi Mungu alivyosema: (Mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote na wafanyieni ihsani wazazi wawili, na jamaa na mayatima na maskini na jirani waliokaribu na jirani walio mbali na rafiki walio ubavuni mwenu na msafiri aliyeharibikiwa, na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kulia (kuume) Bila shaka Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wajionao. Suratu An- Nisaa, aya (36).

Pia ni kama alivyosema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) "Yeyote anaemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho basi asimuudhi jirani yake".[146] Na pia alisema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) "Hakuacha Jibril (Alaihis,salaam) kuwa ananiusia kuhusu jirani mpaka nilidhani

---

[145] Imam Bukhariy ameweka katika Sahihi yake mlango wa kuusia majirani, Juz 7 uk 78. Nayo ni hadithi Muttafakun-alayhi.

[146] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake mlango wa "anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na asimuudhi jirani yake" Juz 7. Na haditi hiyo ni Muttafaku-alaihi

kuwa atamrithisha".[147] Kama alivyosema tena: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu hawi muislamu, Naapa kwa Mwenyezi Mungu hawi muislamu, Naapa kwa Mwenyezi Mungu hawi muislamu", ikasemwa ( kuulizwa ) "Ni nani huyo ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu" akasema: "Yule ambae jirani yake hana amani na shari zake".[148] Wala jambo hili halikuishia kwa waislamu peke yao lakini imelifikisha hadi kwa wasiokuwa wao. Katika jambo lilo wazi na lilo bayana katika uzuri wa kuamliana nao ikawa ni katika wale waliowekeana mkataba (na kuishi nao kwa amani). Katika neno la Mwenyezi Mungu: (Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwawafanyia ihsani na uadilifu wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakukufukuzeni katika nchi zenu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao uadilifu). Al-Mumtahina, aya (8). Na kwa hakika pia Mwenyezi Mungu ameamrisha kuwafanyia hisani mateka wa vita vya Badri na wasiokua hao katika washrikina. Waislamu walikua wanawalisha katika wanachokula na wanafanya nao muamala mzuri, jambo ambalo liliwaathiri likawapelekea kusilimu baada ya hapo.[149]

Miongoni mwa tabia nzuri ambazo umejengwa nazo uma wa kiislamu ni ukarimu na kutoa.[150] Na jambo la kutoa limejulikana

[147] Ameipokea Bukhariy katika kitabu chake "mlango uliokuja katika kumuusia jirani" juz 7 uk 78. Na haditi hiyo ni Muttafaku-alaihi.

[148] Ameipokea Bukhari katika sahihi yake, mlango wa "madhambi ya ambae kwamba majirani hawapati amani kutokana na vitimbi vyake" juz 7 uk 78. Na haditi hiyo ni Muttafaku-alaihi.

[149] Angalia Abul-Aziz al Umariy "mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa mitume- dini na dola- (vita vya Badri) sehemu ya 3 uk 607.

[150] Imam Bukhariy ameweka katika sahihi yake katika "Kitaabul-adab" mlango wa "tabia njema na ukarimu na yale yaliyofanywa kuwa makuruhu katika ubakhili" Juz 7 Uk 81.

katika uma wa kiislamu katika nyanja mbali mbali na katika hizo, ni kutoa kwa mali sawa sawa iwe ni katika kutoa zaka au swadaka ambayo imeambatanishwa pamoja na swala katika sehemu Zaidi ya moja, na katika hilo ni neno lake Mwenyezi Mungu mtukufu. (Kwa hakika binadamu ameumbwa, hali yakua mwenye papatiko. Inapomgusa shari huwa mwenye fazaa. Na inapomgusa kheri huwa anaizuilia, ila wanaosali (hao hawana sifa mbaya hiyo) ambao wanadumisha sala zao. Na ambao katika mali yao iko sehemu maalumu kwa ajili ya aombae na anaejizuilia kuomba (japo muhitaji). Na ambao wanasaidikisha siku ya malipo). Al-Maarij, aya (19-26). Na pia amesema: (Yule anaetoa (zaka, sadaka na vinginevyo) na kumcha Mwenyezi Mungu na kusadiki jambo jema akalifuata tutamsahilishia njia ya kwenda peponi. Na afanyae ubakhili asiwe na haja ya viumbe wenzake, na akakadhibisha mambo mema (asiyafate) tutamsahilishia njia yakwenda motoni. Na mali yake hayatamfaa atakapokua anadidimia (motoni humo) ni juu yetu (kuwabainishia viumbe) njia ya kheri na njia ya shari na ni yetu sisi akhera na dunia). Suratu Al-layl, aya (5-13). Na neno lake Mwenyezi Mungu: (Si juu yako kuwaongoa lakini Mwenyezi Mungu humuongoa amtakaye, juu yako ni kuongoza tu na mali yoyote mtakayoyatoa ni (faida) kwa nafsi zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na mali yoyote mtakayotoa mtarudishiwa kamili (thawabu zake) wala hamtadhulumiwa). Al-Baqara (272).

Pia neno lake Mwenyezi Mungu: (Enyi mlioamini toeni katika vile tulivyokupeni kabla haijafika siku ambayo hapatakua kujikomboa wala urafiki (wa kusaidiana) wala uombezi. Na walio kufuru ndio waliojidhulumu (kweli kweli)). Al-Baqara (254). Na katika hadithi tukufu, amesema Mtume (Swallallwaahu Alaihi

Wasallam) “Hakika Mwenyezi Mungu ni mkarimu anapenda ukarimu”.[151] Na katika njia ya kuondosha vinyongo na kuhusudiana na kujiepusha na vita kwa ajili ya mali alisema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam): “Jiepusheni na dhuluma, bila shaka dhulma ni giza siku ya kiama, na uogepeni ubakhili kwa hakika ubakhili uliwaangamiza waliokuweko kabla yenu, uliwapelekea kumwaga damu zao wakahalalisha walioharamishiwa”.[152] Maelekezo haya matukufu katika kuujenga umma na jamii katika ukarimu na utoaji (kujitolea) alikua Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akiyafanya katika maisha yake na kupitia mwendo wake mpaka ikajulikana kua yeye ni mkarimu kuliko yoyote yule aliyeko juu ya ardhi. Alikua anahimiza kutoa sadaka hata kama ni ya kitu kichache (kidogo), akasema: “uogopeni moto hata kama ni kwa kokwa ya tende).[153] Na kwa hakika walikua waislamu katika zama zake (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) wanashindana katika kutoa sadaka na kutoa kwa ajili ya kuwapa wasiojiweza katika waisilamu na kuyaandaa majeshi yao na kuwakirimu wageni wake Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam), wakitanguliwa na Uthmaan ibn Affaan alieandaa jeshi la wakati wa uzito.[154]

---

[151] Katika riwaya ya Tirmidhiy katika sahihi yake “kitaabul-adab” hadithi nambari 2799.

[152] Ameipokea muslim katika sahihi yake “Kitaabul-birri” mlango wa “kuharamisha dhulma” Juz 8 Uk 18. Na pia imam Ahmad katika musnad yake Juz 2 Uk 160.

[153] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake “kitaabuz,zakaat” mlango wa “uogopeni moto hata kama ni kwa kokwa ya tende” Juz 2 Uk 114

[154] Angalia Abdul-Aziiz al-Umariy “mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa manabii-dini na dola- (vita vya Tabuk) Sehemu ya 3 Uk 817.

Aidha kama ilivyokua kutekeleza ahadi ni katika tabia muhimu za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) na waislamu wote alilitekeleza hilo kwa marafiki zake pamoja na maadui wake na aliijenga jamii ya kiislamu juu ya jambo hilo. Amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: (Sio wema tu ( huo peke yake ) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi (katika kusali, yako na mengine) bali wema hasa ni wa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na Malaika na kitabu na manabii na wanawapa mali juu ya kuwa wanayapenda – jamaa na mayatima na maskini na wasafiri (walioharibikiwa ) waombao na katika (kuwakomboa) watumwa na wakawa wanasimamisha sala na kutoa zaka na watekelezao ahadi zao wanapoahidi, na wavumiliao katika shida na dhara na (katika) wakati wa vita; Hao ndio waliosadikisha (uislamu wao); na hao ndio wamchao Mungu (Mtukufu)). Al-Baqara, aya (177). Na neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Enyi mlioamini tekelezeni wajibu wenu mumuehalalishiwa wale wanyama wenye miguu minne, ila wale mnaosomewa (kuwa ni haramu). Lakini msihalalishe kuwinda mkiwa katika Hijja. Hakika Mwenyezi Mungu anahukumu apendavyo). Al-Maida, aya (1). Na kwa hakika alikuwa Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) akiweka amana na akiahidiana na idadi kubwa ya makabila pambizoni mwa mji wa Madina, na anawatekelezea ahadi zao kama alivyowawekea ahadi baadhi ya mayahudi wakati alipofika mji wa Madina na akawatekelezea ahadi mpaka baadhi yao walipofanya hiana. Na kwa hakika aliweka ahadi (mkataba) na Maqureish katika suluhu ya Hudaibiyyah, na akawatekelezea ahadi yao japokua ilikuwa dhahiri ndani ya mkataba huo kuna

dhuluma kwa baadhi ya wanyonge katika waislamu.[155] Na wakati inapotokea hiana kutoka moja ya pande mbili zilizowekeana mkataba, uislamu umeamrisha kuitupilia mbali ahadi hiyo na kulitangaza waziwazi jambo hilo, sio kufanya hiana kama wao wanavyofanya. Ndipo Mwenyezi Mungu akasema :( Na kama ukiogopa hiana kwa watu (mliofanya nao ahadi) basi watupie ahadi yao kwa usawa; hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wafanyao hiana) Suratul-Anfal, aya (58). Na ameamrisha kutekeleza ahadi wala hakuivunja, na ameamrisha kuukamilisha muda wa ahadi hiyo, na imekuja katika Suratu Attauba katika neno lake Mwenyezi Mungu mtukufu: ((Hili ni ) tangazo la kujitoa katika dhima (ahadi) litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa wale, mlioahidiana nao miongoni mwa washirikina (waambieni) "Basi tembeeni katika nchi miezi minnne ( kwa salama, kisha vitakuwa vita baina yenu na sisi ) na jueni yakwamba nyinyi hamuezi kumshinda Mwenyezi Mungu, na kwamba Mungu ndie mwenye kuwadhalilisha makafiri. Na ni tangazo litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kujuvywa watu siku ya Hijja kubwa kwamba Mwenyezi Mungu yu mbali na washirikina, na pia Mtume wake (yu mbali nao) Hawana haja na ahadi zao. Basi kama mkitubu ndio heri kwenu, na kama mkikengeuka, basi jueni kwamba nyinyi hamuezi kumshinda Mwenyezi Mungu. Na wapashe waliokufuru habari ya adhabu iumizayo (inayowangoja) isipokuwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa hao washirikina, kisha hawakukupunguzieni chochote wala hawakusaidia yeyote juu yenu, basi watimizieni ahadi yao mpaka muda wao. Hakika

[155] Ameipokea Abu-Daud katika Sunan yake, Hadithi nambari 2758.

Mwenyezi Mungu anawapenda wanaomuogopa). Suratu At-Tauba, aya (1-4).

Pia ni kama ilivyokuwa kutekeleza amana ni katika msingi na tabia (njema) ambayo umejengewa nayo umma wa kiislamu. Amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: (kwa yakini sisi tulizidhihirisha amri zetu na makatazo yetu (tukaziuliza mbingu na ardhi na milima (kua zitachukuwa madaraka ya kufuata amri hizo na kujiepusha na makatazo hayo ili zipate pepo zikifuzu, na moto zikifeli) vikakataa kuichukua ahadi hiyo) na vikaogopa, lakini mwanadamu akaichukua. Bila shaka yeye ni dhalimu mkubwa (wa nafsi yake kwa kua amechukua dhamana hii wala haitekelezi) mjinga sana). Al –Ahzab, aya (72). Na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa ni mtu wa kupigiwa mfano kwa maqureish kabla ya kutumilizwa kwake na baada ya kutumilizwa, mpaka walikua wakimuita mwaminifu, na ukweli ulikua ndio tabia yake, amemsifu nao Mwenyezi Mungu Katika kauli yake (Na aliyeleta ukweli na aliyekusadikisha hao ndio wamchao Mwenyezi Mungu). Suratu Az-umar, aya (33). Na alikua (Alaihissalaam) anahimiza ukweli na anawaamrisha (maswahaba wake) na anawalea watu kwa ukweli ndipo akasema: “Jilazimisheni na ukweli, bila shaka ukweli unamuongoza (mtu) kunako wema, na wema unaongoza kunako pepo. Na hataacha mtu kua anasema ukweli na anapupa nao mpaka anaandikwa mbele ya Mwenyezi Mungu kua ni msema kweli. Na jitahadharini na urongo kwa kua urongo unampelekea mtu kunako uovu, na bila shaka uovu unampelekea mtu kuingia motoni na mtu hataacha kusema urongo na kua na pupa ya kusema urongo

mpaka aandikwe kwa Mwenyezi Mungu kua ni mrongo”.[156] Kama ambavyo pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) Ametahdharisha kusema urongo, kwa neno lake: “Dalili za mtu mnafiki ni tatu akizungumza husema urongo na akiweka ahadi hukhalifu (hatakelezi) na akiaminiwa hufanya hiana”.[157]

Ama katika nyanja za kijamii na kifamilia uislamu umejitolea kuzijenga kwa kuzingatia tofauti na kugongana kwa mafungamano, na kwa hilo ndipo ikaletwa sharia na kuamrishwa kuifata katika nyanja za mambo yanayohusu wanadamu na sharia za kifamilia, yakiwemo mafungamano ya ndoa na talaka na yanayoyafuatia katika ugomvi na matumizi ya vyombo, malezi, kunyonyesha, ulinzi na majukumu mengine. Na ukaweka katika hayo haki zilizo wazi na mipaka (ya kisharia) inayochungwa kutoka pande zote, mmoja asimdhulumu mwengine na asifanye uadui juu ya haki ya mtu mwengine. Na Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) amewatahadarisha waisilamu kuiruka na kuivunja mipangilio hiyo na kanuni za ki Mwenyezi Mungu. Na huenda yale yaliotajwa katika Suratul-Baqara katika hukumu hizo na mipaka hiyo inabainisha umakinifu wa kimipangilio katika nyanja hizi. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Kwa wale wanaoapa kwamba watajitenga na wake zao (muda wao) ni kungojewa miezi minne. Na kama wakirejea (wakatangamana na wake zao) basi Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu. Na wakiazimia kuwaacha basi Mwenyezi

[156] Ameipokea Muslim katika sahihi yake “Kitaabul-birri wasswilah” mlango wa “ubaya wa urongo” Juz 8 Uk 29.

[157] Ameipokea Bukhariy “Kitaabul-iiman” mlango wa “alama za mnafiki” Juz 1 Uk 14. Pia ameipokea Muslim katika sahihi yake “Kitaabul-Iiman” mlango wa “aya za mnafiki ni tatu” Juz 1 Uk 56.

Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua na wanawake walioachwa wangoje (wasiolewe) mpaka tahara tatu zishe wala haiwajuzii kuficha (mimba) aliyoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao ikiwa wanamwamini Mwenyezi Mungu ns siku ya mwisho. Na waume wao wana haki yakuwarejesha katika muda huo kama wakitaka kufanya sulhu nao (wanawake) wanayo haki kwa sharia (kufanyiwa na waume zao) kama ile haki iliyo juu yao kuwafanyia waume zao. Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu (na) mwenye hikima.

Talaka (unazo weza kumrejea mwanamke) ni zile zilizotolewa mara mbili (za kwanza) kisha ni kumweka kwa wema na kumwacha kwa ihsani (wala usiwaze kumrejea tena mpaka aolewe na mume mwengine madam ametimiza mara tatu katika kumwacha akimrejea). Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa (wake zenu) isipokuwa (wote wawili) wakiogopa ya kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu hapo itakuwa hapana dhambi kwao (mwanamume wala mwanamke katika) kupokea (au kutoa) ajikomboleacho mwanamke. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi msiiruke na watakaoiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu hao ndio madhalimu (wa nafsi zao). Na kama amempa talaka ya tatu basi mwanamke huyo si halali kwake baada ya hapo mpaka aolewe na mume mwengine. Na mwanamume huyo mwengine akimwacha basi hapo hapana dhambi kwao mume yule wa kwanza na mwanamke huyo kurejeana wakiona watasimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na hii ni mipaka

ya Mwenyezi Mungu anayoibanisha kwa watu wajuao (wanaotaka kujua)

Na mtakapowapa wanawake talaka, na wakafikia kumaliza eda yao, basi warejeeni kwa wema au tokaneni nao kwa wema. Wala msiwaweke kwa kuwapa dhara mkaruka mipaka. Na atakayefanya hivyo, amejidhulumu mwenyewe. Wala msizifanyie mzaha aya za Mwenyezi Mungu na mkumbuke neema za Mungu zilizo juu yenu, na (khasa ile neema ya) kuteremshiwa Qur'an na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu.

Na mtakapowapa wanawake talaka (ya kwanza au ya pili) msiwazuie kuolewa (au kurejewa) na waume zao endapo baina yao wamepatana kwa wema. Hayo mnaonywa nayo yule miongoni mwenu anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hivyo ni mazuri mno kwenu na safi kabisa. Na Mwenyezi Mungu anajua lakini nyinyi hamjui.

Na wanawake waliozaa wanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili, kwa anayetaka kukamilisha kunyonyesha, na ni juu ya baba (yake) kwa sharia. Wala haikalifishwi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya wasaa wake. Mama asitiwe taabuni kwa ajili ya mtoto wake. Na juu ya mrithi (inapokuwa baba kafa) ni kama hivyo. Na kama wote wawili wakitaka kumuachisha ziwa (kabla ya miaka miwili), kwa kuridhiana na kushauriana, basi si kosa juu yao. Na kama mkitaka kuwapatia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha (wengine wasiokuwa mama zao) basi haitakuwa dhambi juu yenu kama mkitoa (kuwapa hao wanyonyeshaji) mlichowaahidi kwa sharia, na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ana habari ya yote mnayoyatenda.

Na wale wanaofishwa (wanaokufa) miongoni mwenu na kuacha wake, hawa (wake) wangoje (wasiolewe) miezi mine na siku kumi. Na wanapofikia mda wao (wa kumaliza eda yao hiyo), basi si dhambi juu yenu kwa yale wanayofanyia nafsi zao (hao wanawake) kwa yanayowafiki (kufuata) sharia. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za yote mnayoyatenda. Wala si dhambi kwenu katika kupeleka habari ya posa kwa ishara tu (si kwa maneno) kuwaowa wake (walio edani), wala (hapana dhambi pia) katika kutia katika nyoyo zenu azma (za kuwaoa). Mwenyezi Mungu anajua kwamba nyinyi mtawakumbuka. Lakini msifunge nao ahadi kwa siri (ya kuwaowa maadam eda haijaisha), isipokuwa mseme maneno yaliyo mazuri. Wala msiazimie kufunga ndoa mpaka muda ulioandikwa (katika eda) ufike mwisho wake. Na jueni yakwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo katika nafsi zenu, basi mwogopeni. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe (na) mpole sana.

Si dhambi kwenu kama mkiwapa wanawake talaka ambao hamjawagusa au kuwabainishia mahari (yao). Lakini wapeni cha kuwaliwaza (kitoka nyumba) mwenye wasaa kadiri awezavyo, na mwenye dhiki kadiri awezavyo. Matumizi hayo (wanayopewa) yawe kama inavyosema sharia. Ndio wajibu kwa wafanyao mema.

Na kama mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea hayo mahari (makhsusi), basi (wapeni) nusu ya hayo mahari mliyoagana, isipokuwa wanawake wenyewe waache (ile nusu wasitake kitu) au yule (mume) ambaye kifungo cha ndoa ki mikononi mwake aache (haki yake ampe mahari kamili). Na kuachiana ndiko kunakomkurubisha mtu sana na kumcha Mungu. Wala msisahau kufanyiana ihsani baina yenu, hakika Mwenyezi

Mungu anayaona yote mnayoyafanya). Suratul-Baqara aya (226-237).

Kwa hakika imekuja misingi mengine tofauti kuhusu mambo yanayofungamana na ndoa, kuanzia kuposa hadi kuachana na kuwaamrisha waume kuwa na tangamano zuri. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Enyi mlioamini si halali kurithi wanawake kwa jeuri wala msiwazuiye (kuolewa na waume wengine kwa kuwa hamuwataki, wala hamtaki kuwaacha ila kwa pesa) ili mpate kuwanyanganya baadhi ya vile mlivyowapa. (Hapana ruhusa haya) isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi. Na kaeni nao kwa wema kama mkiwachukia basi (Msiwaache) kwani huenda mkachukia kitu na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake). An-Nisaa Aya (19). Na sura hii imeitwa kwa jina la *An-Nisaa* (Wanawake) ili kutaka (kuinua) heshima yao katika jicho (nadharia) ya familia, kama ambavyo kwamba sharia imemfanya mwanamke ni mwakilishi wa mama (katika kazi na jukumu lake) ni mtu mwenye thamani na anayestahiki Zaidi kutendewa wema mbele ya mwanadamu. Na uislamu umeyafanya maisha ya kindoa yamesimama juu ya mapenzi na huruma na utulivu nayo ndio maana makubwa ya neno mapenzi. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na katika ishara zake za kuonyesha ihsani yake juu yenu) ni kuwa Amekuumbieni wake zenu kutoka jinsi yenu ili mpate utulivu kwao naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika haya zimo ishara kwa watu wanaofikiria) Suratur-Rrum, aya (21).

Pia mume ameamrishwa kuwafanyia mzaha ahli yake na kumchezea mkewe (kwa ajili ya kutia furaha na mapenzi kwa maneno na vitendo hivyo) na kujipendekeza kwake, na

mwanamke nae ameamrishwa kumtii mume wake,[158] na pia hukumu za kisheria zimekuja (zimeleta) amri ya kuharamisha uhusiano wa kijinsia (kati ya mume na mke) na kufanya mambo yanayopelekea uhusiano ulio nje ya duara ya uke na uume, kwa yale yanayopatikana kwa kufanya hivyo katika kuwakosea wale wanaozaliwa pasi yakuwa na baba katika kuudhoofisha uhusiano wa kindoa na kuwaharibu wanawake kwa waume wao na wanaume kwa wake zao, pamoja na kuzidisha kuchangia maradhi ya kiwiliwili. Na uislamu umeuzingatia uzinifu katika jumla ya makosa makubwa, na zaidi ya hilo ni kua umemuamrisha mwanadamu awe mke au mume, kuinamisha macho yake, asiangalie isipokuwa wale aliohalalisha Mwenyezi Mungu (Mtukufu) katika wake na waume na mahirimu yake mtu (mtu asiefaa kuoa au kuolewa nae). Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Waambie waislamu wanaume wasitazame yaliokatazwa), na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; bila shaka Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) wanayoyafanya na waambie waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasividhihirishe viungo vyao isipokuwa vinavyodhihirika (nao ni uso na vitanga vya mikono -na wengine wanasema na nyayo-) Suratu An-Nur, aya (30-31). Na aya hizi zimekusanya mambo ya matendo na tabia ambazo zinamfanya mwanamume asimuangalie isipokua ahli yake na vile vile mwanamke pia. Wala kuwaangalia wengine hakuwi sababu ya kumuepusha mwanadamu na sababu yoyote inayopelekea kunako mahusiano yalioharamishwa, lakini kujizuia na kuangalia (huko) ni hatua ya kujikinga kwanza na ni tiba iliotangulizwa ili kuleta kuaminiana baina ya wanandoa. Na katika wakati ambao Mtume

---

[158] Al-Kamadaaniy: Fannu taamullin-Nabiyy fil-hayaatiz-zaujiyya. Uk 60

(Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliijenga jamii ya kiislamu juu ya tabia njema bila shaka pia alitahadharisha tabia mbaya zikiwemo kuwadhulumu watu, kama ilivyo katika kauli yake Mwenyezi Mungu: Basi bila shaka wamekukadhibisheni (hao waungu wenu) kwa yale mlioyasema ; na hamtaweza kujiondolea (adhabu) wala (kupata) msaada. Na atakayefanya mabaya miongoni mwenu tutamuonjesha adhabu kubwa Suratu Al-furqaan, aya (19). Na pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) amesema: (iogopeni dua ya mwenye kudhulumiwa kwa hakika (dua hiyo) haina pazia[159] (kati yake (muombaji) na kati ya Mwenyezi Mungu (Mtukufu)). Pia sharia ya kiislamu imekataza uhasidi kama ilivyo katika neno lake Mwenyezi Mungu: (Au wanawafanyia watu husda kwa yale aliowapa Mwenyezi Mungu kwa ukarimu wake. Basi tuliwapa (vilevile) watoto wa Ibrahim kitabu na hikima na tukawapa ufalme mkubwa). An-Nisaa, aya (54). Pia sharia ya kiislamu imetahadharisha waislamu na kupunja watu na (kuwahadaa). Akasema Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) "yoyote atakayetupunja (kutuhadaa) si katika sisi (waisilamu)".[160] Pia uislamu umetahadharisha (kufanya jambo kwa kujionyesha) kama ilivyokuja katika neno lake Mwenyezi Mungu. (Basi adhabu itawathubutukia wanaoswali. Ambao wanapuza (maamrisho ya), swala zao (kama kuwafanyia wema viumbe wenzao). Ambao hufanya (amali zao ili watu wawaone tu) Nao hunyima msaada (Basi sala zao hazina faida kubwa kwao). Suratu Al-Mauun, aya (4-7). Aidha riyaa imetahadharishwa kwa neno

---

[159] Ameipokea Bukhariy katika sahihi yake "Kitaabul-madhwaalim" Mlango wa "Kuogopa dua ya aliyedhulumiwa" Juz 3 Uk 99.

[160] Ameipokea Muslim katika sahihi yake "Kitaabul-Iiman" mlango wa "Anayetupunja si katika sisi" Juz 1 Uk 69

lake Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) aliposema; “Hakika linalotia hofu zaidi katika ninayohofia juu yenu ni ushirikina mdogo”. Maswahaba wake wakamuuliza: “Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni upi huo ushirikina mdogo?” Akasema: “ni riyaa”.[161] Kama ambavyo pia amekataza kughurika na kujiona mtu (nafsi yake kuwa ni bora kuliko wengine ) nalo ni katika madhambi mazito yaangamizayo, kama alivyosema: “Mambo matatu ni katika yenye kuangamiza, ubakhili wenye kuchukiwa na matamanio yenye kufatwa na mtu kujiona nafsi yake (kua ni bora)”.[162] Na kwa hakika Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) ameamrisha yakwamba mtu asihadaike kwa mali yake, ibada yake, nguvu zake, utukufu wake au amali yake, wakasema “Na hata wewe pia ewe Mtume?”, Akasema; “Hata mimi pia isipokua Mwenyezi Mungu (Mtukufu) anifungamanishe na rehema zitokazo kwake, lakini wekeni sawa mambo, na kurubisheni, Wal,qasdu, al- qasdu (fanyeni mambo kwa kipimo, na upole) mtafika”.[163]

Pia Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anachukia uvivu na anajilinda nao, kama ilivyo katika neno lake: “Ewe Mwenyezi Mungu (Mtukufu) hakika mimi najilinda kwako na

---

[161] Ameipokea Imam Ahmad katika Musnad yake kutoka kwa Mahmuud Ibn Lubaid al-Answariy (Radhwiallwahu anhu). Juz 5 uk 428.

[162] Angalia Abu-Bakar al-Jazaairy, “Minhaajul-Muslim” uk 170. Pia angalia Ibnu-Qudaama al-Maqdasiy na mukhtaar ya Minhaajul-Qaaswidina. Uk 234.

[163] Ameipokea Muslim katika sahihi yake “Kitaabu swifatul-Qiyaama wal Jannatu-wannaar” mlango wa “lan yad,khula ahadukumul-Jannata bi-amalihi” Juz 8. Uk 139.

kulemewa na mambo na uvivu na uoga na ubahili na uzee”.[164] Huenda ikawa katika mambo muhimu yaliyoletwa na uislamu kwa jamii za kibinadamu, ni kuupa umuhimu wakati na kuupangilia na kutafautisha kati ya kazi za mchana na utulivu wa usiku, na kuutumia wakati katika mambo ya manufaa na kutokuupoteza katika mambo ambayo hayana faida. Na katika kugawanywa wakati wa swala na kuuwekea mipaka yake kwa umakini na upeo mkubwa, kunadhihirisha namna uislamu ulivyoupa umuhimu wakati, amabao ndio maisha ya mwanadamu na lengo lake katika kupangilia kwenye upeo, kuhusu siku yake na yale yanayofungamana nayo katika ibada na kazi, na yale anayoyahitaji katika mapumziko. Na haki ya mwanadamu juu ya nafsi yake katika mpangilio huu ni kama haki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya mwanadamu katika kutilia umuhimu mambo ya ibada na kupangilia wakati wake.

Ni jambo lililowazi kwa kila mwenye akili kuwa sharia hizi na utekelezaji wake kitabia katika zama za Mtume (Swallallwaahu Alaihi Wasallam), na kupitia sera yake, kuwa zimechangia katika mshikamano wa jamii, kuijenga na kuchanganyika kwake na mapenzi yake na yale yaliyoshariishwa (kufanywa kuwa ni sharia) na Mwenyezi Mungu Mtukufu (Aliyetukuka na kutakasika), na yale aliyokuja nayo Mtume wake Muhammad (Swallallwaahu Alaihi Wasallam).

---

[164] Ameipokea Muslim katika sahihi yake katika maandishi ya sifa za kiama na pepo na moto mlango wa kuonyesha kuwa “hatoingia peponi yeyote kwa amali yake” Juz 8 Uk 139

## HITIMISHO

Anasema ibnu-Khalduun: Mwanadamu ni raia kwa tabia yake, yaani hana budi na tangamano ambalo ndilo maana ya umiji katika istihali yao na ndio maana ya majengo. Na kwa hakika risala aliyoibeba Mtume (Swallallwahu alahihi wasallam) na kuitabikisha (kuifata kivitendo) katika maisha yake ni rehema kwa watu wote. Amesema Mwenyezi Mungu (Mtukufu): (Nasi hatukukutuma (kukuleta) isipokuwa ni rehema kwa wanadamu wote). Qur'ani Tukufu, Suratul-Anbiyaa aya (107).

Huenda baadhi ya watu wa zama hizi wakadhani kuwa kujihimu kwa kuzijenga jamii na kusimama kwake katika misingi ya kiraia na maendeleo ya kijamii ni jambo jipya au la kisasa.

Lakini tukiangalia kwa haraka na kiufupi kupitia matukio ya Mtume (Swallallwahu alahih wasallam) katika kuijenga jamii ya kiraia inatubainikia wazi katika matukio na mambo yanayoonekana yakwamba Mtume (Swallallwahu alahihi wasallam) alikuwa na pupa ya kuitikia haja za wanadamu zinazosimama juu ya kutangamana na kusaidiana kikamilifu katika maisha ya watu binafsi na ya jamii yote. Na maisha yote ya Mtume (Swallallwahu alahih wasallam) na jihadi yake katika nyanja zake zote, ni katika kujenga jamii ya kiraia, ambayo itampa amani mwenye kutaka amani, maisha yanayohifadhi utukufu wa mwanadamu katika jamii ya kiraia iliyoendelea. Kwa hakika kuupa mji wake mkuu jina la Madina badali ya jina lake la zamani (Yathriba) lenye maana ya lawama- kuna lengo kubwa, vilevile mkataba wa Madina ulihifadhi haki za wakazi na raia wake wote na kuikuza jamii inayokuwa kimakao kimaana, kielimu, na mambo ya kijamii, kiuchumi, kiidara na hata ki afya.

Aidha maisha yake yalikuwa na lengo la kupanga uadilifu kwa wakazi wote, uadilifu uliojitenga na ukabila na ukoo, yote hayo yalikamilisha mafundisho yake kwa watu na kuyatekeleza katika jamii ya kimadina mafundisho yaliyoendelea juu ya uadilifu, ndipo yakasahilisha mafungamano na kuyafanya kuwa mazuri kati ya watu, yakawaunganisha katika uabudiaji wa Mwenyezi Mungu (Mtukufu) wa kikweli.

Mwenyezi Mungu (Mtukufu) Amesema: (Musa) Akasema: Mola wetu ni yule aliyekipa kila kitu umbo lake kisha akakiongoza (kufuata kinachowafikiana na umbo lake hilo). Qur,ani tukufu, Suratu Taha, aya (20).

Inawapasa wasomi wa sera ya Mtume (Swallallwahu alaihi wasallam) kuitukuza hakika hii na kuifungamanisha na maana haya ya kibinadamu aliyoyataka bwana wa viumbe vyote, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Oh! Asijue aliyeumba! Naye ndiye avijuaye visivyojulikana na vinavyojulikana). Al-Mulk aya (14). Pia inawapasa wasomi wa sera ya Mtume (Swallallwaahu alaihi wasallam) kuidhihirisha na kudhihirisha kila linalogusa maisha ya mwanadamu kwa jumla, hasa maisha ya wanadamu wa kileo katika kufungamanisha kuliko wazi kunakoangazia kutoka katika sira ya Mtume (Rehema bora na amani za Mwenyezi Mungu zimshukie mwenye sera hizo).

## FAHARASA YA MATOLEO NA MAREJEO.

### KWANZA: MATOLEO


- Ibn-Ishaaq, Muhammad ibn Ishaaq ibn Yasaar al-Muttwalibiy la mwaka 151h
- Sera ya ibn Ishaaq inayoitwa kitaabul-Mubtada wal-mab,ath wal-maghaaziy. Iliyohakikiwa na Humaidullwaah chapa ya 2. Quniya: Turkiya: ambayo ni waqfu wa huduma za heri, mwaka 1401h
- Ibn Abi- Shaiba, Abu-Bakar Abdalla ibn Muhammad
- Al- maghaaziy, iliyohakikiwa na Abdul-Aziiz ibn Ibrahhim al-Umary chapa ya 1, Riyadh: Daaru eshbilia, mwaka 1421h
- Al-Bukhaariy, al-Haafidh Abi-Abdillaahi Ismael ibn-Ibrahiim ya mwaka 256h
- Swahiihul-Bukhaariy (Al- Jaami al-Swahiih) Riyadh: Daar eshbilia-Bairut:Daarul-fikri chapa ya 1, ya mwaka 411h.
- Al- balaadhiriy, Abul-Hasan Ahmad ibn- Yahya ibn Jaabir ibn Daud al-Baghdaadiy (toleo la mwaka 279h)
- Ansaabul-Ashraaf, Sehemu ya tatu, iliyohakikiwa na Abdul-Aziiz al-Dauriy, sehemu ya nne, uhakiki wa Ihsaan Abbaas- Bairut: mwaka 1398h na 1400h. Attirmidhiy Abu-Isa Muhammad ibn Isa ibn Saura (Toleo la mwaka 279h).
- Al-Jaami al-swahiih (Swahihu-Tirmidhy), iliyohakikiwa na Ahmad Mahmoud Shaakir-Bairut: Daaru Ihyaautturaathil-arabiy, haikuandikwa tarehe iliyotolewa.
- Ibnu- hajar Shihaabud-diin abul-Fadhli Ahmad ibn-Aliy ibn Muhammad al-Asqalaaniy (toleo la mwaka 852h)

- Al-iswaaba fii tamyiizis-swahaaba- Cairo: chapa ya Al-Sa,ada 1328h.
- Fat,hul-baariy Sharhu ya Swahiihul-Bukhaariy, imerejelewa na Abdur-Rauf Saad na wengineo- Cairo. Maktaba ya vitivo vya chuo cha Azhar mwaka 1398h.
- Ibn Hazmi, Abu_Muhammad Aliy ibn-Ahmad ibn Saad (Toleo la mwaka 384-486h)
- Hijjatul-Wadaai, uhakiki wa Abdul-haqi al-Turkumaaniy-Bairut: Daaru ibn Hazmi, mwaka 1429h
- Ibnu-Hambal, al-Imaam abi –Abdillaahi Ahmad. (toleo la 241 h)
- Musnad ya imam Ahmad- Bairut: Maktaba ya kiislamu mwaka 1398h
- Al-Khuzaaiy, abul-Hasan Aliy ibnu-Muhamad al-Tilimsaaniy.
- Takhriijud,dalaalati-assam,iyyaa alaa maa kaana fiy ahdir, Rasuul minal-hirafis-swanaai al-amaalaati,shariah, uhakiki wa Ahmad Mahmoud Abu-Salaama chapa ya 1-Cairo: majlis kuu ya mambo ya kiislamu mwaka 1401h
- Khalifa ibn-Khayyaat ibnu abi-Hubaira al-Laithiy al-usfuriy (mwaka 160-240h)
- Tarekhe ya khalifa ibn-Khayyaat, iliyohakikiwa na Akram Dhwiyaa ul-Umariy chapa ya 2- Bairut. Taasisi ya Al-rissaala mwaka 1398h.
- Abu Daud, Sulaimaan ibnul-Ash-ath al-ssajistaaniy
- Sunanu Aby Daud, iliyotiwa taaliq na Izat Ubair, chapa ya 1. Himswi Daarul-hadiith mwaka 1391 h.
- Ibnu Saad Muhammad ibn Maniiy al-Zuhriy (Toleo la mwaka 230h)

- Assiiratul-Nabawiyya kutoka katika Twabaqaitul-kubraa chapa ya 1 Cairo. Iliyochapishwa na Azzahraau – lil,iilamil,islaamiy al-arabiy mwaka 1409h.
- Al - twabaqaatul - kubraa, Bairut: Daaru - Swaadir (haikutajwa tarehe)
- Al-Ssamhuudiy, Nuuruddiin Aliy ibnu-Ahmad (mwaka 911.h.)
- Wafaaul – wafaai – bi,akhbaari Daarul - Mustwafaa, iliyohakikiwa na Muhammad Muhyiddiin Abdul-Hamiid chapa ya 3-Bairut: Daaru Ihyaaul-turaathil arabiy mwaka 1401.h.
- As-Suhailiy, Abdur-Rahmaan ibn-Abdalla ibn Ahmad al-Khuth,amiy (Toleo la mwaka 581.h)
- Al-raudhul-unuf katika tafsiri ya sera cha ibnu-Hishaam Dhwabti ya Twaha Abdur-Rauf Saad-Bairut: Daarul-maarifa mwaka 1398h.
- Assuyuutwiy Abdul-Rahmaan ibn-Abii-Bakari abul-Fadhli mwaka 911h.
- Taarikhul-khulafaa,uhakiki wa Muhyiddiin Abdul-Hamiid chapa ya 3-Cairo. Maktaba ya Madaniy mwaka 1383h.
- Ibnu-Shubba, Abu-Zaid Umar ibnu-Shaiba al-Numairiy al-Busriy (mwaka 264)
- Taarikhul-Madina iliyohakikiwa na Fahiim Shaikhul-Madinatul-munawarah: Imeenezwa na Assayyid Habiib Mahmoud Ahmad mwaka 1393h.
- Atwabariy: Abu-Jaafar Muhammad ibn Jariir (Toleo la mwaka 310h.)
- Taarikul-Umam wal-muluuk-Bairuut: Daarul-fikri (bila tarehe ya kuchapishwa)

- Al-fairuuz,abaadiy, Mujduddiin Muhammad ibn-Yaaquuub (toleo la mwaka 816)
- Sufrus-saada, kilichohakikiwa na Ahmad al-Ssaayih na umar Hamza, chapa ya 1, Cairo kituo cha Al-kitaab mwaka 1417h.
- Al-Qurtubiy Abdalla ibnu-Muhammad ibnu-Faraj al-maalikiy.
- Aq,dhwiatu Rasuulullwaahi. Dauha: chapa za Qatrul-watwaniyya (haikuandikwa tarehe ya kuchapishwa)
- Ibnul-Qayyim Muhammad ibnu-Abi-bakar al-Zuhriy al-Dimashqy (Toleo la mwaka 751)
- Zaadul-maad fiy, hadyi Khairul – ibaad, Bairut: Maktabatul - ilmiyya (haikuandikwa tarehe ya kutolewa kwake).
- Aalaamul-muwaqiien an-Rabbil-a’lamiin, imehakikiwa na Muhammad muhyiddiin Abdul-Hamiid-Bairut: Daarul-fikrul-arabiy (haikuandikwa tarehe ya toleo)
- Atturuqul-hakiimah-fiy al-ssiyaasatil –shar,iyyah, imehakikiwa na Muhammad Haamid al-Faqiy-Bairut: Daarul-kutubul-ilmiyya (haikutajwa tarehe ya toleo).
- Attwibbun-Nabawiy, uhakiki wa Abdul-Ghaniy Abdul-Khaaliq na wengineo-Riyadh: Maktabatul-Riyaadh al-hadiith (haikutajwa tarehe ya toleo)
- Ibnu-Kathiir, Ismeel ibnu-Kathiir Abul-fidaa al-dimashaqiy (toleo la mwaka 774.h)
- Assiiratun-Nabawiyya, uhakiki wa Mustwafaa Abdul-waahid- Beirut: Daarul-maarifa mwaka 1396h.
- Tafsiri ya Qur’anul-Adhwiim chapa ya pili- Riyadh: Daaru kunuuz eshbiliya. Mwaka 1430h.

- Ibnu-Maajah, al-Haafidh Abi-Abdillahi Muhammad Ibnu-Yaziid al-Qazwainiy (toleo la mwaka 207-275h.)
- Sunanu ibn-Maajah, uhakiki wa Muhammmad Fuaad Abdul-Baaqiy-Cairo: mwaka 1373h.
- Muslim, Al-imaam Abul-Hassan Muslim ibnul-Hajjaaj ibnu-Muslim al-Qushairiyya al-Naisabuuriyya (Toleo la mwaka 261h).
- Aljaamiu, swahiih-Bairut: Daarul-afaaqul -jadiidah (haikuandikwa tarehe ya toleo)
- Ibnu-Hishaam Abdul-Malik al-Muafiriy (toleo la mwaka 218).
- Assiiratun-Nabawiyya imehakikiwa na Mustwafaa al-Siqaa Ibrahiim al-Abyaariy na Abdul-Hafiidh shalbiy-Daarul-kunuuzil-adabiyya (haikutajwa tarehe ya chapa wala tarehe ya toleo).


## PILI- VITABU VYA MAREJEO


- Al-Haddaad Ahmad Abdul-Aziiz ibnu-Qaasim.
- Akhlaaqun-Nabiyyi fiyl- Qur,ani was-sunna,chapa ya 2 Daarul-gharbil-Islaamiy, mwaka 1416-1996m.
- Al-harbiy Muhammad ibnu-Ahmad ibn-Naaswir.
- Iqra-bismi-Rabbika chapa ya 1. Naadiy Jaizaanil-adabiy mwaka 1423h.
- Harakatai Ibrahiim.
- Assiyaasatu Wal-mujtamaa fiy,lasrin-Nabawiy-Daaru Afaaqul-jadiida mwaka 1990m.
- Humaidullaah Muhammad
- Majmuuatul-wathaaiqis-siyasiyya fil,ahdin-Nabawiy Wal,khilaafatur-Raashida chapa ya 4- Bairut: Daarun-nafaais ya mwaka 1403h.

- Al-khauliy, Muhammad Abdul-Aziiz.
- Al-adabun-Nabawiyy, chapa ya 1-Bairuut: Daarul-Qalam mwaka 1406h.
- Ashaamiy,Swaaleh.
- Min maeenissiira, chapa ya 1- Bairut: Al-maktabul-islaamiy mwaka 1405h.
- Uthmaan,Muhammad Fat’hiy.
- Min usuulilfikri’ssiyaasiy-al-islaamiy diraasatul-huquuqil-insaaniy Wal,waadhi Riaasatid-daula fiy dhwauis,shariiatil-Islaamiyya wat’uraathihaa al-Taariikhiy wal-fiqhiy, chapa ya 2- Bairut: Muassasatur-Risaalah mwaka 1404h.
- Al-Umary, Akram Dhwiyaau.
- Assiiratin-Nabawiyya asswahiiha chapa ya 3- Al-Madiinatul-munawarah: Maktabatul-Uluum wal-hikam mwaka 1425h.
- Al-Umariy, Abdul-Aziiz ibnu-Ibrahiim.
- Al-wilayatu al-al,buldaan fiy asri-lkhulafaair, Raashidiin chapa ya 3 Riyadh: Daaru-eshbilia mwaka 1422h.
- Al-hirafu Wasswinaati fil-hijaaz fiy asrir-Rasuul chapa ya 3 Riyadh: Daaru-eshbilyaa mwaka 1420h.
- Al-kamdaaniy, Adiib.
- Fannu taamulin-Nabiyyi fil-hayaatizzaujiyya-Damascus: Daarul-bashaairil-Islaamiyya mwaka 1425h.
- Maahir, Suaad.
- Masaajidu fiy siiratin-Nabawiyya-Cairo: Al-hai,atul-misriyyatul-a’mmatu lilkitaab mwaka 1987m.
- Muunis, Husein.
- Attaarikhus-swihiyy lilr-Rasuuli –Cairo: Daarul-maarif mwaka 2000m.

- Al-wazaan, Dr Adnaan ibnu-Muhammad ibnu-Abdul-Azziiz.
- Huquuqul-insaan fiyl-Islaam wasimaatihaa fil mamlakaatil-Aarabiyyati al-ssauudiyya chapa ya 1 Jalada la 5- Bairut: Muas,sasatur-Risaala mwaka 1425h.

## WASIFU WA MAISHA YA USTADH DR. ABDUL-AZIIZ IBN IBRAHIIM SULEIMAAN AL-UMARIY

- Ni katika wazaliwa wa mji wa Bureidah katika mamlaka ya kiarabu ya Saudia.
- Ni ustadh (mstaafu) wa masomo ya juu katika chuo kikuu cha kiislamu cha Imam Muhammad ibn Saud-Riyadh
- Mwanakamati wa jumuia za kishistoria za Saudia na za ghuba la Kiarabu
- Mwanakamati wa jumuiya ya masomo ya Mashariki ya kati ya kiamerika
- Mjumbe wa kamati ya kisayansi na kinyanjani ya ramani ya kihistoria ya sera ya Mtume (Swallallwahu alaihi wasallam) ya (kituo cha utafiti wa kihistoria cha Mfalme Abdul-Aziiz)
- Aliongoza warsha nyingi za kielimu katika America, Canada, Australia, New-ziland na Asia.
- **Ana Zaidi ya bahthi (utafiti) hamsini (50) zilizoenezwa na vitabu hamsini (50) vilivyochapishwa vikiwemo:**
  - Utawala wa kimiji katika zama za makhalifa waongofu.
  - Ufundi na viwanda katika Hijaaz zama za Mtume (Swallallwahu alaihi wasallam) kimechapishwa (chapa tatu)
  - Ufunguzi wa kiislamu katika zama nyingi. Kimechapishwa (chapa 5). Kimefasiriwa kwa Kiengereza na Kiurdu.
  - Al-Maghaaziy cha ibnu Abii-Shaibah (Masomo na uhakiki)
  - Vipengele vya usimamizi kiuchumi, kijamii na Teknolojia katika sera ya Mtume (Swallallwahu alaih wasallam)
  - Abu-Bakar ibnu Abii-Shaibah na athari zake za kihistoria.
  - Amani katika maisha ya Mitume (Alaihimus-salaam). Kimetafsiriwa kwa lugha ya ki Albania.
  - Tamaduni katika upanuzi wa kiislamu

- Mikakati ya kiraia na kijeshi zama za makhalifa waongofu.
- Misingi ya mipango na usimamizi katika sera ya Mtume (Swallallwahu alaihi wasallam)
- Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Manabii-dini na dola- (juzuu tano)
- Kuchagua kutoka katika sera ya Mtume mteule (Swallallwahu alaihi wasalam) ambacho ni (ufupisho wa kitabu “Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa manabii-dini na dola) kimefasiriwa katika lugha kumi na sita (16)
- Kujenga jamii ya kiraia na kuikuza katika sera ya Mtume (Swalallwahu alaih wasallam). Kimefasiriwa katika lugha kumi na mbili (12)
- Encyclopedia ya sifa za Mtume mteule (Juzuu saba)
- Uhusiano wa Mtume (Swallallwahu alaihi wasallam) na maeneo ya bara Arabu.
- Khalifa wa mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wa pili katika wawili, Abuu-Bakar As-swiddiiq (Radhwiallwaahu anhu). Kimefasiriwa katika lugha ya Kiurdu.
- Dhun-nuurain Amiirul-muuminina Uthman bin Affaan (Radhwiallwaahu anhu) mtu ambae malaika wanamuonea haya.
- Kipenzi cha waislamu na kiongozi wao al-shahiid Aliy ibn Abi-Twaalib (Radhwiallwaahu anhu) kipenzi cha waliowekwa karibu (na Mwenyezi Mungu). Kimefasiriwa kwa lugha ya Kiurdu.
- Miongoni mwa waasisi wa elimu Sheikh-Abdallah ibn Ibraahim ibn Suleim (Rahimahul-Lwaahu), sera, athari na historia.
- Mafanikio ya jukwaa la Al-Umariy la kitamaduni katika kukusanya, kuhakiki, kuandaa na kuandika (juzuu 13)

- Hati za kifamilia kutoka Buraidah na milki za mzee Ibrahiim ibn Suleim, sera, athari na historia (juzuu 2).
- Kumbukumbu zangu- kurasa kutoka katika maisha yangu.
- Misafara (matembezi) katika ulimwengu (juzuu 3)